# Nipashe

Jumatano Septemba 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581075

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




MOBETO HATAKI 'SHOBO' NA MTU

UKURASA 27


JACKPOT BABA LAO!

TZS. 346,249,820

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mufti** Zubery achukizwa na tabia wastaafu kuchanganya waumini

UKURASA 9



# Uamuzi mgumu kilio cha tozo

- **Wadau,** wasomi watoa maoni tofauti, wataka uchumi imara kwanza... *Endelea ukurasa 2*



"Kufuta baadhi ya tozo na kupunguza viwango vilivyokuwa vinatozwa ni jambo zuri, linawapa wananchi ahueni na kuongeza kasi ya kutumia huduma za kibenki.

**Mkurugenzi Mtendaji REPOA**



"Bado kuna malipo makubwa ya kodi kwenye miamala ya simu, wamebaki na ile ya mwaka jana, walitoa asilimia 30.

**Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji LHRC**



"Kodi za aina hii zinakatisha tamaa masuala ya uchumi wa kidigitali, kuziondoa tozo hizo kunachangia kasi ya uchumi wakidigitali.

**Prof. Samwel Wangwe, Mchumi Mbobevu**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**JELA KWA KUMKATA SHINGO MAMA MKUBWA**

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita...

UKURASA WA 7

**IGP WAMBURA AENDELEA KUFUMUA UONGOZI POLISI**

MKUU wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) Camilius...

UKURASA WA 7

**CRDB YAWAPA MAFUNZO MAALUM WAANDISHI HABARI**

BENKI ya CRDB imeendesha semina maalum kwa waandishi wa habari...


## CAG aibua malipo hewa ofisi Makamu wa Pili wa Rais

UKURASA 3



## CHADEMA yalia na mikutano vyama vya siasa, Katiba mpya

UKURASA 3


MICHEZO MORRISON: AL HILAL WATANG'OKA CAF UK.32 | KABWELA UK.7



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba

# Uamuzi mgumu kilio cha tozo

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

UAMUZI mgumu. Ndivyo inavyoweza kuelezewa baada ya serikali kusikia kilio cha Watanzania kuhusu tozo za miamala mbalimbali ya kielektroniki iliyokuwa ikilalamikiwa na kutangaza kuifuta na kupunguza kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu.

Katika marekebisho hayo, serikali imepunguza gharama ya miamala hiyo kwa asilimia 10 hadi 50, kulingana na kundi husika.

Jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali imefanya mapitio na kupunguza mzigo wa tozo kwa jamii ili kuchochea matumizi ya miamala kwa njia ya fedha tasilimu, kurahisisha utozaji na kuzuia utozaji wa tozo husika mara mbili, kwa kuwa utozaji wake kwa sasa, unahusisha pande zote mbili, yaani mtoaji na mpokeaji.

"Marekebisho yanayofanyika ni kufuta tozo ya kuhamisha fedha kutoka benki kwenda mitandao ya simu (pande zote), kufuta tozo ya kuhamisha fedha kutoka benki moja kwenda nyingine (pande zote) na kufuta tozo ya kuhamisha fedha ndani ya benki moja (pande zote).

"Wafanyabiashara hawatahusishwa kama ilivyo kwenye kanuni za sasa na kusamehe tozo ya miamala kwenye utozaji wa fedha tasilimu, kupitia wakala wa benki na ATM kwa miamala yenye thamani isiyozidi Sh. 30,000 na kupunguza gharama ya miamala, kwa asilimia 10 hadi asilimia 50 kufuatana na kundi la miamala. Ikumbukwe kuwa tozo hizo ambazo viwango vya tozo vilishushwa kwa asilimia 30 kutoka kiwango cha juu cha shilingi 10,000 hadi kiwango cha juu cha Sh. 7,000, viwango vyake vilianza kutumika Septemba 7, 2021," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Mwigulu, Rais Samia Suluhu Hassan ametaka kupunguzwa zaidi tozo na wizara ilipunguza tozo zaidi kwa kushusha tena kiwango cha juu kutoka 7,000 hadi 4,000.

Pia alisisitiza kwa kuwa ni dhahiri uamuzi huo utapunguza mapato ya serikali na ameelekeza fedha hizo zifidiwe kutokana na kubana matumizi mengineyo ndani ya serikali, ambayo hayataathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi ya mafungu husika.

Waziri alieleza maeneo yatakayotumiwa kubana matumizi hayo ni kuondoa bajeti ya chai, vitafunwa, misafara kwenye safari za ndani na nje kwa maofisa wa wizara kama Rais alivyoelekeza.

"Mheshimiwa Rais ameelekeza tupate mafunzo, semina, matamasha, warsha, makundi yanayokwenda kukagua mradi ule ule kwa nyakati tofauti au makundi yanayokwenda eneo lilelile kila mtu na gari lake (mfano, wilaya ile ile kila ofisa na gari peke yake, mkoa uleule kila kiongozi na gari peke yake," alisema.

### HAKUNA TUME

Kuhusu madai kwamba serikali iliunda tume ya watu 200, kwa ajili ya kuchambua malalamiko ya Watanzania na kutumia mabilioni ya fedha, Waziri wa Fedha, hakuna tume iliyoundwa.

"Naomba kusisitiza hapa, wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mipango, wanaohusika na masuala ya Bajeti na Sera, wamefanya mapitio haya wakiwa ofisini kama sehemu ya majukumu yao ya kila siku, tofauti na taarifa zilizozungushwa kuwa kuna tume ya watu 200 imeundwa na inatumia mabilioni ya fedha," alisema.

### CHANZO CHA TOZO

Wakati anawasilisha kauli hiyo ya serikali Bungeni, Waziri Mwigulu alisema katika mwaka wa fedha 2022/23, kulikuwa na mahitaji muhimu na ya lazima ambayo yangekosa fedha kutokana na ufinyu wa bajeti.

Aliyataja baadhi ya masuala muhimu ambayo yangeathirika kama serikali ingefuta kabisa chanzo hicho; ingeelekeza fedha za mkopo wa ECF kwenye madarasa mwaka huu (chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19), isingeweza kupeleka bilioni 954 kwenye kilimo zinazolenga kujenga miundombinu ya umwagiliaji na mbegu bora.

Alisema fedha za mkopo wa ECF kwenye ujenzi wa VETA (Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi), isingeweza kupeleka bilioni 154 kwenye mifugo, uvuvi na machinga, zinazolenga kujenga na kununua boti za uvuvi, kuchochea ukuaji wa sekta ya mifugo, kujenga miundombinu na mitaji kwa machinga.

Suala lingine kwa mujibu wa Waziri Mwigulu, wangeelekeza fedha za mkopo wa AfDB (Benki ya Maendeleo ya Afrika) kwenye ujenzi wa madarasa na VETA mwaka huu, isingeweza kupeleka Sh. bilioni 150 kwenye ruzuku ya mbolea ili kuwasaidia wakulima wazalishe chakula cha kutosha kwa ajili ya nchi yetu na kudhibiti mfumuko wa bei.

Halikadhalika, waziri huyo amefafanua kuwa, wangeamua kutotoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 kwenye mafuta kila mwezi; isingeweza kuelekeza fedha hizo kujenga madarasa yote, VETA na mengineyo.

## ...Wadau wafunguka

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa masuala ya uchumi wamepongeza uamuzi wa serikali kufuta na kupunguza tozo za miamala ya kielektroniki iliyokuwa inalalamikiwa, huku baadhi yao wakitaka hatua zaidi dhidi ya tozo za miamala ya simu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema kutokana na janga la UVIKO-19, ukuaji uchumi haujafikia kiwango kilichotarajiwa, hivyo ni wazi vipato vya wananchi vimepungua kwa wastani.

"Kufuta baadhi ya tozo na kupunguza viwango vilivyokuwa vinatozwa ni jambo zuri, linawapa wananchi ahueni na kuongeza kasi ya kutumia huduma za kibenki, alisema na kufafanua kuwa "unapokuwa na gharama kubwa, zinafanya wananchi kukwepa huduma za kibenki.

"Waziri amewaambia wataalamu wake waangalie namna ya kupunguza matumizi kwenye maeneo ambayo siyo ya lazima yanaweza kupunguzwa. Tunasubiri wataalamu hao wakokotoe tuone maeneo hayo yatakuwa na athari gani kwenye utekelezaji wa shughuli za serikali."

### PROFESA WANGWE

Prof. Samwel Wangwe, mchumi mbobevu, aliungana na Dk. Mmari kuwa tozo zilizokuwapo, zilikuwa zinaathiri uchumi jumuishi na kukatisha tamaa matumizi ya benki.

Mtaalamu huyo wa uchumi alitoa angalizo kuwa kadri nchi inavyokwenda katika uchumi wa kidigitali, hatua ambazo zinawapeleka watu huko zisitozwe kodi.

"Zikitozwa kodi zinakatisha tamaa masuala ya uchumi wa kidigitali, kuziondoa tozo hizo kunachangia kasi ya uchumi wa kidigitali.

"Wamefanya kitu kizuri lakini kabla ya uamuzi mzito wa namna hii wenye kuumiza haujafanyika, ingekuwa vizuri kuongea na wadau wakiwamo wa taasisi za kifedha, benki, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)," alisema.

Prof. Wangwe alisema kufutwa kwa tozo hizo kunaleta unafuu kwa mtu mmoja mmoja, akisisitiza kuwa jambo la msingi linalotakiwa kufanywa ni kuhakikisha watu wanawezeshwa kuzalisha na kupata faida na ndipo kodi ikatwe.

### LHRC NA WANASIASA

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema kitendo cha serikali kuchukua uamuzi huo kina maana kwamba imesikia malalamiko ya wananchi ingawa maeneo iliyopunguza tozo hizo hayalengi kuondoa kilio cha wananchi wengi.

Hata hivyo, Anna alisema mabadiliko yaliyofanyika ni ya wigo mdogo wa kodi kwa kuwa maeneo ambayo inafanyika miamala ya kifedha mara kwa mara na wananchi wengi, hayajafanyiwa marekebisho yoyote.

"Mwananchi bado anaumizwa katika maeneo ambayo kila siku anatumia, bado kuna malipo makubwa ya kodi kwenye miamala ya simu, wamebaki na ile ya mwaka jana, walitoa asilimia 30," alisema.

Naibu Msemaji sekta ya fedha wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Kombo, alisema kauli ya serikali bungeni haijamaliza kiini cha tatizo la utitiri wa tozo kwenye simu na benki.

Alisema wanachokitaka ni serikali kufuta tozo zote za kibenki ili kumpunguzia mzigo mwananchi.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma wa Chama cha Wananchi (CUF), Mohamed Ngulangwa, alisema ni vyema serikali ikaondoa tozo zote kwenye miamala hiyo na kuongeza nguvu zaidi katika ukusanyaji wa kodi halali kutoka kwa wafanyabiashara wakubwa.

Alisema huko ndiko kuna ukwepaji mkubwa wa kodi hizo pamoja na kutafuta njia za ziada za kukusanya mapato na siyo kuwatwisha mzigo wananchi.

Mkuu wa Idara ya Uenezi na Uhusiano wa Umma wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Edward Simbeye, alisema: "Serikali imesema inasamehe tozo ya miamala kwenye utoaji wa fedha tasilimu kupitia wakala wa benki na ATM kwenye miamala isiyozidi Sh. 30,000, hapa hakuna ilichopunguza, angalau ingesema kuanzia Sh. milioni moja."

**HABARI KITAIFA**

# CHADEMA yalia na mikutano vyama vya siasa, Katiba mpya

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeendelea kulia na zuio la mikutano ya vyama vya siasa na kusisitiza kuwa Katiba mpya ni muhimu ili kudumisha demokrasia na kukuza uchumi.

Chama hicho pia kimetoa sharti kwamba ili mazungumzo kati ya serikali na chama hicho yaendelee ni lazima zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa liondolewe pamoja na kutolewa kwa ratiba ya mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya na hatua zake zote kabla ya kuanza kwa Bunge la Novemba, mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Zanzibar, Salum Mwalimu, alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumzia maazimio ya Kamati Kuu ya chama hicho iliyofanyika hivi karibuni.

Alisema pamoja na mambo mengine, ilipokea na kujadili hali ya siasa ya pande zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

"Kilio hiki cha Katiba mpya angalau kuna hatua tumeshapiga, kwamba angalau wote tunazungumza haja na umuhimu wa kuwa na Katiba mpya. Sasa kama wote tunazungumza hivyo, ni lazima ipatikane sheria itakayotuongoza kufikia huo mchakato wa hiyo Katiba.

"Maana yake hiyo sheria ikishakuwapo itaelezea mchakato wote namna utakavyopatikana, kwa utaratibu gani, imehusisha kina nani, wapi, lini, na wakati gani itaanza, haya mambo hayawezi kufanywa kisiasa, ni lazima itengenezewe sheria yake," alisema Mwalimu.

**MFUKO BIMA YA AFYA**

Mwalimu alisema Kamati Kuu ya CHADEMA imeazimia kumwelekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya uchunguzi katika mfuko huo.

"Kamati Kuu imemtaka CAG kufanya ukaguzi maalumu kwenye mfuko huo na kujua mwenendo wa fedha za wanachama. Siyo kuambiwa hali mbaya pekee, bali tupewe taarifa ya sababu za kufikiwa kwa hali hiyo, kazi hii ifanywe na CAG," alisema.

Mwalimu alisema wanachama wa NHIF hawapaswi kuishia kusikia tu kwamba mfuko huo una hali mbaya kupitia vyombo vya habari, bali wanapaswa kupatiwa taarifa rasmi ambayo imedhibitishwa na CAG.



Salum Mwalimu

Kuhusu muswada wa bima ya afya kwa wote uliowasilishwa bungeni hivi karibuni, Mwalimu alisema kamati kuu imeishauri serikali kutoa muda wa kutosha kwa wananchi kutoa maoni juu ya suala hilo.

Mwalimu alisema miongoni mwa maazimo mengine yaliyofikiwa na kamati kuu ni pamoja na kuitaka serikali kupeleka Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022/23, kufuta kifungu kilichoingiza tozo kwenye miamala ya kielektroniki nchini kutokana na kuwa mzigo mkubwa kwa wananchi.

Alisema kamati kuu imetaka muswada huo wa marekebisho ya sheria, ufute kifungu cha sheria cha mwaka 2022/23 kilichoanzisha tozo mpya ya ving`amuzi ambayo bado haijaanza kutozwa ili kutoendelea kupandisha gharama za maisha kwa wananchi kupitia tozo hizo.

**BEI YA VYAKULA**

Alisema kamati iliitaka serikali kuja na mpango madhubuti wa uhakika wa upatikanaji wa chakula na kudhibiti kasi ya ukuaji wa bei za chakula nchini.

"Nadhani wote ni mashahidi, ukiangalia mahindi, maharage, mafuta mchele, vyote vimepanda, sasa haya pamoja na mambo mengine yanasababishwa na upatikanaji wa chakula na ukosefu wa njia nzuri za usimamizi wa bei za vyakula jambo ambalo linaongeza mzigo wa gharama za maisha,"alisema Mwalimu.

**MAFUTA KUPANDA BEI**

Mwalimu alisema kamati kuu imeitaka serikali kupunguza msururu wa kodi na tozo kwenye mafuta ili kuondoa ukubwa wa bei ya mafuta nchini.

**RIPOTI CAG ZANZIBAR**

Alisema chama hicho hakijaridhishwa na hatua ambazo serikali hiyo imechukua kwa waliohusika na ubadhirifu uliotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar.

"Kamati kuu inataka hatua zaidi ichukuliwe kwa wahusika na taarifa ya hatua hizo iwekwe wazi kwa umma, mambo yasizungumzwe kijumla au kireja reja, tuambiwe hao wanaosababisha ubadhirifu Zanzibar, wamechukuliwa hatua stahiki za kisheria na kinidhamu,"alisema Mwalimu.

Pia, alisema Kamati Kuu imebaini kuwapo kwa utaratibu wa kunyang`anywa kwa kandarasi za miradi mbalimbali kwa wananchi wa Zanzibar. Pia, kilitaka wabunge 19 wa viti maalum waodolewe bungeni.

"Tunataka sheria hizi ziwaondoe bungeni na wale wabunge wa viti maalum wanaoitwa wa CHADEMA kabla ya kikao cha bunge cha Novemba mwaka huu, itawaondoaje, hiyo haituhusu."

**MIKUTANO NCHI NZIMA**

Alisema kamati kuu pia iliazimia kufanyika kwa maandalizi ya mikutano ya hadhara nchi nzima kwa wakati na muda utakoelekezwa na uongozi wa chama hicho, kwa kufuata katiba, sheria na kanuni za nchi zilizopo sasa.

**Imeandaliwa na Elizaberth Zaya, Said Muhibu (SAUT), Evence Evarist (DSJ), Owen Bariki na Golden Kisapile (TUDARCo).**

# CAG abaini malipo hewa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

**Na Mary Geofrey**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, imebaini kuwapo na matumizi ya Sh. milioni 127.5 ambayo hayakuainishwa katika mpango wa ununuzi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu na Baraza la Wawakalishi.

Pia ripoti hiyo imebaini kutokuwapo kwa uwiano wa taarifa baina ya hesabu za mwisho wa mwaka na uhalisia wa matumizi ya Sh. milioni 75.

CAG Dk. Othman Abbas Ali, aliainisha ubadhirifu huo kupitia ripoti ya ukaguzi wa fedha za serikali ya Juni, 2021 katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera 2020/21 uliofanywa kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

Alisema Sh. milioni 127.5 zililipwa hati namba 13/2/2021 ya Septemba 22/2021 ambazo alilipwa Tononoka Fireworks Ltd kwa ajili ya malipo yanayohusu upigaji wa 'fash fash' kwa Januari, 2021.

"Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa matumizi hayo hayo kuainishwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka wa Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais ili kuepusha kufanyika kwa matumizi

ambayo hayaendani na makadirio halisi na kusababisha kutokupatikana kwa uthibitisho wa matumizi katika kipindi cha mwaka husika," alisema.

CAG alibainisha kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria namba 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Alishauri uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu taasisi zake ili kuhakikisha Sheria Namba 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika utayarishaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka ili kuepusha uwezekano wa kutokuingizwa kwa baadhi ya taarifa zitokanazo na ununuzi wa huduma au bidhaa.

Kuhusu kutokuwapo kwa uwiano wa hesabu, alisema Sh. 75,148,676 zinatokana na tofauti iliyobainika kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka na mlinganisho wa taarifa halisi ya matumizi ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa petroli na Dizeli na katika hesabu za mwisho wa mwaka matumizi hayo yanaonekana ni Sh. 161,148,710 lakini katika uhalisia wa taarifa kupitia katika hati za malipo ni Sh. milioni 86 na kusababisha tofauti hiyo.

Dk. Ali alisema kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha Sheria Namba 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

"Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu taasisi zake ili kuhakikisha sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu.

"Hii ni pamoja na kuongeza umakini katika utayarishaji wa taarifa za fedha ili kuepusha uwezekano wa kujitokeza kwa utofauti wa taarifa zinazowasilishwa katika mamlaka husika pamoja na taarifa zinazotumika katika taasisi," alisema.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA UTEKELEZAJI WA HUKUMU 26 LA MWAKA 2022**
**(Imetokana na shauri la Madai Namba 220/2018)**
**BENARD KAMILIUS MEMBE.............................................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **CYPRIAN MAJURA MUSIBA**
2. **THE EDITOR. TANZANIA NEWSPAPER**
3. **CZ INFORMATION AND MEDIA CONSULTANT LTD**
   **PRINTERS OF TANZANITE NEWSPAPER .....................................WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
1. CYPRIAN MAJURA MUSIBA
2. THE EDITOR, TANZANIA NEWSPAPER
3. CZ INFORMATION & MEDIA CONSULTANT LTD
   PRINTERS OF TANZANITE NEWSPAPER
   **DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu, ameleta shauri la maombi utekelezaji wa hukumu dhidi yenu; maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinazopatikana katika mahakama hii, hivyo basi, mnahitajika kuhudhuria katika mahakama hii kupitia wakili au mwakilishi wenu ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 28/9/2022 saa tatu (3:00) kamili asubuhi mbele ya **Mhe. Msajili J.D. Luambano, NAIBU MSAJILI** kujibu maombi hayo dhidi yenu kwanini utekelezaji wa hukumu usiendelee.
Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo mnatarajia kuvitumia kwa ajili ya utetezi siku hiyo.

**ANGALIA**
Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini,basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu.
Hati hii imetolewa na **AMRI** yangu na **CHAPA** ya mahakama hii leo tarehe 15 septemba 2022.

THE HIGH COURT OF TANZANIA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU – DAR ES SALAAM

117054002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA YA KESI. 166 LA MWAKA 2021**
**(Imetokana na shauri la madai Namba 220/2018)**
**BENARD KAMILIUS MEMBE.............................................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **CYPRIAN MAJURA MUSIBA**
2. **THE EDITOR. TANZANIA NEWSPAPER**
3. **CZ INFORMATION & MEDIA CONSULTANT LTD**
   **PRINTERS OF TANZANITE NEWS PAPER**
   **DAR ES SALAAM .....................................................WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
1. CYPRIAN MAJURA MUSIBA
2. THE EDITOR. TANZANIA NEWSPAPER
3. CZ INFORMATION & MEDIA CONSULTANT LTD
   PRINTERS OF TANZANITE NEWS PAPER
   **DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu, ameleta shauri la maombi ya gharama ya kesi dhidi yenu; maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinazopatikana katika mahakama hii, Hivyo basi, mnahitajika kuhudhuria katika mahakama hii kupitia wakili au mwakilishi wenu ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe **28/9/2022 saa tatu (3.00)** kamili asubuhi mbele ya **Mhe.Msajili J.D. Luambano, NAIBU MSAJILI** kujibu maombi hayo dhidi yenu.
Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvituma kwa ajili ya utetezi siku hiyo.

**ANGALIA**
Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu.
HATI hii imetolewa kwa **AMRI** yangu na **CHAPA** ya mahakama hii leo tarehe 15 septemba, 2022.

THE HIGH COURT OF TANZANIA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU – DAR ES SALAAM

117054002

# Jela miaka 10 kwa kumkata shingo mama mkubwa na kusababisha kifo

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu Daudi Juma (33) kifungo cha miaka 10 jela kwa kosa la kumuua mama mkubwa wake, Pili Jeremani kwa kumcharanga mapanga shingoni na kufariki dunia papo hapo.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, John Kahyoza, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa la kumuua mama yake mkubwa bila kukusudia.

Baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa, Jaji Kahyoza alimwambia Wakili wa Serikali Winfrida Ernest amsomee maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Ernest alidai kuwa mshtakiwa na marehemu walikuwa ndugu na mshtakiwa alikuwa akimwita mama mkubwa na Jeremani alikuwa akiishi mkoa wa Mwanza na familia yake.

Ernest alidai kuwa kulikuwa na mgogoro wa chini chini kati ya Jeremani na mshtakiwa ambao ulikuwa ukihusisha mashamba na imani ya kishirikina. Alidai kuwa Agosti, 2016 Jeremani alifika katika Kijiji cha Nyakazeze wilayani Geita kuhudhuria msiba.

Wakili huyo alidai kuwa Agosti, 2016 majira ya usiku, mshtakiwa alifika kwa kaka yake Gurilo Jeremia ambako Jeremani alikuwa amefikia akiwa na lengo la kupata suluhu juu ya tuhuma zilizokuwa zinamkabili za mgogoro wa mashamba na imani ya kishirikina.

Alidai kuwa wakati wako kwenye mazungumzo, kuliibuka ugomvi ndipo mshtakiwa akaamka kwa hasira na kuchukua panga na kuanza kumkata kata shingoni mama mkubwa wake na kufariki dunia papo hapo. Baada ya kuona mama mkubwa wake amefariki dunia, alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Kutokana na kitendo hicho, alidai kuwa taarifa ziliwafikia viongozi wa kijiji na polisi na kuanza upelelezi wa suala hilo na mwili wa marehemu ulifanyiwa uchunguzi na daktari alibaini kuwa alifariki dunia kwa kuvuja damu nyingi baada ya kuwa na jeraha kubwa alilokatwa na panga shingoni.

Alidai kuwa Oktoba, 2016 mshtakiwa alikamatwa na kufikishwa kituo cha polisi Katoro na alipohojiwa alikiri kuhusika kumuua mama mkubwa wake na upelelezi ulipokamilika, alifikishwa mahakamani ili sheria ichukuwe mkondo wake.

Baada ya Wakili wa Serikali Ernest kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali, Jaji Kahyoza alimuuliza mshtakiwa kama maelezo yote yaliyosomwa ni kweli au si kweli? Mshtakiwa alijibu ni kweli alimuua mama mkubwa kwa sababu ya ugomvi.

Jaji Kahyoza alisema: "Mshtakiwa umekiri kosa lako mwenyewe bila ya kulazimishwa, hivyo mahakama hii imekuona unayo hatia na mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa la kumuua mama yako mkubwa bila ya kukusudia. Pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili iweze kukupunguzia adhabu."

Mshtakiwa huyo akiongozwa na wakili wake, Laurent Bugoti, alidai kuwa mteja wake amekaa gerezani kwa muda wa miaka sita pia ana mke na mtoto mmoja wanamtegemea.

Pia wakili huyo alidai kwamba mteja wake ana tatizo la kuishiwa damu mara kwa mara na ni kosa lake la kwanza na kwamba amejifunza ndiyo maana amekiri kosa mwenyewe bila kulazimishwa kwa hiyo anaomba mahakama impe mteja wake adhabu nyepesi.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Ernest uliomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kikatili kama yake.

Ernest alidai kuwa silaha aliyoitumia mshtakiwa ni silaha kali pia sehemu iliyokatwa ni hatarishi na kwamba baada ya kutenda tukio hilo, alikimbia na kumuacha mama mkubwa wake akiwa amefariki dunia.

Alidai kuwa kitendo cha mshtakiwa kukatisha uhai wa mama mkubwa wake na kuacha familia yake ikihangaika, ni cha kikatili, hivyo upande wa mashtaka kuomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake.

Jaji Kahyoza alitupilia mbali utetezi huo na kusema mshtakiwa alimuua mama yake mkubwa kwa imani ya kishirikina pamoja na mgogoro wa ardhi, hivyo kosa alilolitenda ni kubwa sana kwa kutumia silaha tena kukata sehemu mbaya za shingoni.

Kutokana na hali hiyo, alisema mahakama inamhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka 10 jela na anayo haki ya kukata rufani kama hajaridhika na hukumu hiyo.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Madalali wa Madini Tanzania (CHAMMATA), Bahati Damiani, akipokea kadi ya uanachama wa chama hicho kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, wakati wa uzinduzi wa kadi za wanachama, wilayani humo, mkoani Shinyanga jana. **HABARI UK. 24.** **PICHA: SHABAN NJIA**

## Ajali yaua wawili, kujeruhi 7

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU wawili wamefariki dunia na wengine saba kujeruhiwa baada ya magari mawili aina ya Toyota Noah waliyokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso wilayani Ikungi mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stellah Mutabihirwa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Septemba 18, mwaka huu, eneo la Utaho wilayani Ikungi barabara kuu ya Dodoma - Singida.

Mutabihirwa alisema ajali hiyo ilihusisha magari aina ya Toyota Noah yenye namba za usajili T 433 AUY na T 835 CJX.

Aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Katibu wa Msikiti wa Kati wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) mjini Singida, Hamisi Dinya na mtoto mwenye umri wa miaka mitano, aliyefahamika kwa jina la Denisi Majaliwa, wote wakazi wa Singida.

Majeruhi katika ajali hiyo ambao wamelazwa katika Hospitali ya Misheni ya Puma ni Yusuph Athanas (27) ambaye ni dereva, Ramadham Sumwa (64), Mohamedi Ally (54), Mariam Mohamed (8), Lukuman Shaban (4), Hamis Kinyere (51), Diana Masalu (30) na Hussein Athumani (44) wote wakazi wa Singida.

Kamanda Mutabihirwa alisema chanzo cha ajali hiyo ni moja ya magari hayo lililokuwa likitokea Ikungi kwenda Singida mjini dereva wake kuendesha kwa mwendo mkali huku akijaribu kuyapita magari mawili kwa mpigo, hivyo kushindwa kulimudu na kusababisha ajali hiyo.

# Wagonjwa 3 kiharusi wapokewa MOI kila siku

**Na Mary Geofrey**

UGONJWA wa kiharusi umekuwa tishio na kugharimu maisha ya watu kutokana na ongezeko la watu wanaokumbwa na tatizo hilo, huku Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), ikibainisha kuwa imekuwa ikipokea wastani wa wagonjwa watatu kila siku, sawa na 1,095 kwa mwaka.

Daktari Bingwa wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu, Laurent Mchome, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kambi ya siku tatu ya matibabu ya upasuaji kuondoa vivimbe katika mishipa ya damu kwenye ubongo na matatizo ya pingili za uti wa mgongo.

Alisema kiharusi kwa kiasi kikubwa kinasababishwa na shinikizo la juu la damu na lehemu na kusababisha damu kuvilia kwenye ubongo.

Dk. Mchome alisema tatizo la kiharusi limekuwapo kwa muda mrefu na wanaendelea kutafuta teknolojia zaidi ya kuutibu ugonjwa huo.

"Ziko aina nyingi za kiharusi lakini wagonjwa wengi tunaopata MOI ni wale ambao damu imevilia kwenye ubongo. Tatizo hili ni kubwa sana. Kwenye maabara yetu tunawafanyia uchunguzi, tukiona wanahitaji upasuaji ndipo tunawafanyia," alisema Dk. Mchome.

Alisema miaka ya nyuma wagonjwa hao walikuwa wakipatiwa huduma saidizi na wakipata nafuu hupelekwa nje ya nchi kutibiwa lakini sasa wanatibiwa nchini.

"Wagonjwa wengi wenye shinikizo la juu la damu ambao hawatumii dawa kwa kufuata mpangilio maalumu walioelekezwa na wataalamu, wako kwenye hatari ya kupata ugonjwa huu. Pia wapo wanaopata lehemu kwenye damu wako kwenye hatari ya kupata vivimbe ambavyo hupasuka na mtu kupata kiharusi," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respecius Boniface, akizungumzia kambi hiyo, alisema MOI imeshirikiana na Hospitali ya Ramaiyah ya India, kufanya upasuaji huo, iliyoanza juzi na kuhitimishwa leo.

Dk. Boniface alisema tayari wagonjwa watano wameshafanyiwa upasuaji huo, unaogharimu Sh. milioni 10 kwa kila mmoja tofauti na kutibiwa nje ya nchi ungegharimu Sh. milioni 40 hadi 60.

"Tunategemea wagonjwa 12 watafanyiwa upasuaji mkubwa wa kibobezi. Kati ya hao saba watafanyiwa uchunguzi wa tiba ya mishipa ya damu kichwani bila kufungua fuvu, tayari wengine watano wameshafanyiwa jana (juzi) na wengine wawili watafanyiwa kesho (leo).

"Vilevile kipindi hiki tutawafanyia wagonjwa wengine watatu wenye vivimbe kichwani na wawili watafanyiwa upasuaji wa kutibu uvimbe kwenye uti wa mgongo kupitia tundu dogo. Upasuaji huo ni mpya na unaendelea kufanyika kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwenye hospitali yetu,"alisisitiza Dk. Boniface.

TANGAZO


Ministry of Commerce & Industry
Government of India
High Commission of India
Dar-Es-Salaam, Tanzania
सत्यमेव जयते
IBEF
INDIA BRAND EQUITY FOUNDATION
EEPCINDIA
ENGINEERING THE FUTURE
COME & VISIT
INDEE
TANZANIA
Co-located with INDUSMACH AFRICA-2022
22 - 24 September, 2022
10 AM - 6 PM
www.indee-tanzania.com
Meet over 90 Engineering companies from India
VENUE
Diamond Jubilee Expo Centre, Dar es Salaam, Tanzania
Focussed Sectors
Auto Components
Electrical Machinery & Equipment
Articles of Iron & Steel, Aluminum & Brass
Welding Equipment, Tools & Consumables
Pumps & Valves
Agricultural Machinery & Spare Parts
Food Processing Machinery
HVAC-R
Construction & Earthmoving Machinery
Industrial Boilers, Heaters & Furnaces
Building Materials
Packaging & Printing Machinery
TCCIA
indee TANZANIA 2022
PARTNERSHIP FOR GROWTH
Co-located with
22nd INDUSMACH AFRICA 2022
22 - 24 Sept, Dar es Salaam, Tanzania
EXPOGROUP
117054602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunaipongeza serikali kufuta tozo, lakini...

**HATIMAYE** serikali imefuta na kupunguza tozo za miamala mbalimbali ya kielektroniki iliyokuwa ikilalamikiwa na wananchi kuanzia Oktoba mosi mwaka huu.

Katika marekebisho hayo, serikali imepunguza gharama ya miamala kwa asilimia 10 hadi 50, kulingana na kundi la miamala.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitangaza hatua hiyo ya serikali baada ya kusema imefanya mapitio na kupunguza mzigo wa tozo kwa jamii ili kuchochea matumizi ya miamala kwa njia ya fedha tasilimu, kurahisisha utozaji na kuzuia utozaji wa tozo husika mara mbili.

Hatua hiyo ya serikali ni ya kupongeza na kuonesha ni sikivu kwa kusikia kilio cha wananchi wake.

Maoni ya wadau ni kuwa serikali inapotaka kuamua jambo kama lilivyokuwa la kuweka tozo, ni lazima ishirikishe wananchi kupata maoni kabla ya kuchukua uamuzi ili isitokee athari.

Malalamiko yaliyokuwa yakitolewa kila kukicha kutoka kwa wananchi hao kilikuwa hakina afya kwa maendeleo ya nchi.

Tozo hizo sio tu zilikuwa zikiumiza wananchi, bali hata kampuni ambazo baadhi zilidiriki kutangaza jinsi zinavyoathirika na tozo hizo na kusababisha kushindwa kujiendesha.

Wadau mbalimbali pia, walikuwa wakitoa kilio cha tozo kwa kuwa waathirika wakubwa walikuwa wananchi wa kipato cha chini ambao kwa kiasi kikubwa hutumia simu kufanya miamala ambayo ilikuwa ikiathirika kwa tozo hizo.

Akitangaza hatua hiyo ya serikali, Waziri wa Fedha alifafanua kuwa marekebisho yanayofanyika ni kufuta tozo ya kuhamisha fedha kutoka benki kwenda mitandao ya simu (pande zote), kufuta tozo ya kuhamisha fedha kutoka benki moja kwenda nyingine (pande zote) na kufuta tozo ya kuhamisha fedha ndani ya benki moja (pande zote).

Pia wafanyabiashara (merchants) hawatahusishwa kama ilivyo kwenye kanuni za sasa na kusamehe tozo ya miamala kwenye utozaji wa fedha tasilimu, kupitia wakala wa benki na ATM kwa miamala yenye thamani isiyozidi Shilingi 30,000 na kupunguza gharama ya miamala, kwa asilimia 10 hadi asilimia 50 kufuatana na kundi la miamala.

Tozo hizo viwango vilishushwa kwa asilimia 30 kutoka kiwango cha juu cha Sh. 10,000 hadi kiwango cha juu cha shilingi 7,000, viwango vyake vilianza kutumika Septemba 7, 2021.

Waziri Mwigulu ametangaza nia ya Rais Samia Suluhu Hassan kutaka kupunguzwa zaidi ya tozo na Wizara ya Fedha, ilipunguza tozo zaidi kwa kushusha tena kiwango cha juu kutoka 7,000 hadi 4,000.

Pamoja na kuwa kupunguzwa kwa tozo hizo kutapunguza mapato ya serikali, kama alivyoeleza Waziri wa Fedha, lakini kuna njia nyingi za kupata mapato badala ya kutegemea tozo pekee.

Vile vile, kuna matumizi ambayo yanaweza kupunguzwa kwa kubana matumizi ili serikali isiweze kuathiri katika utendaji wake wa majukumu ya msingi ya mafungu husika.

Waziri wa Fedha ameeleza maeneo yatakayotumiwa kubana matumizi hayo ni kuondoa bajeti ya chai, vitafunwa, misafara kwenye safari za ndani na nje kwa maofisa wa Wizara kama Rais Samia Suluhu Hassan, alivyoelekeza.

Kutokana na hatua hiyo, Waziri wa Fedha, amemwelekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali, kukaa na maofisa masuuli wote kuangalia upya mafungu ya matumizi mengineyo ili miradi ya maendeleo yote ithiathirike kwa hatua hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Jenifer Gilla

# Serikali inapoboresha mifumo uchumi bahari isisahau wavuvi

**NI** habari njema zinazowafurahisha raia wa taifa hili kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali za kutosha kuanzia wanyama na mimea ardhini hadi viumbe wa majini waishio baharini, ziwani na kwenye mito.

Lakini, mambo hayajakaa sawa kwa sababu vyote hivyo havijawa na mchango mkubwa kwa pato la taifa kwa vile huchangia asilimia 1.71 pekee ni kwa mujibu wa taarifa za mwaka 2019 zinazotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Taarifa hiyo pia ina mambo mazuri kuwa kwa mwaka 2020, sekta hiyo ilitoa ajira za moja kwa moja kwa takribani 202,053 kwa zaidi ya watu milioni 4.5 katika shughuli za uvuvi ukiwamo wavuvi, wasindikaji, wafanyabiashara wa samaki na wachuuzi wa zana za uvuvi.

Sekta hiyo pia ni chanzo cha lishe bora, ajira na kuongeza kipato, burudani, utalii na kufanikisha mikakati ya nchi ya kufikia lengo namba mbili la maendeleo endelevu kutokomeza njaa, kuwa na uhakika wa chakula, lishe bora na kukuza kilimo endelevu.

Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hiyo kwa jamii na taifa, serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kuiboresha ikiwamo kuweka mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji wa mazao bahari ili kuyaongezea thamani pamoja na kuandaa mazingira bora kwa wawekezaji.

Pamoja na juhudi zote hizo kuna kundi moja muhimu la wavuvi ambalo pamoja na juhudi kubwa linazofanya ya kuhakikisha samaki wanafika sokoni, serikali na wadau wa sekta hiyo hawajawapa kipaumbele cha kutosha.

Nasema hivi kwa sababu kwa muda mrefu wavuvi wamekuwa wakilalamikia kusahaulika na kutaja changamoto wanazokumbana nazo katika shughuli zao ikiwamo kutowapatia vifaa sahihi vya uvuvi, hali inayowasababisha kupata ajali za majini zinazowasababishia vifo na maradhi ya kudumu.

**Kwa mantiki hiyo hali ikiendelea kuwa hivyo taifa linaweza kupoteza nguvu kazi hii muhimu katika sekta ya uvuvi, hali inayoweza kudhorotesha shughuli za uvuvi nchini.**

Wavuvi hao pia wamekuwa wakisumbuliwa na ukosefu wa elimu ya uzamiaji kwenye hali inayowasababishia kupata maradhi ikiwamo kupooza na kutoka damu za puani.

Asilimia kubwa ya wavuvi hapa nchini hasa wale wanaozamia kina kirefu chini ya bahari wanafanya shughuli hiyo kwa mazaoea na kufundishwa na wazazi na walezi wao au washirika wao kwenye kazi na si kupatiwa elimu ya kitaalamu na walimu wanaofahamu fani hiyo hali inayosababisha kukosa ujuzi muhimu ikiwamo vifaa vya kuvaa na mambo ya kuzingatia wakati unazama chini na kupanda juu ya maji.

Licha ya hayo, wavuvi hao wamelalamika kuwa ikitokea wamepata madhara hakuna hospitali maalum za wakuwapa matibabu hali inayowafanya kuelekea kwa waganga wa kienyeji wakiamini kuwa huko ndiko wako salama zaidi hali inayochelewesha matibabu yao au kusababisha vifo.

Hivi karibuni mvuvi Shabani Ally wa Kigamboni, aliiambia Nipashe kuwa alipata ugonjwa wa kupooza akiwa katika shughuli zake za kuvua samaki mita 20 chini ya bahari jambo lililomfanya kupumzika kwenye shughuli hiyo kwa takribani mwaka mmoja.

Kwa mantiki hiyo hali ikiendelea kuwa hivyo taifa linaweza kupoteza nguvu kazi hii muhimu katika sekta ya uvuvi, hali inayoweza kudhorotesha shughuli za uvuvi nchini.

Hivyo basi, wakati serikali inaweka mikakati ya kuboresha mifumo katika sekta hiyo, haina budi kuliweka kundi hilo katika mikakati hiyo ili likue pamoja na kuliko kuliacha nyuma likiangamia wakati mifumo mingine inazidi kuboreshwa.

Ili kuweza kutatua changamoto hizo kwa ufasaha serikali haina budi kukaa pamoja na kundi hili na kusikiliza changamoto zao na kuzitatua kwa kushirikiana na viongozi wao na wataalamu wa wazamiaji.

## IGP Wambura aendelea kufumua uongozi polisi

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) Camilius Wambura, ameendelea kufumua uongozi wa jeshi hilo baada ya jana kufanya mabadiliko mengine kwa kuwahamisha baadhi ya makamanda wa mikoa.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Polisi, David Misime, ilibainisha kuwa IGP Wambura amewahamisha mikoa ya kazi baadhi ya makamanda wa polisi mikoa na mmoja kumhamishia Makao Makuu ya Jeshi hilo yaliyoko Dodoma.

Waliohamishwa ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Henry Mwaibambe aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Geita, akipelekwa Mkoa wa Tanga huku Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Safia Shomary, akihamishiwa Mkoa wa Geita.

Aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Temeke, Kamishna Msaidizi wa Polisi Richard Ngole amehamishiwa Makao Makuu ya Polisi Dodoma na nafasi yake imechukuliwa na Kamishna Msaidizi wa Polisi Kungu Malulu ambaye alikuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji.

Tangu aliposhika nafasi hiyo Julai 20 mwaka huu, IGP Wambura, amekuwa akifanya mabadiliko ya uongozi wa jeshi hilo.

Septemba 13, mwaka huu, IGP Wambura alifanya mabadiliko mengine madogo ya kuwahamisha baadhi ya makamanda wa polisi yakimgusa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Ulrich Matei, aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, akihamishiwa Makao Makuu ya Polisi Dodoma.

Nafasi ya Matei ilichukuliwa na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamini Kuzaga huku Kamishna Msaidizi wa Polisi George Katabazi kutoka Makao Makuu ya Upelelezi Dodoma, akiteuliwa kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, akichukua nafasi ya ACP Benjamini Kuzaga, aliyehamishiwa Mbeya.

Mabadiliko mengine aliyafanya Agosti 12, mwaka huu, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Pili Omary Mande aliyekuwa Ofisa Mnadhimu Namba Moja Mkoa wa Ruvuma, alipomteua kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi.

Kamishna Msaidizi wa Polisi Marco Chillya aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, alihamishiwa Mkoa wa Ruvuma akichukua nafasi ya Kamishna Msaidizi wa Polisi Joseph Konyo ambaye amestaafu.

Vilevile, aliyekuwa Mkuu wa Operesheni Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi Gaudianus Kamugisha aliteuliwa kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, akichukua nafasi ya Kamishna Msaidizi wa Polisi Abdallah Haji Seti aliyehamishiwa Makao Makuu ya Polisi Zanzibar.

Julai 20, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan wakati akiwaapisha wateule wake, akiwamo IGP Wambura, alimtaka (Wambura) kuwa, anachotegemea kutoka kwake ni mabadiliko ya mteule wake huyo kufanya mabadiliko makubwa ndani ya jeshi hilo ili kuwa na ufanisi katika utendaji wao.




Meneja Mwandamizi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Emmanuel Kiondo (kulia),akiendesha mijadala katika semina maalum kwa waandishi wa habari za biashara na uchumi, iliyopewa jina la "CRDB Bank Media Day", jijini Dar es Salaam jana, iliyolenga kuwajengea uwezo ili kutekeleza majukumu yao ya kuihabarisha jamii. Wengine ni (kutoka kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communication Ltd, Bakari Machumu, Mkuu wa Idara ya Huduma ya Radio TBC, Asha Mbaruku na Mhadhiri Chuo Kikuu Dar es Salaam, Dk. Darius Mukiza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yawapa mafunzo maalum waandishi habari

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeendesha semina maalum kwa waandishi wa habari za biashara na uchumi iliyofanyika katika Makao Makuu yake jijini Dar es Salaam jana ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za kuendeleza sekta ya habari nchini.

Akifungua semina hiyo, Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, alisema semina hiyo iliyopewa jina la 'CRDB Bank Media Day', imelenga kuwajengea uwezo na ujuzi waandishi wa habari ili kutekeleza majukumu yao ya kuihabarisha jamii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

"Tukiwa wadau wakubwa wa sekta ya habari, tuna jukumu la kuhakikisha waandishi wa habari wanafanya kazi yao vizuri kwa kuwaongezea maarifa yatakayowasaidia kuandaa na kuhariri habari za biashara na uchumi kwa weledi mkubwa," alisema.

Mwambapa alisema benki hiyo imeona kuna pengo linaloongezeka la ubora wa habari za biashara na fedha kwenye vyombo vya habari, msukumo uliopelekea kuandaa semina hiyo. Alisema mpango wao ni kuendelea kuandaa semina hiyo mara kwa mara ili kuinua kiwango cha taarifa za fedha.

Mkurugenzi huyo alisema mafanikio ya Benki ya CRDB yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na taarifa za vyombo vya habari kwa umma ambazo zilikuwa na matokeo chanya kwa jamii.

"Vyombo vya habari siyo tu vimesaidia kutangaza huduma na malengo ya Benki ya CRDB, bali pia utendaji wa uchumi wa taifa katika hatua mbalimbali," alisema. Mkurugenzi huyo alisema licha ya sera nzuri za uchumi za nchi, kama vyombo vya habari vikipuuzwa, malengo ya kuwawezesha watu kufahamu kinachoendelea katika mazingira yao na fursa zilizopo, hayatafikiwa.

Kutokana na umuhimu wa vyombo vya habari katika kuinua sekta mbalimbali za uchumi, mkurugenzi huyo alisema benki hiyo sasa imepania kuendelea kufadhili waandishi wa habari hususan katika utafiti unaohusu masuala ya uchumi, fedha na taarifa za biashara ili kuwafikia wananchi wengi.

Akichangia mjadala wa 'Jukumu la Vyombo la Habari katika Kukuza Uchumi', Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mwananchi Communications, Bakari Machumu, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuandaa semina hiyo kwa waandishi wa habari.

Machumu alisema waandishi wa habari wanapaswa kujenga uelewa wa kutosha wa sekta mbalimbali, jambo litakalowasaidia katika kujenga hoja katika taarifa zao.

"Kujenga uelewa juu ya sekta husika kutamwezesha mtu siyo tu kuandika taarifa bora, bali pia kujenga uwezo wa kuhoji kutakakowezesha kupata taarifa zaidi," alisema Machumu ambaye pia ni mtaalamu wa habari za biashara.

Meneja Mwandamizi wa PwC, Samwel Karoli, akiwasilisha mada kuhusu namna ya kuripoti taarifa za fedha, alisema mwandishi wa habari anapaswa kusoma kwa kuirudia mara nyingi zaidi taarifa ya fedha anayopaswa kuiandikia habari na akishindwa kuelewa, anapaswa kuwauliza wataalamu ili kuripoti taarifa kwa usahihi.

Kuhusu fursa za habari katika mitandao ya kijamii, Stephen Mokiwa, Mwanzilishi wa Teknokona, alisema vyombo vya habari vinapaswa kutengeneza bidhaa za kidijitali ili kuendana na mabadiliko ya walaji wa habari. Alipongeza baadhi ya vyombo kuanza kuchangamkia fursa hiyo.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa katika semina hiyo ikiwamo Uwasilishaji wa Habari za Taarifa za Fedha iliyowasilishwa na Meneja Mwandamizi PwC, Karoli; Fursa za Mitandao ya Kijamii katika Sekta ya Habari iliyowasilishwa na Mokiwa huku mwandishi wa habari maarufu wa mitandaoni, Millard Ayo, akichangia kupitia mtandao.

Mada nyingine zilikuwa ni Kanuni za Utangazaji katika Kuandaa Vipindi na Habari za Uchumi na Biashara iliyowasilishwa na Rolf Kibaja, Mtaalam wa Maudhui wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) na ya Maadili ya Uandishi wa Habari iliyowsilishwa na Dk. Darius Mukiza, Mhadhiri Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM).

## KABWELA



# Halmashauri sita vinara maambukizi malaria

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

HALMASHAURI sita za mikoa ya Lindi na Mtwara zimetajwa kuwa na kiwango cha juu ya maambukizi ya malaria kwa kuwa na asilimia 15 kulinganisha na wastani wa kitaifa wa asimilia 7.3 ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, alisema hayo mwishoni mwa wiki kupitia hotuba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika hafla ya kampeni ya ugawaji wa vyandarua vyenye dawa kwa wananchi wa halmashauri hizo kwa lengo la mapambano ya kujikinga na malaria.

Kanali Abbas alisema mkoa wa Mtwara maambukizi ya ugonjwa ni asilimia 15, hivyo jitihada za makusudi katika pambano dhidi ya ugonjwa wa malaria zinahitajika.

Alisema katika kukabiliana na ugonjwa huo kwa halmashauri hizo ambazo ni Masasi, Nanyumbu, Newala, Nachingwea, Ruangwa na Mtama, zitapatiwa vyandarua vyenye dawa kwa ajili ya kuwagawia wananchi wao. Kanali Abbas alisema vyandarua vyenye dawa 812,118 vinatolewa na kwamba viko tayari kwa matumizi kwa wananchi.

"Ninayo furaha kubwa kuwaarifa kuwa kampeni hii ninayozindua hapa itagawa vyandarua hivi na nina imani kubwa itasaidia jamii kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu hatari wa malaria. Sote tukahamasishe jamii juu ya matumizi sahihi ya vyandarua hivi," alisema.

Kaimu Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kutoka Wizara ya Afya, Winfrida Mwafongo, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya maambukizi ya malaria. Alisema kiwango cha maambukizi ya malaria kimepungua nchini kwa asilimia 50.

Alisema kiwango kimepungua kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017 kutokana na serikali kuweka juhudi kubwa katika mapambano dhidi ya malaria kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Naye Mratibu wa Malaria Wilaya ya Newala, Dk. Alexandar Samma, alisema wilaya hiyo miongoni mwa maeneo ambayo yamekuwa na kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria. Alisema kwa mwaka jana, asilimia 45 ya watu waliohudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya waligundulika kuwa na malaria.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali ya wilaya imeanza kutekeleza mkakati wa kupambana na malaria kwa kugawa vyandarua na kutoa elimu ya usafi wa mazingira na kununua dawa lita 461 kwa ajili ya kupulizia kwenye mazalia ya mbu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti na tuzo ya Kongamano la sita la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, baada ya wizara yake kushika nafasi ya tatu kwa upande wa kundi la wizara, jijini Dodoma juzi. **PICHA: WANMM**

## Wizara Ardhi yapewa tuzo uwezeshaji kiuchumi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imepata cheti na tuzo katika Kongamano la Sita la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushika nafasi ya tatu kwa upande wa kundi la wizara.

Tuzo hiyo ilikabidhiwa juzi wakati wa kongamano la Sita la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lililofanyika jijini hapo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alikabidhiwa tuzo hiyo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kongamano.

Akizungumza wakati wa kongamano hilo, Waziri Mkuu aliwataka wadau wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kuongeza nguvu katika kutoa huduma za uwezeshaji hasa maeneo ya pembezoni ya miji na vijijini.

Majaliwa alisema kwa kufanya hivyo, nchi itafikia malengo katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini miongoni mwa Watanzania.

Aidha, aliitaka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuongeza kasi katika kupima na kurasimisha maeneo mbalimbali nchini.

# Watumishi 1,400 wahitimu mafunzo kijeshi

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imeendelea kutekeleza mfumo wa Jeshi Usu (JU) na hadi sasa watumishi 1,407 kati ya 1,863, sawa na asilimia 75.5, wamehitimu mafunzo ya kijeshi.

Mfumo huo wa kijeshi ulizinduliwa rasmi Novemba, 2018 na aliyekuwa Makamu wa Rais ambaye kwa sasa ni Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, alisema hivi karibuni wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu shughuli zinazofanywa na mamlaka hiyo iliyoanzishwa mwaka 2016.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mfumo huo ni mwendelezo wa jitihada za kuongeza ufanisi katika ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori.

Nyanda alisema TAWA imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi na ukarabati wa barabara yenye urefu wa kilometa 431.4, kukamilika kwa ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Lake Natron na katika Pori la Akiba Maswa na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Buturi umekamilika kwa asilimia 50.

Alisema vyanzo vikuu vya mapato kwa mamlaka ni uwindaji wa kitalii na utalii wa picha na kwamba kutokana na mlipuko wa UVIKO-19, mapato kwa mwaka 2020/21 yalikuwa Sh. bilioni 25.75 sawa na asilimia 47.46 ya makadirio ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 54.25 katika mwaka husika.

"Ingawa jukumu la kukusanya mapato linatekelezwa na TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), TAWA ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 61.1 katika mwaka fedha wa 2021/22 na kwa mujibu wa mfumo wa serikali (MNRT Portal) Sh. bilioni 49.5 zilikusanywa kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato sawa na asilimia 80 ya lengo," alisema.

Nyanda alisema kwa ujumla mwenendo wa makusanyo ya mapato yatokanayo na utalii umeanza kuimarika.

Alisema katika kutekeleza mpango wa Jeshi Usu, mamlaka ilikamilisha ujenzi wa nyumba 14 za watumishi, kambi 21 za askari, maghala 16 ya silaha, ofisi sita na hosteli moja.

Aidha, Nyanda alisema mamlaka imefanikisha ununuzi wa vitendea kazi ikiwamo magari 115, mahema 1,579, boti 10, mtambo mmoja wa kuchimba visima, gari la kubeba mizigo moja na greda moja.

Katika fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, maarufu fedha za UVIKO-19, alisema TAWA iliidhinishiwa Sh. bilioni 12.9 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ununuzi wa mitambo, magari na vifaa vingine vya utalii na doria.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali ambapo ujenzi wa barabara kilomita 336.2 kati ya kilometa 463.5 sawa na asilimia 72.5 umekamilika katika mapori ya Akiba Wami Mbiki, Kijereshi, Mkungunero, Lukwika Lumesule, Liparamba, Igombe na Rungwa.

Pia alisema ujenzi wa malango makubwa mawili kati ya manne katika Mapori ya Mkungunero na Swagaswaga umekamilika na malango mawili katika Mapori ya Wamimbiki na Kijereshi yapo katika hatua za umaliziaji.

Kadhalika, alisema magari matatu kati ya sita yaliyopangwa kununuliwa yalishapokelewa na magari matatu yaliyosalia yanatarajiwa kupokelewa mwezi huu wa Septemba 2022 kutoka Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA).

Alisema kupitia fedha hizo, mamlaka pia imenunua mtambo wa kulima barabara (greda) na gari la kuchimba visima ambalo litatumika kuchimba visima katika maeneo ya hifadhi na maeneo ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi.

Nyanda pia alisema mamlaka imenunua boti nne kwa ajili ya shughuli za utalii na doria, boti maalum kwa ajili ya shughuli za doria maeneo yenye ardhi chepechepe na boti moja ya kisasa yenye uwezo wa kubeba watu 60 kwa ajili ya shughuli za utalii kwenye eneo la kihistoria la Magofu ya Kilwa.

Alisema ili kuimarisha utendaji wa Mamlaka, jumla ya miongozo 15 ya kimkakati ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya mamlaka kwa ufanisi iliandaliwa na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Alisema miongozo hiyo inalenga kuimarisha utendaji kazi katika maeneo ya rasilimali watu, usimamizi wa fedha, matumizi ya silaha, masuala ya TEHAMA na intelijensia, ugawaji wa vitalu, na ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori ikiwa ni pamoja na miongozo ya utekelezaji wa mfumo wa Kijeshi kwa Jeshi la Uhifadhi (JU).

## TAPO yataka serikali kuongeza ulinzi watoto

**Na Elizabeth Zaya**

UMOJA wa Wanawake Unaotetea Wanawake na Wasichana (TAPO), umeiomba serikali kuweka mazingira mazuri ya kuwalinda watoto kupata mimba za utotoni.

Mmoja wa washirika wa TAPO, Janeth John, alisema bado hakuna mazingira mazuri ya kuwalinda watoto kupata ujauzito licha ya serikali kuwarudisha shuleni baada ya kujifungua.

"Pamoja na serikali kuwaruhusu watoto wanaopata mimba kurudi shuleni baada ya kujifungua, lakini bado hakujawekwa mazingira mazuri namna ya kuzuia vyanzo vinavyochangia wao kupata mimba hizo, bado kuna jambo halijakamilika," alisema Janeth. Alisema, miongoni mwa mambo ambayo serikali inapaswa kuyafanya ili kuwalinda watoto wasipate mimba ni pamoja na kufanyia marekebisho vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

"Tumewaruhusu watoto kurudi shuleni wanaopata ujauzito huku tukiwa hatujapitisha sheria inayowalinda kupata ujauzito huo. Ikumbukwe kuwa mwarobaini wa suala hili ni kurekebisha sheria ya ndoa. Na hii ndio itawapa ulinzi kamili warudi shuleni na itasaidia kuwalinda wasipate mimba wakiwa bado na umri mdogo,"alisema Janeth.

"Itawapa nafasi ya kujua kuwa elimu ni haki yao na wataipata kwa sababu watakuwa na ulinzi mzuri kupitia hiyo sheria kama itafanyiwa marekebisho."

Alisema, mwaka 2016 mahakama iliamuru sheria hiyo kufanyiwa marekebisho baada ya Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi kushinda kesi na kwamba tangu amri hiyo itolewe hakuna mabadiliko yaliyofanyika mpaka sasa.

"Ombi kubwa ni kwa serikali, iharakishe mabadiliko ya sheria hiyo kwa sababu sio tu waliochini ya umri wa miaka 18 ni watoto na hawana uwezo wa kufanya maamuzi sahihi juu ya kuoa au kuolewa bali ndoa za utotoni zinawanyima haki ya kupata elimu na uhuru wa mawazo," alisema Janeth.

"Kwa hiyo, kama ambavyo serikali imeona umuhimu wa kuwaruhusu wasichana kurudi shuleni baada ya kujifungua, basi bunge letu nalo lione jambo hili kwa jicho la kulinda utu na haki za wasichana. Mabadiliko ya sheria hii ya ndoa yatawalinda wasichana wengi dhidi ya changamoto nyingi."

# Mufti akerwa wastaafu kuwavuruga waumini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHEKHE Mkuu wa Tanzania, Mufti Dk. Abubakar Zubeir Ally, amesema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya watu waliostaafu au kuondolewa kazini kwenda misikitini na kuwavuruga Waislamu.

Alisema hayo jana wakati akiongoza mamia ya Waislamu mkoani Singida katika hafla ya kuzindua Mfuko wa Maendeleo wa Mufti (MDF).

"Kumezuka tabia kwa watu waliostaafu au kuondolewa kazini kwenda misikitini huku wakizungumza Kiingereza na kuwavuruga waislamu, jambo hili sio zuri na halikubariki, " alisema.

Mufti Zubeir aliwataka Waislam nchini kujenga tabia ya kujitolea na kutoa kwa kile walichonacho kwa ajili ya kuendeleza dini ya kiislam.

Alisema Mtume Muhammad (SAW) alipokuwa akiutangaza uislam na kuukumbatia kila aliyekuwa nacho alitoa hali kadhalika na waliokwenda hija walifanya hivyo mpaka uislam ukafika ulipofikia.

"Watu walitoa mali zao mbalimbali kwa ajili ya kuipigania dini ya kiislam hivyo na sisi tusiwe nyuma kufanya hivyo," alisema.

Mufti alisema jambo hilo la kuchangia mfuko huo si la ujanjaujanja bali lina mpango kamili hivyo watumie fursa hiyo kwa ajili ya kutoa kwa maendeleo ya waislam na thawabu zao watazikuta mbele ya Mwenyezi Mungu.

Zubeir aliwahimiza Waislam kufanya hivyo kwa kuwa Mungu ataona, Waislam wataona na Mtume Mohamad (SAW) ataona na akaeleza kuwa Waislam hawatakiwi kuwa na tabia ya kuombaomba.

"Waislam wa Tanzania ni matajiri ambao kila mmoja hashindwi kutoa Sh.10,000 kwa mwezi kama alivyojitolea mwanamke Hadija anayesimuliwa katika kitabu kitakatifu cha Quran," alisema.

Alisema Waislam waondoe dhana ya kuwa michango inayotolewa haiendi kufanya maendeleo badala yake wawe na imani akitolea mfano baadhi ya wenzao ambao hakuwataja kuwa wamekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kutokuwa na mtazamo huo.

"Wenzetu wakizungumza jambo wanakusanya pesa na wakiamua linakuwa, mimi nina ushahidi ipo siku nitawaambia lakini sisi tukizungumza jambo na Imam msikitini, baadhi ya viongozi kwenye kata, wilaya na mkoa wanalipinga," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mulagiri, alisema serikali imekuwa ikiamini kwa sehemu kubwa sana kuwa amani na utulivu uliopo hapa nchini ni kwa sababu ya kazi kubwa inayofanywa na viongozi wa dini kwa kuliombea taifa na maadili ya kidini ambayo yanajenga amani na upendo.

Muragiri alitumia nafasi hiyo kuwashukuru viongozi wa dini kwa kushirikiana na serikali katika kuhamasisha waumini wao kwenye zoezi la kitaifa la Sensa ya Watu na Makazi ambalo lilipata mafanikio makubwa.

Alimpongeza Mufti Zubeir kwa kuwa na maono ya kuanzisha MDF. Mfuko ambao ni mkombozi mkubwa kwa serikali kwa kuwa utatatua changamoto mbalimbali za wananchi.

Katika uzinduzi wa mfuko huo viongozi mbalimbali wa dini ya kiislam, serikali, wafanyabiashara, watumishi wa umma, watu binafsi, wananchi na wanasiasa walijitokeza kuchangia mfuko huo miongoni mwao akiwa Salha Amir mkazi wa Iramba ambaye ameitoa hospitali yake yenye vyumba 25 na ardhi yenye ekari 12.5 vyote vikiwa na thamani ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya mradi wa mfuko wa maendeleo wa Mufti.

Miongoni mwa waliochangia mfuko huo ni pamoja na Mwenyekiti wa BAKWATA Mkoa wa Singida, Jumanne Nkii, ambaye naye alitoa nyumba ya vyumba saba na eneo la ardhi na Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, ambaye ametoa ahadi ya Sh. milioni 10.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel (wa nne kushoto), akipokea baadhi ya vifaa vya kuhudumia watoto njiti vyenye thamani ya Sh. milioni 110 vilivyokabidhiwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (wa nne kulia), kwa ajili ya wilaya mbili za Handeni na Kilindi, mkoani Tanga mwishoni mwa wiki, ili kuendeleza juhudi za kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati nchini. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yawafunda wajasiriamali alama ubora

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI 5,446 wakiwamo wanawake katika wilaya tano za mkoa wa Mwanza, wamepatiwa elimu kuhusu viwango na taratibu za kufuata ili kupata alama ya ubora kwa biashara zao.

Elimu hiyo kwa umma ilitolewa na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuanzia Septemba 5 hadi 19, mwaka huu, katika wilaya za Sengerema, Kwimba, Misungwi, Ilemela na Magu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Mwanza wakati akitoa majumuisho ya mafunzo hayo, Meneja Uhusiano na Masoko wa TBS, Gladness Kaseka, alisema kwa kipindi hicho walitoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya shirika na masuala mbalimbali ya udhibiti ubora.

"Kupitia elimu hii tumewafikia watu 5,446 na tuliwafuata kule wanakofanyia shughuli zao ikiwamo kwenye masoko, minada, magulio na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu wengi," alisema.

Kaseka alisema walitoa elimu hiyo kwa wajasiriamali wengi wakiwamo wanawake 96 wa mkoa huo.

"Wajasiriamali tumewafundisha taratibu za kufuata ili kupata leseni ya kutumia alama ya ubora na jinsi inavyoweza kuwasaidia kupata masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema Kaseka.

Kwa upande wa wananchi, Kaseka alisema pamoja na mambo mengine waliwafundisha umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa na TBS, umuhimu wa kuangalia tarehe ya mwisho wa matumizi kwa bidhaa wanazotaka kuzinunua na jinsi ya kuwasiliana na TBS wanapokuwa na maoni au kukutana na changamoto zozote.

Kaseka alisema wananchi waliopata elimu hiyo waliahidi kuhakikisha wanakuwa mabalozi kwa kuhamasisha jamii kutumia bidhaa zilizothibitishwa ubora na shirika hilo pamoja na kuwa makini kuangalia muda wa mwisho wa matumizi wa bidhaa wanazotaka kuzinunua.

Aidha, alisema kupitia elimu hiyo walitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa TBS wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake wa matumizi au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko.

Wananchi waliopatiwa elimu hiyo, walipongeza hatua hiyo ya TBS, wakisema itakuwa mwarobaini wa changamoto wanazokuwa wakikutana nazo.

Mmoja wa wajasiriamali waliopatiwa elimu hiyo, Abdul Shaibu, alipongeza TBS kwa kuelimishwa taratibu za kufuata ili kuthibitisha ubora bidhaa wanazozalisha.

Alisema wanapopeleka bidhaa zao sokoni kama bidhaa hazijathibitishwa na TBS wanakabiliwa na changamoto ya kupata masoko, hivyo elimu waliyoipata imewafungulia milango ya kuanza mchakato wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

"Kwa sasa wananchi wengi wana elimu ya viwango, tukiwa sokoni tunaulizwa kama bidhaa zetu zina TBS (alama ya ubora) sasa tunaanza safari ya kutafuata alama ya ubora," alisema.

# Tathmini kufanywa kuhusu uhimilivu mifuko ya jamii

SERIKALI inatarajia kufanya tathmini ya uhimilivu wa mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na ule wa sekta binafsi (NSSF), katika mwaka wa fedha 2022/23.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Ulyankulu (CCM), Rehema Migila.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kwa sasa kuna mfumuko wa bei vitu vimepanda na wastaafu wanapata pensheni ndogo sana na kutokana na hilo, serikali haioni kama kuna sababu au umuhimu wa kuongeza pensheni kwa wazee wastaafu ambayo haikui.

Pia mbunge huyo alitaka serikali kuwapatia warithi wa mstaafu asilimia 67 ya michango yao pindi wanapofariki dunia.

Alisema kwa mujibu wa sheria iliyoitishwa hivi karibuni, mstaafu atalipwa asilimia 33 katika mafao yake kama pensheni yake ya mkupuo.

"Kama atalipwa asilimia 33 ina maana kwenye asilimia 100 inabaki asilimia 67 kwa ajili ya pensheni limbikizi. Sasa kwa nini hawa wastaafu wanapofariki dunia, asilimia 67 wasilipwe wategemezi wake pindi tunajua kabisa huyu mtumishi kipindi chote amechangia kwa asilimia 100?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Ndalichako alisema tathmini hiyo itaangalia uhimilivu na uendelevu wa mifuko ili kuona kama itaongeza pensheni kwa wastaafu kulingana na uwezo.

Pia alisema malipo ya mafao yanazingatia kanuni na mtumishi anapostaafu analipwa mafao ya mkupuo na mengine kuzingatia umri wa kuishi.

"Anapofariki dunia hajalishi alishavuka wastani wa umri wa kuishi, lakini analipwa miaka mitatu, kiasi cha asilimia 67 kinawekwa kama makisio lakini mstaafu analipwa kulingana na umri wake wa kuishi. Kwa hiyo kwa sasa tunalipa miaka mitatu baada ya kufariki dunia hatuangalii kama alikuwa amevuka umri wa wastani wa kuishi," alisema.

Awali, waziri huyo alisema mifuko ya hifadhi ya jamii hutoa mafao kwa wanachama kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii Sura namba 135 kama ilivyorejewa kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Namba Sita ya mwaka 2019. Kutokana na sheria hiyo, alisema fao la warithi ni moja ya mafao yanayotolewa pindi mwanachama anapofariki dunia.

"Kwa upande wa mfuko wa PSSSF, kupitia Kifungu cha 39(1) cha Sheria ya Mfuko mstaafu anapofariki dunia, mfuko hulipa mafao ya mkupuo ambayo ni jumla ya pensheni ya miezi 36 (sawa na miaka 3) kwa wategemezi. Kwa upande wa NSSF, kwa mujibu wa Kifungu cha 37 (1) (2) (3) cha Sheria ya Mfuko, mstaafu anapofariki dunia mfuko hulipa mafao ya mkupuo sawa na pensheni ya miezi 24 kwa wategemezi," alisema.

Alisema ulipaji wa mafao huzingatia Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018 na marekebisho yake ya mwaka 2019 na Kanuni za Mafao za mwaka 2018 kama zilivyorejewa mwaka 2022.

"Mafao yanayolipwa hayazingatii asimilia ya michango isipokuwa wastaafu na wategemezi hulipwa mafao kulingana na kanuni zinazoongoza ulipaji wa mafao ya pensheni,"alisema.



Mbunge wa Viti Maalumu, Ester Bulaya, akichangia hoja kwenye kikao cha sita cha mkutano wa nane wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Lindi yaingizwa mpango wa kupendezesha miji

BUNGE limeelezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi iko katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Mpango wa Kupendezesha Miji (TACTIC) unaohusisha halmashauri 15 ambao unatarajiwa kuanza Januari, mwakani.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lindi Mjini (CCM), Hamida Abdallah.

Abdallah katika swali lake, alihoji lini serikali itatoa fedha kutekeleza mradi wa ujenzi wa Soko Kuu na stendi ya mabasi Lindi Mjini.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 imejumuisha mradi wa soko kuu na stendi kwenye mpango wa TACTIC unaojumuisha halmashauri 45.

Akiongezea majibu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza utekelezaji wa miradi ya TACTIC uanze mara moja.

"Awamu ya kwanza miji 12 tayari mkataba ulitiwa saini Juni, mwaka huu, usanifu ulishakamilika, kazi ya kupata makandarasi itatangazwa muda wowote kuanzia sasa," alisema.

Aliwatoa hofu wabunge kuwa utekelezaji wa miradi kwenye halmashauri hizo 45 utafanyika kwa kuwa serikali ilishasaini mkataba na Benki ya Dunia.




Habari zote: Augusta Njoji
DODOMA

# Mbunge ahoji chanzo manjano kwa vichanga

WIZARA ya Afya, imetakiwa kufanya utafiti kujua chanzo cha watoto wachanga kupata manjano baada ya kuzaliwa na mama kuishiwa nguvu.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, alibainisha hayo jana alipokuwa akiuliza swali kwa wizara hiyo bungeni.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel, alisema utafiti mbalimbali umefanyika kitaifa na kimataifa kujua chanzo cha watoto wachanga kugeuka wanjano baada ya kuzaliwa.

Pia alisema utafiti huo umeonyesha kuwa hali ya umanjano ikitokea ndani ya saa 24 baada ya kuzaliwa inaonyesha tatizo la kiafya na linahitaji kutambua sababu na kutoa tiba stahiki.

"Tatizo hili likitokea baada ya saa 24, mara nyingi linatokana na sababu za kawaida za mwili wa mtoto kupunguza chembechembe nyekundu nyingi alizokuwa nazo tumboni kwa mama, hata hivyo hili pia uchunguzi wa kina ni muhimu ili kujihakikishia," alisema.

Alisema suala la utafiti ni muhimu na endelevu katika tiba.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati, alitaka mkakati wa serikali wa kusaidia kutoa dawa bure kwa watoto wanaozaliwa na selimundu.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alikiri kuwapo na tatizo hilo nchini na kwamba serikali imechukua suala hilo na sasa dawa hizo zimeunganishwa kwenye kifurushi cha dawa zinazonunuliwa na Bohari ya Dawa (MSD) na kuweka utaratibu maalum.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani wameweka utaratibu maalum unaoshughulikia watoto wenye shida hiyo.

Katika swali lingine la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zuena Bushiri, alihoji ni maeneo gani yaliyofanyiwa utafiti na kuonesha tatizo la selimundu lipo maeneo gani nchini.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema kati ya watoto 20 wanaozaliwa mmoja hukutwa na tatizo hilo.



## HABARI ARUSHA

## Wajasiriamali watakiwa kujiunga kupata bima ya afya

**Na Allan Isack,**
MANYARA

WAJASIRIAMALI na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali za viwandani, wametakiwa kujiunga katika vikundi ambavyo vitawawezesha kupatiwa bima ya afya kwa gharama nafuu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mkoa wa Manyara, Joyce Sumbwe, wakati akizungumza wajasiriamali na wamiliki wa viwanda mkoani humo.

Meneja wa mfuko huo, alisema endapo makundi hayo mawili watajiunga kwenye vikundi hivyo watakuwa na uhakika wa kupata matibabu watakapokuwa na ugonjwa wa aina yoyote.

"Nawasihi mkajiunge kwenye vikundi ambavyo vitawapa fursa ya kupatiwa bima kwa gharama nafuu kwa kuwa hakuna mtu anayefamu siku ya kuumwa, hivyo ukiwa na uhakika wa kupata matibabu ni jambo muhimu sana kwa afya ya binadamu,"alisema.

Kadhalika alisema bima hiyo itawasaidia wajasiriamali hao na wazalishaji wa bidhaa kwenye viwanda kwa kuwa afya ni mtaji muhimu katika biashara na shughuli yoyote.

Wakizungumza kwa niaba ya wajasiriamali mkoni humo, walioshiriki katika hafla hiyo, Alfredina Joseph na Spensoda Emanuel, walisema watajiunga katika vikundi ili watape urahisi wa kupatiwa bima ya gharama nafuu.

**Meneja wa mfuko huo, alisema endapo makundi hayo mawili watajiunga kwenye vikundi hivyo watakuwa na uhakika wa kupata matibabu watakapokuwa na ugonjwa wa aina yoyote.**

# Watendaji mahakama wanolewa usalama waandishi wa habari

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WATENDAJI wa mahakama nchini, wakiwamo majaji, wasajili wa mahakama, mahakimu pamoja na wadau wa sheria, wamekutana jijini Arusha kwa ajili ya mafunzo maalumu ya uhuru wa kujieleza na usalama wa waandishi wa habari wakati wakitekeleza majukumu yao.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, David Ngunyale, alisema uhuru wa kutoa habari unakwenda sambamba na utawala wa sheria.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kwamba Jaji Ngunyale alimwakilisha Mkuu wa Chuo cha Mahakama Lushoto.

Kwa mujibu wa Jaji Ngunyale ni vigumu kwa maofisa wa mahakama kuelewa umuhimu wa kujieleza na kuhusiana na utoaji wa habari, kwa kuzingatia haki na utawala wa sheria.

Alisema baada ya kumalizika kwa mafunzo hayo, anaamini kwamba maofisa wa mahakama watashirikiana kikamilifu na vyombo vya habari katika kutoa taarifa.

Aidha, alisema sasa hivi wananchi wanapata haki ya kupata taarifa za kesi zao zilizoko katika hatua mbalimbali kwa njia ya mtandao na wanaweza hata kutumia simu zao za kiganjani.

Rais wa Mahakama ya Afrika na Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), Jaji Iman Aboud, alisema uhuru wa vyombo vya habari na usalama kwa waandishi ni muhimu kwa kuwa kada ya uandishi wa habari inamchango mkubwa kwa jamii yeyote ambayo inaheshimu misingi na utawala wa sheria, demokrasia na haki za binadamu.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa kuwa majaji watafundishwa kuhusu kesi zinazohusu habari jinsi gani wanaweza kuzishughulikia kwa kuzingatia sheria za nchi na za kimataifa,"alisema.

Kuhusu mahakama hiyo, Jaji Iman, alisema uamuzi wa mashauri mbalimbali yakiwamo yanayohusu vyombo vya habari, wanasiasa, biashara na mengine yatazingatiwa na kufanyiwa kazi.

"Tumetoa uamuzi mbalimbali katika mashauri yanayohusu vyombo vya habari ikiwamo kesi mbili kutoka nchini Bukina Faso tumetolea uamuzi na kesi moja kutoka nchini Rwanda,"alisema.

Vilevile alisema uhuru wa vyombo vya habari katika kupata taarifa na kutoa taarifa kwa kuzingatia utawala wa sheria unatakiwa kuzingatiwa na kupewa kipaumbele kwa kuwa wakati mwingine vinatoa taarifa ambazo hazina uhalisia zinaweza kuleta machafuko na uvunjifu wa amani.

Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EACJ), Jaji Nestor Kayobera, alisema mafunzo hayo yatakuwa na tija katika sekta ya mahakama kwa kuwa yatajenga mahusiano kati ya mahakama na waandishi wa habari kupata habari na usalama wakati wa kutekeleza kazi zao.

Jaji Kayobera, alisema licha ya kesi hiyo, pia kuna kesi mbili zilizofunguliwa katika mahakama hiyo, moja ilifunguliwa na chombo cha habari dhidi ya uamuzi uliyotolewa na Waziri wa Habari wa wakati huo, pamoja na kesi nyingine iliyofunguliwa na chama mseto.

"Mahakama ilipitia mashauri haya kwa pamoja na kubaini kuwa yamekiuka sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutoa uamuzi,"alisema.

Kwa mujibu wa Jaji Kayobera, alisema Mahakama ya EACJ, inatoa uhuru wa wananchi kutoka nchi wanachama kufungua kesi zao, katika mahakama hiyo, bila kutoa taarifa kwenye mahakama za nchi zao, na zikipokelewa zinasajiliwa bila gharama yoyote.

"Katika mahakama za kikanda, Mahakama ya Afrika Mashariki, inaongoza kwa kusikiliza mashauri mengi kwa kuwa kesi 170 zilizofunguliwa katika mahakama hiyo, ziko katika hatua mbalimbali huku kesi 630 zimeshatolewa uamuzi kwa kipindi cha miaka 20," alisema.

Mwakilishi wa UNESCO, Mehdi Benchelah, alisema matatizo wanayokutana nayo waandishi wa habari yako katika maeneo mbalimbali, moja ya njia ya kukabiliana na matatizo hayo ni kuwapatia mafunzo watendaji wa mahakama wa ndani ya nchi na za kikanda ili kutambua umuhimu wa kusimamia uhuru wa habari na usalama wa waandishi wa habari.



Baadhi ya wafanyabiashara wakishiriki semina maalumu ya kuwajengea uelewa wa mabadiliko ya sheria mbalimbali za kodi, iliyoendeshwa na Ofisa Msimamizi wa Kodi na Elimu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Odupoi Papa (hayupo pichani), mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MARY MOSHA**

# Mangariba wafichua mbinu mpya ukeketaji

**Na Allan Isack,** HANANG'

MANGARIBA wa jamii ya Wabarbaig wilayani Hanang' mkoani Manyara, wamefichua mbinu mpya inayotumiwa na wenzao kuwakeketa watoto wa kike wa jamii hiyo wakiwa wachanga pindi wanapozaliwa.

Awali watoto wa kike wa jamii hiyo walikuwa wakikeketwa wakiwa wasichana, lakini baada ya mapambano makali ya serikali na wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, mangariba katika eneo hilo wamebadilisha mbinu na kuanza kukeketa watoto wanapozaliwa.

Ngariba mstaafu, Hawa Njolo aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye kikao kazi cha kutokomeza ukeketaji kilichoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alisema awali watoto wakike walikuwa wakikeketwa wakiwa wasichana, lakini kwa sasa wahusika wamebadilisha mbinu ya kufanya vitendo hivyo na kuwakeketa pindi wanapozaliwa.

"Mbinu hii imekuwa ikitumika kwa siri sana hivyo tunaiomba kwa kushirikiana na jamii kuongeza kasi ya kudhibiti na kutokomeza vitendo hivi vya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo kwa kuwa vina madhara makubwa kiafya na kisaikolojia,"alisema.

Alisema baada ya serikali na wadau kupiga marufuku nyembe za mangariba walibadili mbinu na kuja na njia ya kuwakeketa watoto wakizaliwa au wakiwa wachanga.

Ofisa Programu ya Sayansi Jamii kutoka UNESCO Tanzania, Uyanjo Ntandu, alisema wananchi na serikali wapaswa kuwa na mpango mkakati na kuweka juhudi za pamoja za kutokomeza ukatili huo kwa jamii.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Wilaya ya Hanang', Elionora Bernad, aliwataka wananchi wa eneo hilo kuendelea kufichua vitendo hivyo ili hatua kali za kisheria zichukuliwe kadhalika na kutokomeza ukeketaji.





## Wataka sheria itakayowabana watoto kutoa huduma wazee

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BAADHI ya wazee katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjro, wamesema umefika muda mwafaka kwa serikali kutunga sheria ya kuwabana watoto kuwasaidia na kuwatunza wazazi kama ilivyokuwa sheria ya wazazi

kuwahudumia watoto kwa kuwapa mahitaji ya msingi.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wazee katika eneo hilo, akiwamo Husen Said (75), mkazi wa Pasua, alisema kwa sasa watoto hawapendi kuwahudumia wazazi wao, hali inayosababisha kuteseka japokuwa waliwekeza nguvu nyingi kuwalea na kuwasomesha watoto.

"Umefika wakati kwa serikali kutunga sheria kwa watoto kuwahudumia wazazi na endapo itabainika wameshindwa kufanya hivyo hatua za kisheria zichukuliwe.

"Unakuta mzee ana watoto watano, hana hata sehemu ya kulala, mgonjwa wa maradhi ya uzeeni na unakuta watoto wanarushiana mpira mtu wa kutoa huduma hivyo wanamuacha mzee anateseka, tunatambua Bunge limeanza tunaomba wakaliangalie hili,"alisema Saidi.

John Nnko (67), mkazi wa Mawenzi, alisema wazee wengi hasa wa vijijini wanaishi kwa mateso huku mwengine wakikosa chakula na kusaidiwa na majira.

"Wenye kasumba ya kusahau nyumbani ni baadhi ya watoto wa kiume ingawa hata wa wa kike wako baadhi yao, zamani vijana walikuwa na hofu ya Mungu, hivyo walikuwa wakiamini kuacha kumtunza mzazi ni kumkosea Mwenyezi Mungu, lakini kwa sasa hawakumbuki hilo, tunaomba serikali itunge sheria ya kuwabana hawa watoto,"alisema.

Elizabeth Simon, mkazi wa Njoro kwa Dobi, alisema wako baadhi ya wazee kwenye kambi za wazee mjini Moshi, wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ya kutokutazamwa na ndugu, jamaa na marafiki.

"Licha ya kuwapo kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii kuna haja ya serikali kupitia Bunge kuangalia namna ya kuweka sheria kuhakikishwa kila mzee anatunzwa na wana jamii wanaomzunguka, wakiwamo watoto na ndugu

kabla ya kufikishwa mikononi mwa serikali, kwa kuwa itasaidia kupata huduma muhimu za kijamii,"alisema Saumu Idd (60), mkazi wa Pasua.

Mjumbe wa Baraza la Huru la Ushauri la Wazee la Taifa na Mwenyekiti wa Mkoa huo, Eliamini Mkongo, alisema matatizo yanayolikabili kundi hilo yanafanana nchi nzima.

Alisema kutelekezwa kwa wazee hospitalini, kukosekana kwa chakula hasa maeneo ya vijijini ni jambo la kawaida kwa sasa na endapo kutakuwapo kwa sheria itasaidia kupungua kwa matukio hayo.

# Ataka kujiua kisa manyanyaso, kipigo kutoka kwa mumewe

**Na Mary Mosha,** SIHA

MKAZI wa Kijiji cha Orkolili, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, Elizaberth Thomas (42), amenusurika kifo baada ya kunywa sumu ya panya ili aachane na mume wake, (Israeli Daudi), ambaye anadai alikuwa akimpiga mara kwa mara.

Akizungumza na Nipashe jana Mjomba wa Elizabeth, Antony Mwega, alisema jaribio la kutaka kujiua lilitokea Septemba 16 mwaka huu, Elizabeth alikimbizwa Zahanati ya Ngaritati kwa ajili ya kupatiwa matibabu na kuokoa uhai wake.

Alisema: "Sisi kama familia mara nyingi, tumekuwa tukisuluhisha ugomvi wa manyanyaso na ukatili dhidi ya ndugu yetu, kutoka kwa mume wake, hali iliyosababisha kupata majeraha mbalimbali mwilini mwake, hasa maeneo ya mgongoni japokuwa sehemu nyingine zimeanza kupona ikiwamo kwenye kidole aliposhonwa. Aliongeza: "Siku ya tukio alimpigia simu mdogo wake wa kiume, baada ya kunywa sumu hiyo, akidai kwamba ameamua kunywa sumu ili afe kuliko aendelee kuishi na mume wake anayemnyanyasa na kumpiga kila siku."

Nipashe lilifika katika zahanati hiyo na kuzungumza na Elizabeth ambaye alisema kilichomsababisha kunywa simu ni manyanyaso ya ukatili anayofanyiwa na mume wake pamoja na ugumu wa maisha.

"Nimekaa kwenye ndoa miaka 21, nimevumilia mengi, sitaki kutoa siri ya ndani, lakini kwa sasa ilipofikia ni bora nife tu, mwaka 2017 alinikata na panga mkono na kushonwa nilivumilia.

"Pia akanikata kichwani nikaenda nyumbani akaonywa na aliahidi kutokurudia tena kwa kuwa mara nyingi anapofanya matukio haya, anasingizia kwa sababu ana kunywa pombe".

Vilevile alisema Septemba 12, mwaka huu, alikwenda sokoni kwa ajili ya kujitafutia riziki ya familia na aliporejea nyumbani majira ya jioni alipigwa.

"Nimekaa siku tano ndani tangu nipigwe nikiwa na maumivu makali, nikimweleza anazidi kunipiga, ameshinda hata kunipeleka hospitali, ninamajeraha kila sehemu ya mwili wangu, hivyo nimechoka bora nife ili abaki na maisha yake mazuri, lakini siku akija kwa Mungu tutafanya patano,"alisema.

Diwani wa Kata ya Orikolili, Jonathan Nasari, bado hajapata undani wa tukio hilo na kueleza kuwa endapo atapata atatoa taarifa.

Mganga Mkuu wa Hospitali Wilaya ya Siha, Peter Mahuu, alisema hana taarifa ya jambo hilo na aliahidi kufuatilia na kulitolea ufafanuzi.

"Sina taarifa kuhusu tukio hilo niko kwenye kikao huku halmashauri, lakini nikitoka nitampigia muhusika wa zahanati hiyo ili anipe taarifa kamili," alisema Mahuu.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Thomas Epson, alisema hana taarifa yoyote kuhusu tukio hilo na aliahidi kulifuatilia na atavijulisha vyombo vya habari.




Baadhi ya wananchi wa Kata ya Kifula, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro, wakiwa kwenye uzinduzi wa mradi shirikishi wa kusaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi unaotekelezwa kwenye kata tatu za wilaya hiyo, jana. Kushoto (aliyeshika bango) ni Mwakilishi wa wahisani kutoka Ujerumani, Dk. Regine Brandt na (wa tano kulia) ni Mratibu wa Idara ya Maendeleo wa Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Pamela Mainda. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

## Walalamikia kukithiri biashara dawa za kulevya mtaani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa Barabara ya Njia Panda ya Marangu Mtoni, mkoani Kilimanjaro, wamesema usafirishaji wa magendo, biashara ya dawa za kulevya, kwa vijana katika eneo hilo imekuwa ni kikwazo cha kukwamisha kazi za maendeleo na kuchochea ukatili.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi katika eneo hilo, akiwamo Laurent Meena, alisema licha ya kuwapo kwa jitiada zinazofanya na Jeshi la Polisi kudhibiti matukio hayo, lakini bado matatizo hayo yanaikumba jamii ya eneo halo.

"Biashara ya dawa za kulevya inafanywa na kundi la vijana waendesha pikipiki, wanapita kwa kasi ya ajabu, hofu yetu kuna watoto wadogo wa shule za awali huwa huo ndiyo muda wao wa kutoka shuleni.

"Kwa sasa wazazi wanaogopa kuwaacha watoto waende shule wenyewe hivyo inawalazimu kuacha shughuli za kujiingizia kipato ikiwamo kutoka shambani kwenda kuwachukua watoto shuleni,"alisema Helen Mkenda.

Akijibu suala hilo, Katibu wa Chama cha Waendesha Pikipiki Mkoa wa Kilimanjaro, Rashidi Omary, alisema kuna baadhi ya watu wamenunua pikipiki kwa ajili ya kufanya uhalifu, hivyo, aliliomba Jeshi la Polisi kuhakikisha wanakamatwa.

"Usafiri wa pikipiki ulikuja kwa ajili ya kuzisaidia jamii yetu na siyo vinginevyo, hawa wachache wanaotaka kutuchafua sisi kama chama hatutakubaliana, tutashirikiana kuhakikisha tunawafichua na kutokomeza uhalifu," alisema.

Aliongeza: "Natoa rai kwa viongozi wa vijiwe vyote na wanachama, wakumbuke jukumu la kulinda kijiwe chao liko mikononi mwao usiku na mchana, pia tushirikiane na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha wateja wanaokuja kijiweni hawapati madhara."

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliliagiza Jeshi la Polisi, kuhakikisha wanawasaka wauzaji, wasafirishaji na watumiaji wa dawa za kulevya popote waliko.

Babu alisema: "Umefika wakati wananchi kutazama upya tabia za baadhi yetu, kuwaficha wahalifu hao, hakika hili haikubaliki tuachane na shughuli ya usafirishaji wa bangi na mirungi, kwa kuwa kazi hii inawaharibu watoto wetu na kuongeza ukatili.

"Nawapongeza vijana wa Jeshi la Polisi, wanafanya kazi usiku na mchana, endeleeni mpaka siku tutafanikiwa kudhibiti dawa za kulevya yasiwapo tena katika jamii," alisema.



Ukurasa 16

**Wingi wanawake haujatafsirika kiuchumi, kisiasa kwanini hasa?**



Ukurasa 18

Baada ya uchaguzi ulaji wa mabilioni waripotiwa

siasa

JUMATANO SEPTEMBA 21, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 19

**ELIZABETH TRUSS, THERESE COFFEY**

**Vigogo wakuu wanaoiongoza Uingereza baada ya Johnson**

SIKU YA DEMOKRASIA

# Viongozi wa dini walipowashukia wenzao kujifanya sehemu ya siasa

- Komu: Wanahabari nanyi mko humo

**Na Sabato Kasika**

SIKU ya kilele cha Demokrasia Duniani, ambayo iliendelea kuwa mwendelezo wa kumbukizi ya miaka 30 tangu kurejeshwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini, inajadili mengi kuhusu kurutubisha demokrasia, amani na utulivu lakini pia kuwatupia macho wanaojigonga kwa wanasiasa ili kufanikisha maslahi binafsi.

Ilikuwa Septemba 15, wiki iliyopita kwenye kilele cha maadhimisho hayo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) cha Dar es Salaam, kiliandaa mjadala unaohusu tafakuri ya miaka 30 ya demokarsia ya siasa za ushindani nchini unaowakutanisha wadau wa siasa na wengine mbalimbali.

Miongoni mwa wadau walioalikwa katika mjadala huo uliofanyika jijini Dar es Salaam, ni viongozi wa vyama vya siasa, dini, asasi za kiraia, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Lilianza neno la kukemeana kuhusu viongozi wa dini kutosimamia linalowapasa badala yake wanasaka maslahi yao, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, anasema kwa miaka 30 tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini, kumekuwa na hoja ambayo Watanzania wameendelea kuwa nazo dhidi ya viongozi wa dini ambao sasa wanatakiwa kuzifanyia kazi

"Watanzania wanahoji, mbona kuna moja mbili tatu na sisi viongozi wa dini tunakabiliwa na ukosefu wa maadili kwenye zoezi zima la uchaguzi Tanzania imepoteza hadhi yake kimataifa kutokana na ukosefu wa maadili kwenye kusimamia uchaguzi," anasema Padri Kitima.



Shekhe Issa Ponda (kushoto), akiwa miongoni mwa waalikwa katika mjadala wa miaka 30 ya urejeshwaji wa mfumo wa vyama vingi nchini. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Katibu Mkuu huyo anawataka viongozi wa dini kusimamia ukweli na kwamba kuna hatari kubwa iwapo watashikamana na viongozi wa serikali kwa malengo ya kisiasa na badala ya kusimamia maslahi ya umma.

"Taasisi za dini zimeshiriki kwa karibu kukuza demokrasia ya vyama vingi vya siasa tangu kurejeshwa mfumo huo miaka 30 iliyopita, hata tuliponyamazishwa tuliendelea kutoa elimu ya uraia kwa uwazi na siyo kificho," anasema Kitima bila kufafanua.

Anaungwa mkono na Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha NCCR- Mageuzi Tanzania Bara, Anthony Komu, anayewataka viongozi wa dini na waandishi wa habari kutokaa kimya wanapoona vyama vya upinzani vinaonewa.

"Viongozi wa dini na waandishi msijipendekeze kwa wanasiasa tumieni nafasi zenu kukosoa na siyo kuegemea upande mmoja wakati mnaona vyama vya upinzani vinanyanyaswa, vinanyimwa haki ya kufanya siasa," anasema Komu.

Aidha, Kiongozi wa Jumuiya na Taasisi za Kiislam, Shekhe Rajabu Katimba, anawashukia viongozi hao, akidai walio wengi ni wanafiki, huku akikumbusha kuwa kiongozi wa dini anatakiwa kwanza kumtumikia Mungu, kutenda haki, kusema ukweli na kuonyesha matendo ya huruma na pia kukemea vitendo vinavyokwenda nje ya mstari.

"Viongozi wenye msimamo dhaifu ndio wanaokumbatiwa na serikali, lakini kiongozi wa

**INAENDELEA UK. 20**

# Mauaji, uvamizi 'panya road' liwe funzo polisi wanapojipanga upya



Ulinzi shirikishi kukabiliana na wahalifu usitegemee polisi na sungusungu hata wanyama kama mbwa maalumu wanaweza kutumiwa kukabiliana na maeneo yenye uhalifu sugu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

WAKATI serikali na wadau wameanza kujipanga kutoa hoja za nini kifanyike ili kubadili taswira ya Jeshi la Polisi kwenye kushughulikia haki jinai inayohusisha kukamata, kuweka rumande, upelelezi na kufikisha mashtaka mahakamani, wimbi la mauaji ya panya road linaleta tafakuri mpya.

Ni kutolewa kwa maagizo rasmi ya bunge kuwa serikali ishughulikie kwa haraka suala la wahalifu wenye umri mdogo 'panya road' ambao wameibuka na kuvamia mitaa kwenye miji na majiji ikiwamo Dar es Salaam, na katika tukio mojawapo walimwua mwanafunzi wa mwaka wa pili wa chuo kikuu aliyekuwa anasomea uandishi wa habari.

Kinachoonekana ni kuwa taifa limechoshwa na hali hiyo hivyo ni hitaji la maelekezo kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa wanaohusika na hali hiyo wanaondolewa mitaani.

Suala la taratibu zitakazofuatwa halipo katika hitaji hilo, ila kutokomeza wimbi la watoto wahalifu na wauaji wanaojiita panya road, ambao wazazi na walezi wao wamepata matatizo ya kuwalea, sasa inabidi walelewe na vyombo vya dola, ikielezwa kuwa ni njia pekee ya kuwezesha usalama kudumishwa mitaani.

Akitoa tamko la kuanza kutekelezwa kwa maagizo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, anawaasa wazazi na walezi wa watoto au vijana hao kuwa endapo hatakuwa amemwona mwanae, kwa kitambo cha kuleta wasiwasi, basi amtafute kituo cha polisi au hospitalini.

Wachambuzi wa habari katika baadhi ya redio nchini wanasema angesema wamtafute kwenye vyumba vya kuhifadhi miili hospitalini wakimaanisha kuwa huenda atakuwa ameshapigwa risasi na kufa. Na siyo kwamba waliongeza hiyo chumvi kwa wasiwasi na taharuki, ila kwa ufafanuzi muafaka.

> Serikali inaongeza Shilingi bilioni 100 kila mwezi kupunguza makali ya bei ya mafuta, hivyo haina nafasi ya kuongeza bei katika eneo hilo.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akionyesha silaha zinazodaiwa kuwa za 'panya road' . **PICHA: MAKTABA**

Suala hapa ni kuwa wimbi la 'panya road,' nje ya mauaji yenye sura ya kuchanganyikiwa au ushirikina, limehamasisha uelewano kiitikadi unaohitajika kwa hiyo ajenda ya kubadilisha kanuni na taratibu za Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai.

Huenda kinachotazamwa ni kulinda haki za watuhumiwa, wasikamatwe na kuwekwa rumande ili upelelezi ufanyike, ila polisi wamalize kwanza upelelezi ndipo wawakamate.

UGumu unaanzia pale inapokuwa vigumu kuwaambia, wakazi wa Dar es Salaam na maeneo mengi wawe wavumilivu na watulivu hata kama kuna mashambulizi mengine ya 'panya road,' ili kufanya upelelezi wa makundi hayo ambauyo pengine siyo rahisi!

Changamoto kwa mabadiliko hayo ambayo kwa jumla yalianza kuwa 'ncha ya mkuki' wa mabadiliko ya katiba kwa jumla, ni ishara kuwa hata hayo matazamio yako mashakani, kwani msingi wake ni uhuru mpana wa raia.

Kama ilivyo katika suala hilo la upelelezi wa makosa ya jinai, mabadiliko yanayolengwa yanawezesha mhalifu kuendelea na shughuli zake mradi polisi hawajapata ushahidi wa kutosha dhidi yake, unaoweza kusimama mahakamani. 'Panya road' wakisikia hayo, ni shangwe na kujiamini.

Wanaotaka uhuru mpana wa mtu binafsi, kupunguza udhibiti wa matendo ya mtu mmoja mmoja kwa kutumia vyombo vya dola, kimsingi wanaanzia katika dhana dhaifu kuwa binadamu ni mwema. Anazaliwa na kukua katika familia, anafundishwa maadili na dini na uhalifu ni kukosea kwa mithili ya kujisahau na kwa maana hiyo anahitaji kurekebishwa, kupewa mafunzo ya kuishi kwa tija kama watu wengine.

Ndiyo hapo linakuja suala la kutomwondolea uhuru wake bila uhakika wa kina, kwa maana ya kukusanya ushahidi unaoweza kusimamisha kesi mahakamani akiitwa na kufunguliwa mashtaka.

Unaweza kusema kuwa hitaji hilo la kutaka utendaji wa Jeshi la Polisi ubadilike na uhuru wa mtuhumiwa uongezeke umechangia kwa kiasi fulani kuongezeka na kushamiri kwa wimbi la ujambazi na uhalifu ukiwamo wa 'panya road.'

Ni mazingira ambako wahalifu wamepindua meza ya hitaji la mabadiliko utendaji Jeshi la Polisi baada ya jamii na bunge, kutaka kadhia hiyo iondolewe kwa njia zozote zile, hata kama ni kuwapiga risasi wahalifu sugu waliozoea kwenda rumande na kurudi uraiani ili kuendeleza uovu huo.

Kimsingi ni vijana wasiotibika, waalimu wa 'panya road' wapya, waliopata picha kuwa sasa mambo ni mazuri, pengine wakihoji polisi watamaliza upelelezi lini?

Licha ya kuwa suala hili ni tofauti na tozo, ambako pia Rais Samia Suluhu Hassan, alipokea ushauri akaukubali na kuiruhusu Hazina kuboresha tozo ukilinganisha na ilivyokuwa mwaka jana, yanafanana kimsingi jinsi ya utoaji wa haki jinai. Katika hali hii ya wimbi la ujambazi-uchwara wa 'panya road,' haitakuwa rahisi kwa Rais Samia kumwambia Waziri wa Mambo ya Ndani au mkuu wa Jeshi la Polisi kuwa mtu asikamatwe bila uchunguzi kufikia tamati na kuwa tayari kufikisha kesi hiyo mahakamani.

Hata kama yako maeneo ambapo kanuni hiyo inaweza kutumika bila madhara kwa mustakabali wa jamii, ni wazi kuwa watuhumiwa wa 'panya road' hawatahusika.

Na wanaodaiwa kuwa majambazi wote sawia, na kwa maana hiyo itakuwa ni kesi za madai ya kodi na wizi wa kalamu kanuni zinaweza kurekebishwa mtu akawa huru upelelezi ukiendelea, watu wasijali.

# Kinana alipotikisa, kuangusha ngome kampeni za kidini, ukabila uchaguzi

**Na Beatrice Shayo**

ZIARA ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, imeibua shangwe mikoani kwa namna alivyowateka wananchi kwa kuwapa nafasi ya kuwasilisha kero zao na zikatatuliwa papo hapo, lakini pia kukemea figisu ndani ya uchaguzi wa chama hicho.

Kinana kuanzia Agosti 16 alizuru mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita na Mwanza akiambatana na Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka, akilenga kukagua uhai wa chama, utekelezaji wa ilani na kusikiliza kero za wannachi.

Akianza kuzungumzia uchaguzi anawaambia wananchi kuwa kiongozi anayetaka kuchaguliwa kwa kutumia udini na ukabila ni adui wa maendeleo hafai ndani ya CCM wala kwenye jamii na chama kikimbaini aondolewa jina lake mara moja na asipewe nafasi.

Kinana anatema cheche baada ya kupatiwa taarifa kutoka kwa Katibu wa CCM Mkoa wa Kigoma, Mobutu Malima, kuhusu kuwepo kwa viongozi wanaotumia udini katika kampeni kipindi cha uchaguzi.

"Jambo moja ambalo niliseme lipo katika taarifa ya katibu wa mkoa kwamba inavyofika wakati wa uchaguzi katibu wa mkoa na kamati ya siasa imeonyesha ujasiri wa kuandika kuwa kuna tatizo la ukabila, ukanda na udini,"anasema Kinana.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana katika kazi za kufuatilia utekelezaji wa ilani ya CCM. **PICHA: MAKTABA**

### UDINI, UKABILA 'NO'

"Sijui kama mnazikumbuka hotuba za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kuhusu ukabila. Tunavyokwenda karne ya 21 umepanda bado basi la ukabila hili lilimuudhi Mwalimu Nyerere tangu zamani. Wapo Wakuu wa Wilaya hapa wametoka mikoa mingine na wengine wameishi hapa wanajulikana wanathaminiwa, wanagombea, wana sifa na wanafaa halafu unamhukumu kwa kitu kimoja kabila lake hii sio sawa." Anaonya.

Anasema kiongozi anaona mambo yake hayaendi vizuri na fursa ya kuchaguliwa haipo anaamua kueleza fulani sio mwenzao, si kabila analotaka au si wa ukanda huo na hata dini, na kwamba huo si wakati wake.

"Wanachama hawana hayo matatizo mtu achaguliwe kwa sifa zake, apimwe kwa uwezo wake, kwa historia yake ya utendaji lakini isifike mahali ukasema huyu kabila langu. Kabila lako ovyo, mvivu, hana uwezo, hafai, hajui hata anachokiomba eti tunatoka eneo moja, je anakusaidia kitu gani hana mawazo hana jambo jipya na kuleta maendeleo. Hakufai ,"anasema Makamu Mwenyekiti Bara.

"Tukikaa na kuanza kuhukumiana kwa ukabila... ukiona mtu anahukumu wengine kwa ukabila mwenyekiti tafadhali mkateni jina lake, achaneni naye na sisi tunawatafuta hao watu wa aina hiyo,"anasema Kinana.

> unapokuwa kiongozi unatakiwa kutenda haki na wakati mwingine kutumia busara ili jambo limalizike kwa wakati na wananchi kuwa na amani.

Akizungumzia uchaguzi, Kinana anasema kumekuwa na figisu zinazofanyika katika uchaguzi unaoendelea ndani ya chama tena kuna viongozi wanaonunia wenzao wanaotaka kugombea huku wakitumia rushwa ili wasiondolewe.

Anasema wana CCM kuchukua fomu sio dhambi ni haki yao ya kikatiba na hakuna mwenye hati miliki ya chama hicho, hivyo kila mmoja ahusike na uchaguzi na wala asiogope uongozi kandamizi.

Anaeleza utaratibu wa chama kuwa wanaochaguliwa hukaa kwa miaka mitano baada ya kumalizika nafasi zipo wazi na yeyote anayetaka kugombea yupo huru kufanya hivyo.

"Mtu anataka kugombea ikibainika anaacha urafiki siku hiyo hiyo, kiongozi ananuna utafikiri amegongewa misumari kwenye kiti, hataki kuondoka anajisahau na yeye alimtoa mwingine katika nafasi hiyo, tuache nongwa ndugu zangu" anasema Kinana

Anaeleza kuwa wakati wakitafuta uongozi wamekuwa wanafanyiwa mizengwe kwa kuwakata majina yao na kusingiziwa uzushi, huku wengine wananyimwa fomu za kugombea nafasi hizo.

"Sababu ni moja ubinafsi. Viongozi wanataka watu wao ndiyo wachaguliwe sio watu wanavyotaka bahati nzuri mnawajua viongozi wanaotumia nafasi zao, wanaowanyima wenzao nafasi, wanaotengeza mizengwe, wanaotaka wachaguliwe watu wanaowataka wao hawafai. Na mimi naomba kiongozi wa namna hiyo akifika katika uchaguzi mpigeni chini hafai," anahimiza Kinana.

Anaeleza kuwa inashagaza kuona baadhi ya viongozi wanajisahau walipoingia madarakani waliwakuta wenzao wanapoona wanaotaka kugombea wanawainulia vikwazo hilo halipo sawa.

"Kiongozi anaetaka kuingia madarakani kwa kutisha watu, kwa upendeleo, mizengwe ni shida. Kila mmoja ana haki ya kuchaguliwa na kuchukua fomu, CCM imasimama kwa kuzingatia katiba, kanuni, miongozo na sio viongozi wenye mizengwe" anawaeleza Kinana.

Aidha anakemea kiongozi anayetumia fedha kusaka uongozi akiwaambia wana CCM kuwa hawafai na kwamba wapo baadhi yao hawana fedha wanaogopa hata kuchukua fomu licha ya kuwa na sifa zinazohitajika.

### KERO ZA WANANCHI

Katika eneo hilo Makamu Mwenyekiti wa CCM anatoa muda mwingi kusikiliza kero za wananchi huku akiwataka viongozi wa serikali walioguswa kutoa majibu hapo hapo badala ya kuchelewesha haki za wananchi.

Anawaambia chama kazi yake ni kuwasikiliza watu kwa kuwa ndiyo wenye chama na viongozi watakaoguswa watoe majibu yenye tija badala ya kuwazungusha Watanzania hao wenye kero.

Kitendo hicho kiliwavutia wananchi huku wakimshangalia kwa kuendesha mambo kwa uwazi ambayo wanasema yatasaidia kutambua figisu figisu wanazofanyiwa na kuongeza uwajibikaji kwa viongozi hao.

Kinana akiwa Kigoma alikerwa na kisa cha mwananchi kudhulumiwa ardhi na Manispaa akiwa kwenye matibabu na baada ya kurejea mkoani humo, ikawa imeuzwa kwa mwingine na kupewa hati.

Kinana anasema: "Ni jambo la kushangaza kwa mwananchi huyu kuzungushwa ardhi yake na viongozi mmekiri eneo ni lake, hivyo jambo hilo halihitaji ucheleweshaji, limalizwe."

Anasema unapokuwa kiongozi unatakiwa kutenda haki na wakati mwingine kutumia busara ili jambo limalizike kwa wakati na wananchi kuwa na amani.

"Nashauri huyu mwananchi mpatieni ardhi eneo jingine hata kama ni mjini ninyi ndiyo wenye makosa kwa nini anateseka na ardhi yake hata kama hana uwezo wa kujenga nyumba ya kisasa katika maeneo hayo mpatieni,"anaagiza Kinana.

Anaongeza :"Anaweza akawa hana uwezo wa kujenga nyumba ya kisasa katika hayo maeneo lakini akawa na uwezo wa kuuza ardhi na kujenga kijijini na hela nyingine akabakiwa nazo tena akaanzisha biashara.Tusicheleweshe haki za wananchi,".

### SHERIA KANDAMIZI

Kinana anazungumzia sheria nyingi ambazo ni kandamizi akisema zinatakiwa kufanyiwa kazi ili kuwaondolea mzigo wananchi badala ya kuendelea kuteseka.

Anasema dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni njema kwa wananchi katika kuwakomboa kiuchumi na hayupo tayari kuona wanawekewa sheria ngumu wakati lengo ni kuwarahisishia maisha Watanzania.

"Niwambie mimi ni msaidizi wa Rais najua msimamo wa wake anataka kuondokana na sheria zote zinazoleta vikwazo kwenye shughuli za wananchi, kazi yangu na viongozi wengine ni kumpa moyo kumwambia njia unayokwenda ni sawasawa,"anasema Makamu Mwenyekiti wa CCM-Bara.

Kinana anawaambia wananchi kuwa Aprili mwaka huu wakati Rais Samia akizungumza na mawaziri baada ya kuwaapisha aliwaomba wapitie sheria zote, waangalie zile zinazokwaza maendeleo ya wananchi, zinazowapa shida na zinazokanyaga haki wampelekee apeleke bungeni zifutwe.

"Sasa nina mpango wa kwenda kuwauliza wakubwa tangu walipoambiwa wameshapeleka sheria ngapi ili zifutwe? Hiyo ndiyo kazi tuliyonayo,"anasema.

Wananchi wanawategemea wao kuwasaidia kuinua kipato chao, hivyo madiwani wanaotunga sheria za halmashauri, watendaji wa serikali ambao wanasimamia sheria za halmashauri na za nchi, wanatarajia wabunge kutengeneza sheria na kanuni rafiki kwa Watanzania ziwasidie kufanya shughuli zao kwa urahisi na ufanisi anasema.

KUKABILI WALIO MITAANI:

# Wadau wanahimiza utashi wa kisiasa utumike kuwasaidia



Waziri Dorothy Gwajima (wa tatu kushoto), alipozungumza na baadhi ya watoto mitaani.

**Na Sabato Kasika**

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeanza mkakati wa kuwaondoa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, ili kupunguza matatizo ya kijamii, kuwasaidia kusoma na pia kuondoa umaskini miongoni mwa watoto.

Wakati serikali ikiendelea na mkakati huo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kaya Foundation inayojishughulisha na malezi ya watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi, Annapili Ngome, anasema utashi wa kisiasa una nafasi kubwa kufikia azma hiyo

Katika mazungumzo yake na gazeti hili jana, Mkurugenzi Annapili anasema inawezekana tatizo lisimalizike, lakini anaongeza kuwa bado kuna haja kwa kila mdau kufanya sehemu yake kukabiliana na wimbi la watoto wa mitaani.

"Nina maana kwamba, wanasiasa ambao kimsingi wana ushawishi mkubwa kwenye jamii, wanaweza kuhamasisha jamii kuzingatia malezi bora kwenye maeneo yao ili kupunguza wimbi la watoto wa mitaani," anasema Annapili.

Anafafanua kuwa wanasiasa wakijitenga kwenye suala la kuhamasisha malezi bora na kuangalia maslahi yao kwenye sanduku la kura tu, inawezekana juhudi zinazofanywa na serikali zisizae matunda.

"Kwa kawaida, wanasiasa wanajikita zaidi kwa watu wenye umri wa kupiga kura na kuacha kundi la watoto, kwa sababu hawana msaada katika mikakati yao ya ushindi, lakini wakumbuke kuwa watoto ni wapigakura wa miaka

> "Nina maana kwamba, wanasiasa ambao kimsingi wana ushawishi mkubwa kwenye jamii, wanaweza kuhamasisha jamii kuzingatia malezi bora kwenye maeneo yao ili kupunguza wimbi la watoto wa mitaani.

ijayo, hivyo wasiwatenge kwa namna yoyote ile," anasema.

Mkurugenzi huyo anawashauri wanasiasa kuungana na serikali na wadau wengine kuhamasisha malezi bora, ili kuandaa watoto ambao wanategemewa kuwa taifa bora la baadaye badala ya taifa bovu la baadaye.

"Tunaweza kuitengeneza Tanzania ya kesho, kwa kuwekeza katika maslahi mapana ya watoto kimaadili, kiuchumi na kielimu, hivyo utashi wa kisiasa ni muhimu kwenye suala zima la malezi bora," anasema.

### KUWEKEZA KATIKA MALEZI

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, Seleman Biashagazi, anasema pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali za kuondoa watoto wa mitaani, ipo haja kwa jamii kuwekeza zaidi katika malezi bora.

"Kuna sababu mbalimbali ambazo zinatajwa kuhusu watoto kukimbia kutoka kwao na kwenda mitaani, lakini ninaamini kuwa malezi duni ni chanzo kikuu cha kuwapo kwa watoto wa aina hiyo," anasema Bishagazi.

Anasema ndani ya familia kuna unyanyasaji wa aina mbalimbali na ukatili kwa watoto ukiwamo wa kijinsia, kimwili au kihisia, na kwamba hali hiyo inawalazimu kukimbilia mitaani.

"Hivyo kwa hali kama hiyo, ninadhani ipo haja ya kuwekeza nguvu kubwa kwenye malezi bora, lakini pia kuhakikisha kunakuwapo na maofisa wa ustawi wa jamii kuanzia ngazi ya chini ili watoe msaada wa kisaikolojia," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema aliwahi kwenda wilaya moja na kukuta ina maofisa ustawi wa jamii wanne, ambao anafafanua kuwa



Mkurugenzi wa Taasisi ya Kaya Foundation, Annapili Ngome anayetamani utashi wa kisiasa utumike kumaliza wimbi la watoto wa mitaani. **PICHA: SABATO KASIKA**

ni vigumu wachache hao kuweza kuhudumia watu wote katika wilaya hiyo.

"Nikumbushe tu kwamba, watoto ndio viongozi wa baadaye, lakini inasikitisha kuona wabunge, madiwani katika maeneo yao wakiwa kimya bila kusaidia kuhamasisha malezi bora," anasema.

### MKAKATI WA KUWAONDOA

Hivi karibuni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima alifanya ziara ya kushtukiza maeneo ya Ubungo mkoani Dar es Salaam na kukutana na kikundi cha watoto hao.

Katika ufafanuzi wa ziara hiyo, anasema baadhi ya watoto hao walimwelezea sababu za kuwafanya wakimbie nyumbani kwao na kuonyesha migogoro ya familia, ni chanzo cha wao kukimbilia mitaani.

"Sio kwa sababu wazazi hawana uwezo au wamefariki, bali ni kwa sababu ya migogoro iliyopo kwenye familia ikiwamo wazazi kutengana, migogoro ya urithi ambayo inasababisha watoto wakimbilie mitaani ili kuepuka kuishi na mzazi wa kambo au kwa ndugu badala ya kuishi na wazazi wake,"anasema.

Anaongeza kuwa, katika mazungumzo yake na watoto hao wa kati ya miaka 12 hadi 17, anasema alibaini wamechoka kuishi maisha ya kuomba omba na wako tayari kurejea mikoa walikotoka, ili kuungana na familia zao.

"Wanadai katika maisha hayo ya mtaani, wamekutana na changamoto mbali mbali ikiwamo kutumiwa na baadhi ya wananchi kuwafanyia biashara na kuwapa ujira mdogo, kujiunga na makundi ya vijana wavuta bangi na watumiaji wa dawa za kulevya, kushiriki vitendo vya wizi, ulawiti, ubakaji na kupata magonjwa mbalimbali yanayohatarisha afya na kupoteza ndoto za maisha yao ya baadaye," anasema Dk. Gwajima.

Aidha, Dk.Gwajima anawataka watoto wote wa mitaani waliopo maeneo mbalimbali nchini, kutoa ushirikiano kwa maafisa maendeleo ya jamii, ili serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, ikiwamo wamiliki wa vyombo vya usafiri na Jeshi la Polisi kuwasafirisha, ili waungane na familia zao.

"Lakini pia niwatake wazazi na walezi kusikiliza ndoto za watoto wao na kubaini wanachohitaji, ili waweze kusoma na kufikia malengo yao, badala ya kuwapotezea malengo walionayo kwa ajili ya maisha yao," anasema.

### WAPATE USHAURI NASAHA

Mtaalam wa saikokojia Roselight Ringo anasema, hatua inayochukuliwa na serikali ya kiuwaindoa watoto hao mitaani ni ya muhimu, na kwamba kabla ya kurudishwa nyumbani waandaliwe kisaikolojia kwanza.

"Unajua wanapokuwa katika mazingira hayo ya mitaani, wanajiona kama hawapendwi na jamii na hata wenyewe hawajipendi, hivyo muhimu wakalishwe chini ili kuwaondoa katika hali hiyo," anasema Roselight.

Anasema bila kuwapeleka kwa watu wa saikolojia ili wapate ushauri nasaha, watoto wanaweza kuondolewa mitaani wakafika nyumbani wakaanzisha vitendo vya ukatili kwa wenzao au kurudi tena mitaani.

Msaikolojia huyo anayefanya kazi katika Taasisi ya Children Youth Parent Empowerment Tanzania (CYPE), anasema watu wa saikolojia wakiongea na watoto hao wanaweza kugundua mengi na kutoa ushauri utakaosaidia kuwafanya warudi katika familia zao huku wakiwa ni watoto wema.

MAMA MARIYAM ASHANGAA

# Wingi wanawake haujatafsirika kiuchumi, kisiasa kwanini hasa?

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



Mwenyekiti Taasisi ya Maisha Bora Mariyam Mwinyi pamoja na mke wa Rais wa Burundi, Angeline Ndayishimiye,Ikulu Zanzibar. **PICHA: IKULU**

"LICHA ya wanawake kuwa wengi hapa Tanzania kinachoshangaza na kibaya ni kwamba wingi huo haujatafsiriwa katika nguvu ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na katika maendeleo ya taifa."

Ni maneno ya kuuumiza moyo wa mama, anayoyatoa Mwenyekiti wa Taasisi ya Maisha Bora (Zanzibar Maisha Bora Foundation) Mariyam Mwinyi, mke wa Rais wa Zanzibar Hussein Ali Mwinyi.

Anasema takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwa asilimia 51 ya Watanzania ni wanawake lakini bado linabakia kutazamwa kama kundi dhaifu linalohitaji huruma, fadhila na stara, jambo ambalo wakati umefika wa kulifanyia kazi.

Mama Mariyam anazungumza kwenye kongamano la masuala ya wanawake linaloandaliwa na Taasisi ya Mtandao wa Kuinua Wanawake Tanzania -Tawen hivi karibuni mjini Zanzibar.

"Wanawake mashujaa wapo na wamefanyakazi kubwa, kama waliotangulia akiwamo Bibi Titi Mohamed kwa Tanzania Bara na Biubwa Amour kwa Zanzibar na wengine walitoa mchango mkubwa katika harakati za Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar wakiwa na elimu ndogo, fursa kidogo na nyenzo duni kuliko wanawake wa sasa. Wamefanya makubwa. Hili linashangaza, kina mama mko wapi?"

Kwa sasa hakuna kisingizio cha kuwafanya wanawake kutofanya mambo makubwa zaidi ya mashujaa hao waliotangulia kwani zama hizi kinamama wana elimu zaidi, fursa na teknolojia ya kisasa, anasema Mama Mariyam.

"Tuna kisingizio gani safari hii ya kutofanya mageuzi makubwa ambapo Rais wa Tanzania ni mwanamke? Tena wanawake walioshika hatamu katika nyanja nyingi za uongozi lakini pia Rais wa Zanzibar ni muumini na muhamasishaji mkubwa wa maendeleo ya wanawake?"Anahoji Mwenyekiti wa Maisha Bora Zanzibar.

Anaongeza kusema "Watu wa pwani wanasema kuwa kijua ndiyo hiki tusipouanika tutautwanga mbichi hivyo silaha ya kwanza ni kupambana na unyonge, tena tuwe na umoja ili kuwa na sauti moja"anaeleza.

Aidha, anawaambia wanawake kuwa waangalie inavyoelekea wamekosa jukwaa la kujiunganisha pamoja juhudi zao na matokeo yake wanashindana kuhasimiana na kuhujumiana badala ya kushirikiana.

"Wakati wa mwanamke ni sasa zinduka ni sahihi sasa kuliko wakati wowote, leo hii wanawake tumesoma zaidi, tuna kipato zaidi na tunafursa zaidi za kubadilisha hali zetu tukilinganisha na huko tulikotoka"anasema Mama Mariyam.

Takwimu za Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), zinaonyesha kuwa ni wanawake nane pekee ndiyo walioshindana katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kati ya kinamama 61 waliogombea nafasi ya uwakilishi majimboni,wakati wanaume waliogombea nafasi hiyo na kushinda ni 42 kati ya 190 waliojitokeza.

Kwa upande wa nafasi za ubunge wanawake, walioshinda ni wanne kati ya 81 waliojitosa majimboni wakati wanaume walioshinda ni 46 kati 257 waliogombea na madiwani wanawake walioshinda ni 25 kati ya 74 waliogombea katika wadi wakati wakiongozwa na wanaume ambao katika mchuano huo walioshinda ni 85 kati ya 276 walipanda ulingoni kugombea.

Mama Mariyam anasema licha ya Tanzania kuchukua juhudi ya kuongeza nafasi za uongozi kwa wanawake lakini hata hivyo hali halisi ya ushiriki wao bado hairidhishi ikilinganishwa na wanaume ambao kwa miaka takribani 60 ya Uhuru wamedumu kwenye uongozi.

Anaeleza kuwa wanawake ambao wameshika nafasi za mbalimbali za uongozi ni chachu ya kuleta mabadiliko katika nchi na tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa wanawake wanafanya vizuri katika nafasi za uongozi kutokana na ukweli kwamba ni watu wa kutimiza ahadi, viongozi wa kujitolea, si wapenda rushwa, wanaheshimu usawa wa kijinsia na waadilifu.

Anasema ili wanawake kufikia usawa wa kijinsia kwa uwiano wa asilimia 50/50 ni vyema wakazifahamu vizuri sera na sheria ili kuwasaidia kusimama imara katika kujieleza bila ya kuvunja utaratibu wa nchi hasa wanaposaka uongozi na kulitumikia taifa katika maeneo mbalimbali.

Anaamini kuwa hatua hiyo kwa kiasi kikubwa itawasaidia kuondoa ubaguzi uliopo baina ya wanaume na kuwainua wanawake kimaendeleo badala ya kuendelea kubakia kwenye uongozi usio na uwiano sawa baina ya wanawake na wanaume..

"Sera zenye malengo ya kuwainua wanawake na kufikia malengo ya uongozi zipo lakini kwa bahati mbaya wanawake hawazifahamu ikiwamo ya maendeleo ya wanawake,utawala bora pamoja na ushirikishwaji wa wanawake katika siasa"anakumbusha.

Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Zanzibar (TAMWA) Dk. Mzuri Issa, anamuunga mkono mke wa Rais akisema mahitaji ya kimkakati wa kivitendo yanahitajika nchini ili kuwanyanyua watoto wa kike kukua katika uzoefu wa masuala ya uongozi na kupaza sauti za ili zisikike pale inapostahiki.

"Nataka kuwasisitiza vijana wa kike kwamba huu sio wakati wa kujishughulisha katika vitendo vya anasa badala yake ni vyema kujiwekeza katika kugombea nafasi za uongozi kwa ajili ya kuyafikiya maendeleo yawe ya kiuchumi, kisiasa, kielimu na kijamii,"anasema Mzuri.

Mwanzilishi wa Taasisi ya Uwezeshaji Maendeleo Binafsi (The Purple Planet), Hilda Kisoka, anasema wanawake wanao wajibu kuwainua wenzao ambao wapo chini ili nao watoke kimaisha kwa kuangalia fursa mbalimbali zilizoko na zinazojitokeza.

Anasema katika kazi za kuisaidia jamii hakuna sababu ya kushindana kikubwa ni kufanya kazi kwa malengo ya kuiinua hivyo ni vyema kuingia ubia katika kutimiza malengo hayo lakini kila mmoja akishirikishwa ili pasiwepo na unyanyasaji wa kijinsia.

> Serikali itatoa kipaumbele kwa wanawake katika kila wizara kushiriki kazi za uhandisi, ufundi umeme na nyingine ili kuweka usawa kwa wanawake wenye sifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Mtandao wa Kuinua Waneweke Tanzania -Tawen iliyoandaa kongamano hilo, Tunu Pinda, mke wa Waziri Mkuu mstaafu Tunu Pinda, anasema umefika wakati sasa kuwa na ushirika wa kiviwanda , njia itakayofanikisha kuwainua wanawake wengi ikilinganishwa na hali ilivyo sasa.

Anasema : "Iwapo wanawake wakiwa na viwanda vya pamoja hatua hiyo itafungua fursa zaidi, kutoa ajira nyingi, kuwapa majukumu ya kazi rasmi wanawake, yakihusisha kufikia masoko mengi ya nje kwa maana viwanda hivyo vitakuwa na ubora na uzalishaji wa kukidhi mahitaji ya wateja wan je na ndani".

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar, Zena Ahmed Said, anasema serikali itatoa kipaumbele kwa wanawake katika kila wizara kushiriki kazi za uhandisi,ufundi umeme na nyingine ili kuweka usawa kwa wanawake wenye sifa.

Zena ambaye ni mhandisi na mwanamke wa kwanza Tanzania kushika wadhifa huo, anasema ipo haja kuangalia usawa kwa sekta zote pamoja na kuacha mfumo dume uliopo ekisisitiza kuwa endapo mwanamke amekidhi vigezo apewe nafasi ya ajira kwenye sekta ambazo wengi wanaozitumikia ni wanaume kuliko wanawake.

Anasema utafiti unaonesha kuwa bado kuna idadi ndogo ya matumizi ya nishati za kisasa kwa wanawake kutokana na mitazamo iliyojengeka ndani ya jamii kuwa sekta ya nishati ipo kwa ajili ya wanaume hali iliyopelekea kuwa na wahandisi wachache wanawake.

AFRIKA MASHARIKI/AFRIKA

# Baada ya uchaguzi ulaji wa mabilioni waripotiwa

## • Gashagwa aendeleza vita na Kenyatta

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutinga ikulu Rais William Ruto na serikali yake mpya, wameshtusha wapigakura wao kutokana na taarifa za kuwapo matumizi ya pesa nyingi takribani Shilingi milioni 579 za Kenya kusafiri kwa miezi mitatu hadi uchaguzi ulipofanyika Agosti 9, mwaka huu.

Rais Ruto na mtangulizi wake Kenyatta wanatajwa kuwa waliongeza zaidi ya maradufu ( mara mbili) matumizi ya usafiri wa ndani hadi kufikia milioni 579 katika muda wa miezi mitatu kuanzia Mei hadi Agosti wakati kampeni za uchaguzi mkuu wa Kenya uliompa ushindi Ruto, zikishika kasi.

Ingawa Dk Ruto ndiye aliyekuwa Naibu Rais, Kenyatta alieegemea upande wa kiongozi wa upinzani Raila Odinga, na hivyo kuchochea kampeni mbaya dhidi ya naibu wake kwenye kuwania wadhifa huo mkuu nchini Kenya.

Kuongezeka kwa safari hizo kulisababisha matumizi makubwa ya pesa kwa safari za Ofisi ya Rais Dk Ruto na mstaafu Kenyatta ambayo yameongezeka kwa asilimia 191.3 kutoka Shilingi milioni 198.79 walizotumia katika miezi mitatu hadi Juni 2021, ripoti ya Mdhibiti wa Bajeti inaonyesha.

Shilingi milioni 579 ni sawa na asilimia 66.2 ya Shilingi milioni 873.90 ambazo Ofisi ya Rais ilitumia katika safari za mwaka hadi Juni, ikionyesha kuongezeka kwa safari za wahusika wakuu hao wawili Kenya ikikaribia Uchaguzi Mkuu wa Agosti 9, inasema Ofisi ya Bajeti.

Mwezi uliopita, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Wafula Chebukati, alitangaza kuwa Dk Ruto ameibuka mshindi baada ya kupata asilimia 50.5 ya kura, huku mpinzani wake Odinga akipata asilimia 48.8. Lakini makamishna wanne kati ya saba wa tume ya uchaguzi walikataa matokeo, na kutia shaka ushindi wa Dk Ruto.

Hata hivyo, Mahakama ya Juu ya Kenya, kwa kauli moja iliidhinisha kuchaguliwa kwa Dk Ruto kuwa Rais, ikitupilia mbali ombi lililowasilishwa na Odinga na mgombea mwenza Martha Karua, la kutaka matokeo hayo kubatilishwa.

Kuongezeka kwa matumizi hayo ya usafiri kunakuja huku kukiwa na mpango wa kubana matumizi wa Hazina wa kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo na huduma muhimu kama vile afya na elimu katika nchi inayokabiliana na viwango vya juu vya umaskini na mfumuko wa bei.

Takwimu za ofisi ya bajeti zinaonyesha kuwa serikali ilitumia Shilingi bilioni 20.17 kwa usafiri wa ndani na nje katika mwaka uliomalizika Juni, ikionyesha kuwapo na ongezeko la asilimia 41.9 kutoka Shilingi bilioni 14.21 zilizotumiwa mwaka mmoja uliotangulia.

Mdhibiti wa Bajeti Margaret Nyakango, anataja kuongezeka kwa matumizi ya fedha katika safari na kuondolewa kwa vikwazo vya mikusanyiko ya kijamii na safari za ndege za ndani, na hivyo kuweka mazingira ya matumizi makubwa.



Naibu Rais wa Kenya na Mfalme wa Mlima Kenya, Rigathi Gachagua. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Wangekuwa wakweli kwamba Azimio haiwezi kuuzika kwenye Mlima Kenya, tusingekuwa hapa tulipo leo lakini kwangu mimi ni mkweli na watu wanatakiwa kunizoea.



Rais mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

Matumizi ya serikali yalishuka kufuatia kupiga marufuku usafiri wa ndani hayo yakiripotiwa kutokea mwaka 2020. Aidha, Kenya kupiga marufuku mikusanyiko ya kijamii na kusimamisha safari za ndege za ndani ili kudhibiti ugonjwa wa corona Machi mwaka 2020.

Lakini maofisa hao tangu mwishoni mwa mwaka jana wameanza safari za ndani, hasa kwenda kwenye mafunzo. Wabunge kadhalika walianza kampeni za mapema wakijiandaa na uchaguzi wa Agosti 9 baada ya kupunguzwa kwa vizuizi vya COVID-19 Julai mwaka jana.

### NAIBU RAIS Vs KENYATTA

Naibu wa Rais wa Kenya Rigathi Gachagua (husomwa Rigadhi Gashagwa), amesema hataomba radhi kufuatia matamshi yake yanayodaiwa ni ya kuudhi aliyoyatoa kwa rais mstaafu Uhuru Kenyatta, wakati wa sherehe za kuapishwa kwa Rais William Ruto wiki iliyopita.

Akijigamba kuwa kiongozi mnyoofu, Naibu Rais katika mahojiano na NTV Jumapili iliyopita anasema hakufanya kosa kwa kuwaambia Wakenya 'ukweli'. "Ninasema ukweli bila kujali tukio. Nilizungumza na watu wa Kenya na wale ambao wana wasiwasi hawapaswi kuwa na kile nilichosema.. Wakenya walikubaliana nami," anasema Gachagua

Aidha, anasema hata katika nafasi yake ya sasa ya Naibu Rais, ataendelea kusema ukweli akitamba kuwa kuwa bosi wake Rais William Ruto na yeye mwenyewe walichaguliwa kwa kuzingatia hilo kwa kusema ukweli.

"Ukweli lazima usemwe. "Hata miaka yote nitakayokuwa Naibu Rais, nitasema ukweli ulivyo. Niliingia kwenye matatizo mengi katika utawala uliopita kwa sababu ya kuwa mkweli na siwezi kujiweka mbali na ukweli hata siku moja," anasisitiza.

"Kuna ubaya gani kusema kwamba tumerithi uchumi uliodorora? Huo ndiyo ukweli. Kuna ubaya gani kusema kwamba mashirika ya serikali yalipewa silaha na jukumu la kuwashambulia marafiki wa William Ruto? Ni ukweli ambao kila mtu anajua," anasema Naibu Gachagua.

Anasema uchumi wa nchi uko katika hali mbaya kwa sababu Makatibu wa Baraza la Mawaziri na viongozi wengine wakuu wa serikali waliamua kumdanganya Rais huyo wa zamani.

"Kama maofisa wa serikali wangekuwa wa kweli kwa Kenyatta, hangekuwa amefikia ambapo amefikia leo. Wangekuwa wakweli kwamba Azimio haiwezi kuuzika kwenye Mlima Kenya, tusingekuwa hapa tulipo leo lakini kwangu mimi ni mkweli na watu wanatakiwa kunizoea," anasema .

Anasisitiza kuwa anafungamana na ukweli na anatamani kubakia vivyo hivyo, katika matamshi yake, hata hivyo wadadisi wa mambo ya kisiasa wana wasiwasi kwamba ingawa ni vyema aendelee kuwa mkweli na anayesimamia ukweli haijabainika ni nani atamwambia ukweli kuhusu yeye mwenyewe.

Gachagua mwenye miaka 57, amerithi kiti cha uongozi cha Mlima Kenya na sasa ni mfalme wa Mlima Kenya kwa ghafla na bila kutarajiwa, ni mara ya kwanza eneo hilo kupata mfalme wa kisiasa ambaye uzoefu wake wa kisiasa ni chini ya miaka mitano kama mbunge kwa mara ya kwanza na sasa ni Makamu wa Rais.

Kabla ya Gachagua kushika nafasi hiyo ya ushawishi ilikuwa ikishikiliwa na Dedan Kimathi (zamani kabla ya uhuru wa Kenya), Mzee Jomo Kenyatta kuanzia mwaka 1963 hadi 1978, Njenga Karume mwaka 1978 hadi 1992, alifuata Kenneth Matiba mwaka 1993-1997, kisha Mwai Kibaki alieanza mwaka 1997- 2013 na Uhuru Kenyatta kuanzia 2013 hadi 2022. **MITANDAO**

JUKWAA LA VIONGOZI

ELIZABETH TRUSS, THERESE COFFEY

# Vigogo wakuu wanaoiongoza Uingereza baada ya Johnson

• Mfumuko bei, athari Brexit vigingi vinavyowakabili

**Na Gaudensia Mngumi**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza kutoka Chama cha Conservative Elizabeth 'Liz' Truss, anashika wadhifa huo na ndiye kiongozi mpya wa chama hicho.

Anarithi mikoba ya Boris Johnson, aliyelazimishwa kujitumbua au kung'atuka Julai mwaka huu, kutokana na madai ya misururu ya kufanya tafrija wakati wa tahadhari na vikwazo vya kudhibiti COVID-19.

Truss mwenye miaka 47, amemshinda waziri wa zamani wa fedha mwenye asili ya Afrika Mashariki Rishi Sunak, kwenye uchaguzi wa chama ambao ni wanachama hai 170,000 wa chama cha Conservative waliopiga kura.

Truss alipata kura 81,326 huku Sunak akiibuka na 60,399, inaripoti Idhaa ya Kiswahili ya DW.

Elizabeth au "Liz" Truss, alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Uingereza kazi ambayo mara nyingi ndiyo inayotoa Mawaziri Wakuu. Kwa mfano Anthony Eden, alikuwa na wadhifa huo kisha kuwa Waziri Mkuu mwaka 1955, yuko pia Alec Douglas-Home mwaka 1963.

Mwingine ni James Callaghan mwaka 1976 na John Major mwaka 1990 na kwamba hata Johnson aliyetumbuliwa karibuni alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje kuanzia 2016 hadi 2018.

Hata hivyo, iwe isiwe changamoto nyingi ambazo Johnson alipambana nazo katika miezi ya hivi karibuni zinaweza pia kumsumbua Truss, hivyo naye akae chonjo saa ni mbaya.

Kama Waziri Mkuu mpya analazimika kushughulika na matatizo yanayohusiana na Brexit au Uingereza kujiondoa EU, mzozo unaoendelea wa gharama ya maisha na mgogoro wa bei ya nishati unaoongezeka, japo hakuna uthibitisho kuwa mambo hayo yalikuwa sababu ya moja kwa moja ya kuanguka kwa Johnson na kuinukwa Truss, lakini hilo halikwepeki kuna kazi ngumu miongoni mwa zinazozungumzwa ni jambo la EU, hivyo Liz anapaswa kujipanga, wachambuzi wanaserma..

Truss anachukua nafasi ya Boris Johnson kwenye ofisi ya juu au kuu ya Uingereza ambaye miaka yake mitatu ya misukosuko kama kiongozi wa nchi ilifichua 'gharama au hasara taifa hilo linazopatia kwa uamuzi huo wa kujitoa Umoja wa Ulaya -EU.

Kabla ya Borris Johnson alikuwapo Theresa May, ambaye Baraza la Mawaziri aliloliunda lilikataa kuunga mkono uongozi wake na mipango yake ya kujiondoa EU na kumshinikiza kujiuzulu.

Kama ilivyokuwa kwa Borris, Theresa May alikuwa anakabiliwa na uasi ndani ya baraza lake la mawaziri na ikawa sababu ya kujiuzulu mara moja mwaka 2019.

Kuondoka kwake hakutaepusha Uingereza na uharibifu wa kudumu wa kiuchumi na kidiplomasia unaosababishwa na kujiondoka katika Umoja wa Ulaya. Lakini wazo la Brexit kama nguvu ya kupanga upya jumuiya ya Uingereza imemalizika ila huyo ni Waziri Mkuu wa pili kuondoka ofisini baada ya kujitoa EU.



Waziri Mkuu wa Uingereza Liz Truss na Naibu wake Therese Coffey, kinamama hao kutoka Chama cha Conservative ndiyo viongozi wakuu wa nchi hiyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Therese Coffey.

> Kama ilivyokuwa kwa Borris, Theresa May alikuwa anakabiliwa na uasi ndani ya baraza lake la mawaziri na ikawa sababu ya kujiuzulu mara moja mwaka 2019.

Kibarua kinaelezwa kuwa ni kigumu yeye pamoja na timu yake wanakabiliwa na kibarua kigumu, hasa kuhusu mfumuko wa bei na jinsi ya kukabiliana na kupanda kwa gharama ya maisha kwani bei za nishati zinatarajiwa kupanda hadi asilimia 80 kuanzia mwezi ujao na kisha kupanda tena mnamo i Januari mwakani.

Benki Kuu ya Uingereza imetabiri kuwa nchi hiyo itakabiliwa na mdororo wa kiuchumi baadaye mwaka huu, hivyo Truss pia ametwikwa jukumu la kushughulikia mipango ya biashara ya nchi hiyo baada ya Brexit katika kisiwa cha Ireland ya Kaskazini, na katika moja kati ya mazungumzo yake ya kwanza alikubaliana na Rais wa Marekani Joe Biden kuhusu umuhimu wa kulinda amani Ireland ya Kaskazini, ambayo ni sehemu ya Uingereza.

Licha ya changamoto lukuki zinazomkabili Waziri Mkuu mpya wa Uingereza, anaonyesha matumaini kuwa ana uwezo wa kuzikabili wakati alipoingia kwenye ofisi yake iliyoko katika mtaa wa Downing Street, mjini London. Anasema "Nina imani kwamba kwa pamoja tunaweza kuondokana na dhoruba hii inayotukabili."

Liz anachukua uongozi akirejea historia iliyojengwa nchini humo na Margareth Thatcher aliyekuwa Waziri Mkuu wa kwanza mwanamke barani Ulaya. Waziri mkuu pekee wa Uingereza katika karne ya 20 aliyeshinda mihula mitatu mfululizo na pia Waziri Mkuu wa Uingereza aliyekaa madarakani kwa muda mrefu zaidi tangu 1827.

Hivyo Liz hana shaka maana Uingereza imeanza kuwaamini wanawake na huenda atawaonyesha kuwa kinamama wanaweza na siyo lazima wangojee kuwezeshwa kama misemo inavyosema..

Liz pamoja na makamu wake ambaye ni mwanamama wanaandika historia kwa kuwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu wote wanamama. Atashirikiana na Therese Coffey ambaye ni Waziri wa Afya na Naibu Waziri Mkuu wa Uingereza, anayedaiwa kuwa anapenda sigara.

Therese ambaye awali alikuwa Waziri wa Kazi na Pensheni, anachukua nafasi ya Stephen Barclay kuongoza wizara hiyo ya afya.

Mwanamama huyo amehusika kwa karibu katika kampeni ya uongozi ya Truss na hapo awali aliwahi kuwa Waziri wa Mazingira, Naibu Kiongozi Shughuli za Bunge la House of Commons.Alichaguliwa kuwa mbunge wa Suffolk Coastal, mwaka wa 2010.

**MITANDAO**

# Viongozi wa dini walipowashukia wenzao kujifanya sehemu ya siasa




Wadau wa siasa wakiwa katika mjadala. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

**INATOKA UK. 13**

dini hutakiwi kutishika anapostushwa, lakini wakitishwa kidogo tu wanalegea," anasema Shekhe Katimba na kuongeza kuwa wanatakiwa kuwa na msimamo bila kutishika, na kwamba baadhi wanatishika na kushindwa kusimamia haki, huku akiwataka kutambua kuwa dini haiwezi kutenganishwa na siasa.

"Ukiangalia hata kwenye vyombo vya habari, vimeminywa na kujikuta vikiegemea upande mmoja hasa vya binafsi, ni vyema viwe huru ili viweze kufanya kazi yake inavyotakiwa," anasema na kuwataka wanahabari kukemea na kuonyesha ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili demokrasia.

Shekhe Issa Ponda, anapochukua jukwaa anasema katika miaka 30 ya urejeshwaji wa vyama vya siasa nchini viongozi wa dini wananyimwa ruhusa ya kutoa elimu ya uraia kwa wananchi kama mbinu ya kutaka wasielewe haki ya kushiriki uchaguzi.

"Kutoa elimu ya uraia haturuhusiwi hadi tuombe kibali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Kwa ujumla kuna vikwazo vingine katika maendeleo ya demokrasia nchini, hivyo tushirikiane kuvimaliza,"

**DEBE KWA CHADEMA**

Mwanasiasa mkongwe John Shibuda, ambaye amewahi kuwa mbunge wa Maswa kupitia CCM na CHADEMA, anapigilia msumari kwa kuwataka viongozi wa dini kukemea dhuluma katika demokrasia, kwa ajili ya ustawi wa vyama vya siasa, kwa kuwa wana nafasi kubwa kwa ustawi wa demokrasia.

"Viongozi wa dini muelewe kwamba, hamtakwenda katika Ufalme wa Mungu iwapo mtakaa kimya bila kukemea dhuluma na ukatili unaodhuru demokrasia kama mnavyokemea mapepo," anasema Shibuda

Shibuda anadai katika uwanja wa siasa Tanzania, ushahidi wake unaonyesha kuwa leo hii ukishindanisha ni chama gani kina ushawishi, chukua CCM, CHADEMA, CUF, ACT-Wazalendo na TLP, chama cha kwanza kwa nguvu za ushawishi, mnyonge mnyongeni, ni CHADEMA.



Kiongozi wa Jumuiya na Taasisi za Kiislam Shekhe Rajab Kàtimba akichangia mada katika mjadala huo.

Anasema pamoja na vikwazo ambavyo kimekuwa kikipitia katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, bado kimeendelea kuwa na nguvu kubwa ya ushawishi na kukubalika kwa wananchi wakiwamo wasio na vyama.

Aidha, anawataka viongozi wapinzani kutoigetemea Ofisi ya Vyama vya Siasa, kwa madai kwamba haiwezi kukubali kupunguza nguvu za CCM. ili upinzani shinde badala yake itahaakikisha inaendelea kuwa madarakani

"Huwa ninashangaa mnapomuita kwa jina la mlezi wa vyama vya siasa, huyo ndiye anayekondesha demokrasia, msitegemee kuwa atakubali kuona upinzani unapata nguvu huku akiwa ameajiriwa na serikali ya CCM," anasema.

Mhadhiri Mwandimizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Richard Mbunda, anasema ndani ya miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi kumekuwapo na udhaifu mwingi ndani ya vyama.

"Unakuta baadhi ya vyama vinakuwa vya kusubiri wakati uchaguzi ndipo vinaibuka, taasisi za aina hii si za umma bali zinakuwa na malengo ya maslahi binafsi, hivyo ni vyema wenye vyama vya aina wabadilike,"anasema Dk. Mbunda.

Mhadhiri huyu anasema, upungufu wa demokrasia ndani ya vyama, akidai kuwa viongozi wanashika nafasi kwa miaka mingi, na kwamba ni muhimu vijisafishe kwanza kabla kudai demokrasia nje.

"Lakini ukiangalia pia Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), ninatamani chombo hiki kijiendeshe chenyewe kikiwa na nguvu ya kisheria ili kinapotoa maamuzi, basi yaweze kuzingatiwa na kutekelezwa," anasema.


## CHEMSHABONGO NA -00 2 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
2. teketea kwa moto
7. majabali ya majini au nchi kavu
8. kuwa bahili
9. ndugu mkubwa wa kike
11.kuwaza
16.Itikadi
17.amini jambo
18.Watanganyika na Wazanzibar kwa pamoja

Chini:
1. muungano wa nchi nyingi
2. masafa
3. dhamira
4. Muasisi wa taifa la India
5. pata majeraha
6. daima, milele
10.tamko la kuulizia wakati
12.ng'ata
13.hangaiko la moyo
14.ubamba
15.mji wake mkuu ni Kampala





Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| SAMADI | OKA |
| SADAKA | BAO |
| AMANA | RAI |
| MNARA | ODA |
| KINAI | NAI |
| AALIMU | AMA |
| FATAKI | SASA |
| MASIKA | AILI |
| MADINI | ISAKA |
| ANASA | NAIRA |
| DAKAR | ILANI |
| AKAR | RUDIA |
| URENO | MBAO |

A MA

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | W | A | K | A | | M | M | E | A |
| P | A | S | A | K | A | | A | | |
| A | M | A | N | I | | A | Z | M | A |
| K | A | L | I | L | I | | I | | D |
| A | S | I | S | I | | M | N | A | A |
| | A | | A | | | A | G | U | A |
| K | I | A | N | G | A | Z | I | | |
| A | | G | I | A | | I | R | A | N |
| M | | U | | R | | W | A | L | I |
| A | L | A | M | I | N | A | | A | A |



| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | K | | M | J | A |
| O | B | A | M | A | | N |
| R | | L | | L | | Z |
| O | P | E | R | E | T | A |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | A | M | A | K | O | | U | M | A | |
| A | G | A | N | O | L | A | K | A | L | E |
| H | A | T | I | | E | D | A | | O | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | | A | | B | | H |
| S | U | N | G | U | R | A |
| H | | D | | N | | N |
| A | R | A | B | I | K | A |



maoni: 0755429240





# Polisi yaombwa kuingilia mgogoro wa ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limeombwa kuingilia mgogoro unaozihusisha familia mbili ambazo zinagombea eneo la ardhi lenye ukubwa wa ekari tatu.

Mgogoro huo umeendelea baada ya familia moja kushindwa kesi katika Mahakama ya Ardhi na Nyumba wilayani Rungwe, lakini imeendelea kuishi kwenye eneo hilo licha ya hukumu kutolewa.

Katika hukumu iliyotolewa Agosti 26, mwaka huu na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba wilayani Rungwe, Bon Cyril, ilimpa ushindi Anyisile Mwamwimbe mkazi wa Kijiji cha Busisya dhidi ya Amidu Mwambona.

Baada ya hukumu hiyo familia hizo zimeingia tena kwenye mgogoro mwingine wa kuwindana baada ya hukumu ya mahakama kutolewa, kwamba Anyisile Mwamwimbe anadai kumiliki eneo hilo na kujenga nyumba kwa zaidi ya miaka 20 baada ya kulinunua kutoka kwa familia ya Mwambona ambaye kwa sasa ni marehemu.

Mwamwimbe alieleza kuwa alishangaa kuvamiwa na watoto wa marehemu Mwambona waliofika nyumbani na kubomoa nyumba yake huku mkewe Winifa Nkemwa akiamua kurejea kwa wazazi wake.

"Agosti 26, mwaka huu, kesi iliisha na mimi kushinda lakini nashangaa siku hiyo hiyo wakafika kwenye shamba langu na kuanza kukata migomba na baadaye kuvunja nyumba iliyokuwapo eneo hilo," alisema Mwamwimbe.

Winifa Nkemwa ambaye ni mke wa Mwamwimbe alisema baada ya kuona familia iliyoshindwa kesi inaendelea na vurugu za kukata migomba na mazao mengine shambani pamoja na jiko alikimbia na kuamua kurudi nyumbani.

Francis Mwambona alisema kwa kipindi kirefu familia ya Mwambona imekuwa ikiishi hapo na kufanya usafi wa mazingira kama vile kuhudumia migomba na kufyeka nyasi.

Balozi wa eneo hilo, Adam Mwampaka alisema kwa miaka aliyoishi eneo hilo anaamini eneo linalogombaniwa ni mali ya Anyisile Mwamwimbe.

"Huu ni mwaka wa 22 tangu nianze kuishi kwenye eneo hili Mwamwimbe nilikuta anamiliki mji huu na siyo Mwambona hivyo nashangaa kwa nini anagombea mahali hapa," alisema Mwampaka.

Akizungumzia suala hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga alisema amezitaka familia hizo kudumisha amani na utulivu na kwamba eneo la familia moja haijaridhika na uamuzi wa mahakama ikate rufani na siyo kujichukulia sheria mkononi.

# Vikundi vya wajasiriamali wa batiki kufufuliwa tena

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya unatarajia kufufua vikundi vya wajasiriamali wanaojishughulisha na utengenezaji wa batiki ili kuongeza wigo wa wananchi kujiingizia kipato na kutimiza malengo waliyojiwekea.

Katibu Tawala Msaidizi Viwanda, Biashara na Uwekezaji mkoani Mbeya, Mwajabu Nyamkomora, alitoa kauli hiyo jana baada ya kuzindua mpango wa kuzalisha batiki na kuhakikisha wanawawezesha wajasiriamali hao vifaa vya utengenezaji na kuwatafutia masoko ndani na nje ya nchi.

Alisema sababu ya kufa kwa viwanda vingi vya kutengeneza batiki ni kukosekana kwa soko la uhakika la kuuza bidhaa hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo wameanza upya kwa kuanzia vikundi 15 mkoani humo ambavyo vitakopeshwa vifaa na kutafutiwa soko la kuuzia batiki hizo.

"Tumeanza mchakato wa urağhibishi kwa vikundi vya wanawake wanaojihusisha na utengenezaji wa batiki hapo tunajikita kuwafundisha namna ya utengenezaji kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, tunawapatia vifaa na kuwapa mbinu za namna ya kupata masoko huku nasi serikali tukiendelea na jitihada za kutangaza bidhaa wanazozalisha, tumeamua kufufua viwanda vyote vilivyokufa vianze kufanya kazi tutahakikisha halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya zinakuwa na viwanda vya namna hiyo," alisema Nyamkomora.

Mratibu wa mpango huo, Rose Urio aliwahakikishia wajasiriamali hao kuwa kuna soko la uhakika, hivyo wasiwe na hofu juu ya wapi watauza bidhaa hiyo na kuwasisitiza waendelee kuzalisha kwa wingi kwa kuzingatia ubora unaokidhi mahitaji ya soko la nje. Aliongeza kuwa tayari bidhaa hizo zitaanza kupelekwa kwenye mataifa ya Marekani na Uingereza, kwamba batiki hizo zitasafirishwa kwa msamaha wa kodi kwa sababu ya makubaliano ya kimataifa yaliyofanyika kati ya Tanzania na mataifa ya Ulaya sambamba na nchi za Afrika Mashariki kuhusu masuala ya kibiashara.

Baadhi ya wajasiriamali, Lina Fredy, alisema miongoni mwa vikwazo wanavyokabiliana navyo watengenezaji wa batiki ni ukosefu wa vifaa vya kutengeneza bidhaa hiyo kama vile vitambaa na rangi.

Alisema kikwazo hicho kinasababisha kupunguza ufanisi wa utengenezaji wa bidhaa wanayoitaka hivyo kukopeshwa kwa vifaa kutasaidia kutengeneza vitu vya kupendeza na kuwavutia wateja wao.



Meneja Uchenjuaji wa Madini ya Dhahabu wa Kiwanda cha Apex wilayani Chunya, mkoani Mbeya, Abdulkarim Shauri (mwenye kofia kijani), akifafanua jambo kwa wachimbaji wadogo wa madini waliotembelea kiwanda hicho jana, kwa lengo la kujifunza namna teknolojia mpya ya Boran inavyotumika kuchenjua dhahabu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Sekondari Mbeya yapokea msaada matangi manne

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imekabidhi msaada wa matangi ya maji manne yenye ujazo wa lita 40,000 yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa uongozi wa Shule ya Sekondari ya Mbeya.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa jitihada za kuhakikisha benki hiyo inasaidia kuboresha sekta ya elimu hapa nchini.

Meneja wa Benki ya NBC, Tawi la Mbeya, Asia Mselemu, alikabidhi msaada huo jana kwa uongozi wa Shule ya Sekondari Mbeya.

Makabidhiano yaliyowashirikisha Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, walimu, wanafunzi, wadau wa elimu mkoani humo pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema msaada huo unalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha hali ya elimu mkoani humo na kwamba msaada huo utasaidia kupunguza kero ya muda mrefu ya upatikanaji wa majisafi kwa walimu na wanafunzi shuleni hapo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Francis Mwakihaba, alisema kupitia msaada huo wanafunzi wa shule hiyo takribani 1,464 na watumishi 71 wakiwamo walimu wamehakikishiwa upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa uhakika hali ambayo itaokoa nguvu na muda mwingi uliokuwa ukitumiwa na wanafunzi kutafuta huduma hiyo muhimu na kuathiri muda wao wa masomo.

Asia Mselemu alisema kuwa benki hiyo imejitolea kusaidia katika kuboresha ustawi wa jamii kupitia misaada ya kijamii ikiwamo elimu na kwamba wameguswa sana na suala la kero ya upatikanaji wa majisafi shuleni hapo, sababu iliyosababisha wao kuchukua hatua hiyo ili kuwasaidia wanafunzi na walimu kuepukana na changamoto hiyo.

Akitoa shukrani zake kwa niaba ya wanafunzi wenzake wa shule hiyo, mwanafunzi Dorcas Jerry alisema msaada huo umewanusuru dhidi ya tatizo lililokuwa likiwakabiri.

"Msaada huu pia una faida kiafya hususani kipindi cha hedhi kwa sisi wanafunzi wa kike kwa kuwa huwa tunahitaji usafi wa hali ya juu, hivyo tunahitaji maji ya kutosha. Tunawashukuru sana Benki ya NBC kwa msaada huu na tunaahidi kufanya vizuri zaidi kimasomo," alisema.



## Serikali kuboresha miundombinu ufundishaji shuleni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuboresha miundombinu ya elimu katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuhakikisha Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) yanafikia lengo.

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Dk. Grace Magembe, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati akifungua MEWAKA kwa wawezeshaji wa kitaifa lengo likiwa kuwajengea uwezo wakati watakapokwenda kutekeleza majukumu yao katika ngazi ya mikoa na halmashauri.

Alisema serikali imeendelea kuboresha vituo vya walimu (TRCs) vitakavyotumika kutoa mafunzo endelevu ya walimu kazini pamoja na kununua vifaa vya TEHAMA vitakavyosaidia katika uendeleshaji wa mafunzo hayo.

"Mafunzo haya yamepangwa kutolewa katika ngazi za shule na vituo vya walimu, kwamba walimu wote wanaelekezwa kushiriki kikamilifu," alisisitiza Dk. Magembe.

Mafunzo hayo yamelenga kufikia halmashauari 40, ambazo hazijapatiwa mafunzo.

Aidha, Dk. Magembe alisema halmashauri 19 kati 40 zilizobaki katika mikoa ya Kigoma, Tanga, Simiyu, Mara, Rukwa, Singida na Dodoma zitapatiwa mafunzo kwa walimu wa shule ya msingi kupitia programu ya shule bora.

Aliwataka viongozi wanaosimamia mpango huo ulioanzishwa na serikali kwa kushirikiana na wadau kuusimamia kikamilifu.

Kadhalika, aliwataka kuhakikisha kuwa mafunzo hayo yanakuwa na tija na endelevu kwa walimu.

Pia aliwaagiza walimu wote nchini kushiriki kikamilifu mafunzo hayo katika jumuiya za kujifunza kwa ngazi ya shule na vituo vya walimu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Dk. Aneth Komba, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwawezesha walimu kwa kuwapatia mfunzo.

Dk. Komba alisema mafunzo hayo yatatoa nafasi ya walimu kuweza kupata mbinu tofauti za kufundisha na kuwaelekeza jinsi ya kuweza kusoma kwa maktaba mtandao.

Mwenyekiti wa Mafunzo Endelevu ya Walimu, Modesta Ng'aida alisema, mafunzo hayo watakayopata yatakuwa ni mwongozo wa kuwawezesha kwenda kuwa mabalozi wazuri katika maeneo watakao elekezwa kwenda kuyatekeleza.

Alisema: "Tunaihakikishia serikali yetu hamjakosea sisi tunaowakilisha wenzetu tutahahakikisha tunaifikisha elimu tuliyoipata kwa manufaa ya watoto wetu ambao ndio wanafunzi wetu".

# Wazazi watakiwa kuwaruhusu watoto kushiriki katika mabaraza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wazazi na walimu kuwaruhusu watoto kushiriki shughuli za mabaraza yao ili kuimarisha uwezo wao kwenye malezi na makuzi.

Aidha, ameagiza Idara ya Watoto kupitia wizara hiyo kuandaa kikao cha Baraza la Watoto wa Tanzania ili mtoto Victor Ntatau aliyeshiriki mkutano wa dunia wa watoto nchini Denmark awasilishe maazimio ya mkutano huo.

Dk.Gwajima aliyasema hayo jana alipokuwa akipokea bendera ya taifa kutoka kwa mtoto Victor baada ya kushiriki mkutano huo uliofanyika Septemba 13-16, mwaka huu.

Alisema mabaraza ya watoto yametoa mchango mkubwa katika kuendeleza watoto kupitia nyanja mbalimbali ikiwamo kuwajengea uwezo wa kujieleza, kujiamini na kuimarisha mahusiano miongoni mwao.

"Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wazazi wa mtoto Victor kwa kumruhusu kushiriki mabaraza haya na kipindi chote cha usaili mtandaoni ambao naambiwa umechukua takribani miezi sita hatimaye kuibuka mshindi wa nchi yetu na kati ya watoto saba waliochaguliwa katika Baraza la Afrika amejumuika na wenzake 80 nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN),"alisema.

Aliagiza watendaji wake kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuhakikisha vipaji vya watoto kama Victor vinatambuliwa na kuendelezwa ili kufikia malengo ya makuzi na utimilifu wa maisha yao ya utoto. Naye Mtoto Victor alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha mazingira bora ya elimu yanayowapa nafasi ya kujifunza na kuibua vipaji na fursa sawa kwa wenye ulemavu na watoto wa Tanzania.

"Nimejifunza mambo mengi kwa faida ya watoto na nchi hii. Jumla ya watoto 60 tuliokusanya mawazo na kutoka na tamko ambalo naamini Rais wangu Samia Suluhu Hassan amelisikia," alisema.

Alisema watoto wametoa tamko pia kuomba jamii kuangalia athari ya mabadiliko ya tabia nchi katika ukuaji wa watoto, kwa sababu watoto ni mtaji wa kizazi kijacho.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akipokea bendera kwa Victor Tantao, jijini Dodoma jana, aliyewakilisha watoto wa Tanzania kwenye Baraza la Watoto Duniani lililofanyika nchini Denmark. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watu wenye ulemavu wataka mwakilishi EALA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI uchaguzi wa wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, ukitarajiwa kufanyika kesho, watu wenye ulemavu wamewaomba wabunge kumpigia kura Seif Kondo, ambaye ni mtu mwenye ualbino ili kuliwakilisha kundi hilo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kampeni za uchaguzi wa ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki zilianza jana na zikitarajiwa kuhitimishwa leo kwa kila mgombea kunadai sera zake kwa wabunge wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kabla ya kufanyika kwa uchaguzi huo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Kamati ya kampeni ya mgombea Seif Kondo, Alex Mhando alisema ni wakati muafaka kwa Bunge hilo kuwa na mwakilishi wa watu wenye ulemavu.

Mhando, ambaye ni mjumbe wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, alisema Kondo, ameingia katika kinyang'anyiro hicho kupitia Chama cha Wananchi CUF, atachuana na wagombea wa vyama vingine ikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo.

Mhando, alisema kutokana na uzoevu wa mgombea huyo katika masuala ya watu wenye ulemavu atakuwa mtu sahihi kuwawakilisha kwenye jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Amefanya kazi katika mashirika yanayojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu kama vile Under the Same Sun, lakini ameshiriki kwenye kuandaa mwongozo wa masuala ya elimu kwa watu wenye ulemavu nchini lakini pia amefanya kazi kwa muda mrefu ndani ya SHIVYAWATA.

"Toka Bunge hili la Afrika Mashariki lianzishwe hatujawahi kuwa na mwakilishi mwenye ulemavu hivyo sasa ni wakati mwafaka kwetu walemavu kuwa na mtu huyu ili atusadie katika kutuunganisha na fursa mbalimbali zinazopatikana katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki,"alisema Mhando.

Uchaguzi huo ambao unatarajiwa kufanyika kesho wagombea tisa tuu ndiyo watakaochaguliwa kuiwakilisha nchi katika Bunge hilo la Afrika Mashariki huku CCM kikitoa wabunge nane na vyama vya upinzani mbunge mmoja.





# Dk. Mwinyi: Zanzibar, Australia zitaendeleza ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar itaendeleza uhusiano na ushirikano uliopo kati yake na Australia kwa maslahi ya nchi mbili hizo.

Aliyasema hayo Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na Balozi wa Australia nchini Tanzania, Luke Williams ambaye alifika kwa ajili ya kujitambulisha.

Alisema kuna umuhimu kwa nchi mbili hizo kuendeleza ushirikiano uliopo kati huu Zanzibar ikiweka kipaumbele katika kuimarisha uchumi wake kupitia Sekta za Uchumi wa Buluu, unaohusisha sekta za utalii, kilimo cha mwani na uvuvi.

Dk. Mwinyi alitumia fursa kuiomba Australia kusaidia uimarishaji wa sekta hizo na kumpongeza balozi huyo kwa dhamira yake ya kusaidia Zanzibar katika sekta ya kilimo.

Balozi wa Australia nchini Tanzania, Luke Williams aliahidi kuendeleza ushirikano uliopo kati ya Australia na Tanzania pamoja na kuunga mkono azma ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya uchumi wa buluu kwa kuzingatia uwapo wa fursa mbalimbali.

Alisema Zanzibar ni kituo muhimu cha utalii kutokana na historia yake, kuwa na mandhari ya kuvutia pamoja na utamaduni wa watu wake.

Alimhakikisha Rais Dk. Mwinyi kuwa atafanya juhudi kusaidia uendelezaji wa kilimo kwa kuzingatia Zanzibar ina utajiri katika uzalishaji wa viungo.

**Dk. Mwinyi alitumia fursa kuiomba Australia kusaidia uimarishaji wa sekta hizo na kumpongeza balozi huyo kwa dhamira yake ya kusaidia Zanzibar katika sekta ya kilimo.**

# ZAECA yawaburuza mahakamani watuhumiwa kesi ya rushwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) imefikisha kesi mbalimbali Mahakama Kuu Zanzibar zinazohusu makosa ya rushwa na uhujumu wa uchumi zikiwahusisha watuhumiwa 15.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Mnazimmoja Mjini Zanzibar, Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Ali Abdallah Ali, alisema kesi hizo zimewahusisha watuhumiwa 15 wakiwamo wahasibu wakuu wa taasisi za serikali.

Mkurugenzi huyo alizitaja kesi zilizofikishwa mahakamani pamoja na majina ya watuhumiwa wanaohusika na tuhuma hizo. Alisema kesi namba 84/2022 inayowahusu watumishi wawili wa ofisi ya mtakwimu mkuu wa serikali.

Aliwataja watumishi hao ni Issa Ramadhan Senga (56) ambaye ni Ofisa Manunuzi na Fadhil Ali Hassan (48) ambaye ni Ofisa Takwimu wote kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Alisema washtakiwa hao wamekabiliwa na kosa la ubadhirifu wa mali na mapato kinyume na kifungu 42(1), (a) 60(1)(2) (a) na 61 vya Sheria ya ZAECA nambari 1/2012.

Alisema washtakiwa hao wanatuhumiwa kujipatia Sh. milioni 51, zilizopangwa kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri katika mradi wa afya ya mama na mtoto.

"Washtakiwa wote hao wamekana kuhusika kufanya kosa hilo na kesi hiyo imepangwa kuendelea tena Oktoba 3, mwaka huu kwa hatua ya maamuzi ya maombi ya dhamana ya washtakiwa," alisema.

Alitaja kesi zingine ni namba 86/2022 inayowahusu wahasibu wawili kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na wamiliki wawili wa kampuni binafsi.

Aliwataja washtakiwa hao ni Mouhammed Mussa Ussi (53) ambaye ni Mhasibu Mkuu, Issa Barakat Abdallah (42) Msaidizi Mhasibu wa wizara hiyo ya ujenzi, Said Shaaban Mintanga (38) Mkurugenzi wa Kampuni ya Skifaru Investment and Engineering ltd na Suleiman Hamad Rashid (63) mmiliki wa Kampuni ya SH Traders and Fumigation.

Alisema washtakiwa hao wameshtakiwa kwa kosa la ubadhirifu wa Sh. bilioni 1.3 kwa kutengeneza miradi hewa ya maendeleo ya serikali na kujipatia fedha hizo kinyume na utaratibu.

Alisema washtakiwa hao wamekana kuhusika kufanya makosa hayo na kesi kuahirishwa hadi Oktoba 5, mwaka huu kwa hatua ya maamuzi ya maombi ya dhamana ya washtakiwa.

Alisema kesi namba 83/2022 ya kughushi fedha za kigeni ambayo inawahusisha washtakiwa, Khatib Ameir Haji (42) Mkaazi wa Mtopepeo Mjini Unguja, Feruz Omar Khamis(52) Mkaazi wa Machui, Abubak Khamis Bakari (25) Mkaazi wa Fuoni Chunga na Ali Omar Ahmed (25) Mkaazi wa Mombasa Zanzibar.

Alisema washtakiwa hao wameshtakiwa kwa kosa la kughushi Dola za Marekani 800 na Euro 100 kinyume na kifungu cha 51 na 61 cha Sheria ya ZAECA namba 1/2012 na washtakiwa wamekana kufanya kosa hilo.

Pia alitaja kesi namba 85/2022 inayowahusu watumishi watano wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ambao ni Kassim Idrisa Mussa (39) Meneja wa Kitengo cha Mapato, Abdulatif Abdallah Waziri(26) Ofisa TEHAMA, Aisha Yussuf Said(33) Ofisa Kitengo cha TEHAMA, Fatma Kombo Mohd (35) Ofisa Kitengo cha TEHAMA na Asia Abdisalam Hussein (44) Mkuu wa Kitengo cha Mapato.

Alisema mshtakiwa Idrisa Mussa, Abdulatif Abdallah Waziri, Aisha Yussuf Said na Fatma Kombo Mohd wameshtakiwa kwa makosa ya kutumia vibaya mali kinyume na kifungu cha 43, matumizi mabaya ya ofisi kinyume na kifungu 53 vya sheria ya ZAECA.

"Washtakiwa hao wameshtakiwa kwa kujipatia Sh. milioni 278.4 na Dola za Marekani 103,817.72 baada ya kuuchezea mfumo wa ukusanyaji wa kodi na kutoa risiti ambazo fedha zake hazikuingia katika nambari za hesabu za bodi ya mapato," alisema Mkurugenzi Ali.

Alisema mshtakiwa, Asia Abdisalam Hussein, ameshtakiwa kwa kosa la matumizi mabaya ya ofisi kinyume na kifungu cha 53 cha Sheria ya ZAECA.

Alisema washtakiwa hao wamekana kuhusika kufanya makosa hayo na kesi hiyo imepangwa kuendelea tena Oktoba 5, mwaka huu.

Mkurugenzi wa ZAECA aliwataka na watumishi wote wa serikali kuendelea kutoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi kwa kutoa taarifa kupitia nambari ya simu 113 ambayo ni bure ili kutokomeza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi wa nchi.



Waziri wa Habari, Vijana, Sanaa na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mradi WB kukarabati vituo vya afya vijijini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidhi, amesema kupitia mradi wa Benki ya Dunia (WB) wanakusudia kuvifanyia ukarabati vituo mbalimbali vya afya hususani vilivyoko vijijini hatua ambazo zitasaidia kuimarisha huduma za afya ikiwamo za kinamama wajawazito.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa Nungwi, Abdalla Abasi Wadi aliyetaka kujua lini kituo cha Nungwi kitajengwa na kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Hafidh alisema mradi wa WB awamu ya kwanza umevifanyia ukarabati jumla ya vituo vya afya 10 ikiwamo vitano viliopo Unguja ambavyo awali vilikuwa katika hali mbaya.

Aidha, alisema awamu ya pili ya mradi huo utaimarisha zaidi vituo vya afya ya kinamama wajawazito na kuona wanapunguza masafa ya kupata huduma za afya ikiwa ni mikakati ya kuhakikisha uzazi salama.

Alisema lengo la Wizara ya Afya ni kuona vifo vya kinamama na watoto vinapunguzwa kwa kiwango kikubwa ambapo sehemu ya mikakati hiyo ni kujenga vituo zaidi vya afya.

"Mheshimiwa Spika awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa vituo vya afya unaotekelezwa na Benki ya Dunia ni kujenga vituo zaidi vitakavyotoa huduma za kinamama wajawazito na kuona vifo vinavyotokana na uzazi vinapungua," alisema.

Alisema kufuatia ujenzi wa hospitali 11 za Wilaya ya Unguja na Pemba zinazotokana na fedha za UVIKO -19, matumaini ni kuona huduma za afya kwa kinamama wajawazito zitaimarika kwa kiwango kikubwa kwa sababu hospitali hizo zote huduma za afya kwa kinamama wajawazito zinapatikana.

Alisema: "Tunajenga hospitali 11 za Wilaya ya Unguja na Pemba ambazo zote zitakuwa na huduma za kinamama wajawazito kujifungua, kwamba tunaamini tutapunguza vifo vinavyotokana na kinamama wajawazito ikiwezekana kuvitokomeza moja kwa moja".

## DC ataka usahihi vipimo vya maabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewataka wamiliki wa maabara zinazopima magonjwa tofauti kuhakikisha zinakuwa na vipimo sahihi ili kumsaidia mgonjwa kupata tiba ya uhakika.

Amesema baadhi ya maabara hazina vipimo bora, na kwamba mtu anakwenda kupima ugonjwa kwenye kituo cha afya anaambiwa hana ugonjwa wowote, lakini akiende kwenye kituo kingine anabainika na maradhi.

Alitoa maagizo hayo juzi mjini Shinyanga wakati akifungua mafunzo ya ufahamu juu ya elimu ya sayansi na vipimo kwa wataalamu wa maabara yaliyolenga kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya vipimo.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la Viwango Nchini (TBS), kwamba baada ya mafunzo hayo wataalamu hao watatakiwa kufanya kazi kwa weledi na kutoa majibu yanayofanana.

Alisema: "Baada ya mafunzo haya tunaamini vipimo katika maabara vitakuwa sahihi na siyo kutofautiana, mfano unakuta mtu amepima kwenye kituo fulani cha afya majibu yanakuwa tofauti na kituo kingine, unaweza kukuta unaumwa, lakini vipimo vinaonesha huna ugonjwa ukienda kupima kwingine unaibainika unaumwa." Aliongeza: "Msiumbe takwimu, msiunde matokeo ya vipimo mtaumiza wananchi, TBS watapita kwenye maeneo yenu ya kazi kukagua vipimo mnavyotumia, tunataka vipimo sahihi ili hata ukienda kwenye kituo kingine cha afya ukute majibu yanafanana".

Katika hatua nyingine aliwataka TBS kuendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa zilizomaliza muda wake kwenye maduka mbalimbali yakiwamo ya dawa za binadamu ili kutosababisha madhara kwa watumiaji.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Johanes Maganga, alisema wametoa mafunzo hayo ya sayansi ya vipimo kwa ajili ya kusaidia taifa kuwa na vipimo sahihi.

# Watorosha dhahabu, wakwepa kodi kunyang'anywa leseni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha Madalali wa Madini Tanzania (CHAMMATA), kimetangaza kuwanyang'anya leseni na kuwazuia kununua dhahabu wanachama wake watakaokamatwa wakitorosha madini kwa njia za panya, wanaokwepa kulipa kodi.

Mwenyekiti wa CHAMMATA, Jeremia Kituyo, aliyabainisha hayo jana wakati wa uzinduzi wa kadi za chama hicho na kuwasihi kutokuwa sehemu ya madalali wanaokwepa kodi kwa kutorosha madini.

Aliongeza kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikiwachafua na kuonekana siyo waaminifu kwa serikali na vimesababisha tume ya madini kuweka leseni kila mkoa kwa lengo la kudhibiti utoroshaji huo.

Kituyo alisema viongozi wa CHAMMATA watakaozembea katika maeneo yao na kusababisha wanachama kutorosha madini watawajibishwa kwa kuwa hawataki kuona kila siku wakichafuliwa jina kutokana na watu wachache wasiokuwa waadilifu.

Kituyo alisema mikoa ya Arusha na Manyara wachimbaji wake wadogo wa madini wa tanzanite walikuwa wanaongoza kwa utoroshaji wa madini hayo, lakini walisimama imara kwa kushirikiana na viongozi na kufanikiwa kutokomeza tabia hiyo na kwamba wanataka kuona Kahama wanamaliza tatizo hilo.

Kaimu Ofisa Madini Mkoa wa Kimadini Kahama, Jeremillah Hango, alisema kuna tatizo kubwa la utoroshaji wa madini kwa madalali ambao siyo waadilifu na wanasababisha serikali kuendelea kukosa mapato.

Alisema wafanyabiashara wakubwa wanawatumia madalali wa madini kupitisha madini na wanapokamatwa wanawakana jambo ambalo husababisha serikali kutaifisha mitaji yao.

Mmoja wa madalali kutoka Soko la Madini Kakola, Baraka Lazaro, aliiomba serikali kuwaruhusu kuuza madini nje ya mikoa wanayotoka ili kupata bei nzuri.

Alisema kuna wakati wafanyabiashara wa eneo hilo wanakosa fedha za kununua madini na kusababisha washindwe kuuza madini waliyonayo.



Wavuvi wa mwalo wa Barabara ya Ukerewe, jijini Mwanza, wakiwa kwenye mtumbwi wakijiandaa kuelekea kutega nyavu katika Ziwa Victoria jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wavuvi wa dagaa waacha matumizi ya karabai

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAVUVI wa samaki aina ya dagaa Ziwa Victoria mkoani Mwanza wameachana na matumizi ya karabai zinazotumia mafuta ya taa kufanyia kazi zao.

Hivyo, wameanza kutumia umeme wa nishati ya jua (sola), kwa lengo la kuimarisha usalama wao na zana wanazotumia.

Kwa zaidi ya miaka miwili sasa wavuvi hao katika Ziwa Victoria wameacha kutumia karabai ili kulinda mazingira na ikolojia ya ziwa.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wavuvi wa dagaa kutoka katika mialo ya Mswahili na Sweya mkoani Mwanza walieleza kuwa matumizi ya taa za sola yamekuwa na faida kwao na kwenye utunzaji wa mazingira katika shughuli za uvuvi.

"Kipindi tunatumia karabai tulikuwa tukihatarisha maisha yetu na mitaji yetu kwani kuna kipindi mafuta ya taa yalikuwa yakimwagika tukiwa ziwani na kusababisha moto na muda mwingine kumwagika ziwani na kuua mazalia ya samaki," alieleza Hamisi Magesa mmoja wa wavuvi.

Alisema wakati wanatumia karabai ilitokea dagaa zote zikamwagikiwa mafuta ya taa na kuwasababisha hasara kwa wavuvi hao.

Mmoja wa wavuvi hao, Amosi Mwijage aliieleza Nipashe kuwa taa za sola ni tofauti na zile za karabai kutokana na kuwa na mwanga unaohitajika katika uvuvi na kuwaka kwa kipindi kirefu ziwani ikilinganishwa na karabai.

Alieleza kuwa karabai zilikuwa zinatoa mwanga mkali, moshi pamoja na harufu kali ya mafuta ya taa na kwamba wakati mwingine waliishiwa mafuta ya taa wakiwa ziwani.

Aliongeza kuwa taa hizo zinawaka kwa saa 12 kabla ya kuzimika na kwamba hazina usumbufu wakati wa kuzitumia ziwani.

"Kipindi tunatumia karabai tulilazimika kununua mafuta ya taa ambayo kwa sasa yamepanda bei, lakini ukitumia taa za sola huhitaji kununua chochote, labda kuanika tu juani wakati wa mchana, " alieleza Zakaria Mashimba ambaye ni mvuvi kutoka katika mwalo wa Sweya.

Mwenyekiti wa wavuvi katika mwalo wa Mswahili, Robert Mussa alieleza kuwa licha ya faida kubwa zitokanazo na taa hizo za sola ilikuwa ni kazi ngumu mtazamo wa wavuvi kutoka katika matumizi ya karabai.

"Kwa sasa takribani wavuvi wote wanatumia nishati hii katika uvuvi wao, lakini ilikuwa ni kazi kubwa mpaka kuwahamisha na kukubali kutumia sola na hii ni kutokana na bei yake kuwa juu zaidi ya bei za karabai," alisema.

Kwa mujibu wa wavuvi hao taa za sola zililetwa na serikali ya Ujerumani kwa ajili ya majaribio mwaka 2015, kama njia ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira.

HABARI KIMATAIFA

# UN yatahadharisha elimu kuigawa dunia

**UN,** New York

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres ametahadharisha kuwa elimu inageuka kuwa nyenzo inayoigawa dunia kwa kasi, wakati akijaribu kuyaweka maendeleo katika ajenda ya mkutano wa hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, Antonio aliyabainisha hayo akiwa katika kikao maalumu cha kilele kuhusu elimu kabla viongozi wa dunia kukutana kwa mkutano wa hadhara kuu ya UN.

Alisema kila mtu anafahamu elimu huyabadili maisha, uchumi na jamii mbalimbali lakini wanafahamu pia kwamba lazima waifanyie mageuzi kwa sababu iko katika mgogoro mkubwa, huku akibainisha kuwa asilimia 70 ya wanafunzi wenye umri wa miaka kumi katika nchi masikini hawawezi kusoma, ama hawaendi shule au wako shule lakini hawasomi vizuri.

"Elimu inageuka kwa kasi kuwa nyenzo kubwa inayosababisha mgawanyiko, mifumo ya elimu haizingatii sana kwamba elimu haina mwisho na walimu hawajapokea mafunzo wakahitimu vizuri, hawathaminiwi na wanalipwa mishahara midogo, pengo la ufadhili wa elimu linaendelea kutanuka kuliko ilivyowahi kushuhudiwa," alibainisha Guterres.

**Msitoe ahadi ndogo za choyo na za muda mfupi, jitoleeni kuilinda haki ya kupata elimu kamili na kuondosha kabisa pengo la ufadhili, tumieni mamlaka mliyonayo kuchukua hatua, tengeni asilimia 20 ya bajeti zenu kwa elimu.**

Aliongeza kwa kuutahadharisha mkutano huo kwamba janga la ugonjwa wa Covid-19 lilisababisha athari kubwa kwa elimu, huku wanafunzi maskini wakikosa teknolojia na mizozo ikitatiza masomo shuleni, akizitolea wito nchi zote zitoe kipaumbele kuongeza matumizi ya fedha kwa kila mwanafunzi huku kukiwa na maswali mengi kuhusu uchumi wa dunia.

### KUIMARISHWA ELIMU WASICHANA

Katika ripoti iliyochapishwa mwanzoni mwa mwezi huu na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) lilisema ugonjwa wa Covid-19 ulirudisha nyuma maendeleo ya binadamu kwa miaka mitano.

Guterres pia aliutaka utawala wa Taliban nchini Afghanistan ufute vikwazo vyote kuhusu elimu kwa wasichana na iwaruhusu waendelee na masomo katika shule za sekondari.

Akizungumza katika mkutano huo mshindi wa tuzo ya amani ya Nobel mwaka 2014 ambaye pia ni balozi wa amani wa Umoja wa Mataifa, Malala Yousafzai, alizitaka nchi zenye kipato cha juu ziongeze misaada, zifute madeni na ziweke mifumo ya haki ya kimataifa ya kodi ili nchi zenye kipato cha chini ziweze kutumia fedha zaidi kwa ajili ya wasichana.

"Msitoe ahadi ndogo za choyo na za muda mfupi, jitoleeni kuilinda haki ya kupata elimu kamili na kuondosha kabisa pengo la ufadhili, tumieni mamlaka mliyonayo kuchukua hatua, tengeni asilimia 20 ya bajeti zenu kwa elimu," alishauri Yousafzai.

Mkutano wa hadhara kuu ya UN unafanyika baada ya miaka miwili ya janga la Corona, huku viongozi wakitakiwa kuhudhuria vikao mjini New York ikiwa wanataka kuhutubia, isipokuwa Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky.

Pia ilielezwa kuwa hadhara kuu ya UN, ilipiga kura kumruhusu rais Zelensky, ambaye anaongoza upinzani dhidi ya uvamizi wa Urusi, ahutubie bila kufika NewYork.

Katika mkutano huo, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, alisema mataifa yanapaswa kujitoa upya na kuongeza uwekezaji zaidi katika sekta ya elimu ili kuhakikisha watoto wanapata elimu bora na ya uhakika katika kuelekea mwaka 2030.

Alisema elimu ni sehemu muhimu ya ajenda ya maendeleo yam waka 2030 hivyo hakuna budi kuchukua hatua katika kuleta mabadiliko kwenye sekta hiyo na kuongeza kuwa kupatikana kwa elimu bora kutapunguza matabaka katika ajira pamoja na kipato baina ya wananchi.

"Tanzania imechukua hatua mbalimbali katika kuboresha sekta ya elimu ikiwamo kuanza mchakato wa kuboresha mitaala kwa kuwashirikisha wadau wa elimu, kuwekeza katika vyuo vya ufundi stadi na mafunzo, kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari na kuongeza bajeti ya wizara husika kufikia asilimia 18 ya bajeti yote ya serikali," alisema Dk. Mpango. **DW**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres akihutubia katika kikao maalumu cha kilele kilichokuwa kikizungumzia mustakabali wa elimu duniani. **PICHA: MTANDAO**

## Moto waongezeka msitu wa Amazon

**BRASILIA,** Brazil

TAKWIMU rasmi zilizotolewa na idara ya anga za juu za Brazil (INPE), zimeonyesha kwamba idadi ya mioto ya mwituni mwaka huu imepita ile ya mwaka jana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na INPE, hali hiyo inaonekana kuwa tishio kubwa kwenye msitu wa Amazon ambao ni wenye mvua nyingi zaidi ulimwenguni.

Picha za satellite kuanzia Januari mosi hadi mwezi huu zilionyesha jumla ya mioto 75,592 ikiwa idadi kubwa kulinganishwa na 75,090 mwaka uliopita.

Inaelezwa kuwa ripoti hiyo huenda ikamuathiri Rais Jair Bolsonaro ambaye anawania tena uongozi kwenye uchaguzi wa mwezi ujao, huku akikabiliwa na shutuma za kimataifa, kutokana na uharibifu wa msitu wa Amazon.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa wataalam wanalaumu Bolsonaro kwa kulegeza kanuni zilizokuwa zikilinda msitu huo kutokana na wakataji haramu wa miti, pamoja na wafugaji tangu alipochukua madaraka mwaka 2019.

Aidha, inaelezwa kuwa hadi sasa hakuna tamko lolote kutoka kwa ofisi ya Bolsonaro wala wizara ya mazingira ya Brazil, Msemaji wa shirika la kimazingira la Greenpeace nchini humo Andre Freitas ametaja takwimu zilizotolewa kuwa janga lisilo na kifani. **VOA**

## Uganda yathibitisha mlipuko mpya Ebola

**KAMPALA,** Uganda

WIZARA ya Afya ya Uganda imesema mtu mmoja mwenye miaka 24 aliyeambukizwa virusi vya Ebola amefariki dunia katikati mwa nchi hiyo baada ya mlipuko mpya wa ugonjwa huo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Waziri wa Afya wa Uganda Margaret Muhanga, alieleza kwamba mwathiriwa alikuwa alionyesha dalili kabla ya kuugua ugonjwa huo.

Alisema timu ya kliniki ilitoa sampuli za majaribio kwenye (UVRI) na kwamba matokeo yalithibitisha kuwa mgonjwa alikuwa na ugonjwa wa Ebola, ambaye ni mkazi wa kijiji cha Ngabano, wilaya ya Mubende iliyopo umbali wa kilomita 147 kutoka mji mkuu wa Kampala.

"Uganda ina uzoefu mkubwa katika kushughulikia milipuko na magonjwa ya milipuko ya aina hii, wizara imetuma timu katika Wilaya ya Mubende ili kuimarisha ufuatiliaji na ufahamu wa jamii, umma unahimizwa kuwa waangalifu na watulivu wakati timu zikichukua hatua zinazohitajika," alisema.

Aliongeza kuwa wizara ya afya na washirika wengine wametuma timu ya majibu ya haraka katika Wilaya ya Mubende ili kusaidia timu katika ufuatiliaji wa anwani na udhibiti wa visa.

Aidha, Shirika la Afya Duniani (WHO) katika taarifa yake lilisema kisa cha aina hiyo ambacho ni nadra kilithibitishwa na Taasisi ya Utafiti wa Virusi vya Uganda.

Mkurugenzi wa WHO kanda ya Afrika Dk. Matshidiso Moeti, alisema hatua imechukuliwa ili kubaini virusi hivyo haraka na kwamba watatumia ujuzi uliopo ili kukomesha kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Nchi hiyo ya Afrika Mashariki iliripoti mlipuko wa ugonjwa huo mara ya mwisho mwaka 2012. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## TANGAZO LA KUPOTELEWA KWA HATI YA KIWANJA

**FADHILA MAFIMBA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA HATI YA KIWANJA KILICHOPO MTAA WA WANDAMBA-MWEMBETOGWA-IFARAKA- KILOMBERO MMILIKI ZAMDA MBISHO
POLISI TAARIFA:
**IFA/RB/81/2018**

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

**KIZUMO OMARI KIZANGO**
ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI yenye namba za usajili **T 828 BZZ**
Chasis Namba: **2MZ2356944**
Engine Namba: **MCP600025923**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/371651/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EGBERTUS BUSIGAZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0189-0522 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FEZA BOYS SECONDARY SCHOOL** May, 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: DAR/MSI/RB/371173/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA MIKONGENI**
**WILAYA YA MVOMERO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......18/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU:**
**RAMADHANI SALUMU NG'ERUMBA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA OLIVER JOSEPH NG'ERUMBA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 09 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......20/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: DEOGRATIUS ABEDI MASALIKA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA SHAKILA BAKARI ISSA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 11 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 13 mwezi 09 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI YA TALAKA NA 06/2022**
**NANZIA LYIMO..........................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**GODWIN SAMWEL DOTTO................MJIBU MAOMBI**
**KWA: GODWIN SAMWEL DOTTO**

**POPOTE ULIPO,**

Unafahamishwa kwamba mwombaji katika shauri la madai ya talaka tajwa apo juu, amefungua shauri katika mahakama hii na sasa lipo katika hatua ya kutajwa. Hivyo shauri hilp limepangwa kutajwa tena mnamo **tarehe 28/09/2022** saa 02:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo ili shauri hili liweze kuendelea dhidi yako kama sheria inavyoelekeza.
**ZINGATIA KWAMBA,**kutokufika kwako tarehe iyo mahakama itaendelea na hatua inayofuata bila ya uwepo wako kwa kusikiliza shauri hili upande mmoja.
**IMETOLEWA,**na kutiwa saini na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 16/09/2022.

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**RAHMA HUSSEIN PAUL** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 417672** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 20/08/2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye.
**POLISI TAARIFA: MBD/RB/2988/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ERNEST LAMECK** anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato mcha nne chenye **Index NO. S0560-0149** kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia KASULU SECONDARY SHOOL mwaka 2007, Cheti cha Diploma in mechanical Engineering Chenye No. 0805015247 kilichotolewa na Dar- es- salaam Institute of Technology (DIT) mwaka 2012 Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **TAB/RB/8891/2015.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PEREPETUA ALEX SANGA** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye **index namba S.0278/0070** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IGUMBILO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba: **0768072911.** POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB/342077/2022**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Dully Sykes ataja waliomsumbua kwenye 'gemu'

**Na Mwandishi Wetu**

MKONGWE wa Bongo Fleva, Prince Dully Sykes, amefunguka kwa kuwataja wasanii wenzake watatu ambao walimsumbua sana wakati akitoka kwenye gemu hiyo.

Akihojiwa na kipindi cha Refresh, Dully alisema Inspekta Haroun, Juma Nature na TID walimsumbua mno hadi kuhisi kukonda, kwani kazi zao zilikuwa moto sana.

"Nilipata changamoto kubwa tatu, ya kwanza kabisa ilikuwa ni ujio wa Inspekta Haroun na ngoma yake ya 'Mtoto wa Getikali', ya pili ni Juma Nature na wimbo wa 'Jinsi Kijana' na ya tatu ni TID na wimbo wa 'Zeze'," alisema Sykes.

"TID ni moja kati ya watu ambao walinitingisha sana kipindi kile wakati naingia kwenye gemu.

"Aliingia na gia nzuri akatingisha, halafu yeye ndio akawa mara kwa mara anakwenda Ulaya.

"Kiukweli yeye ni mmoja wa wasanii walionipa changamoto kubwa sana, kwa sababu mimi nilijiona kama niko peke yangu kipindi kile."





# MOBETO HATAKI 'SHOBO' NA MTU

**Na Mwandishi Wetu**


MWANAMITINDO na msanii wa muziki, Hamisa Mobeto, amesema katika maisha yake ya sasa amechagua kuishi maisha kivyake.

Mobeto amesema kuwa, kwa kufanya hivyo ndiyo maana hapati shida yoyote kutoka kwa watu wanaomzunguka kwenye maisha yake.

Kupitia ukurasa wake wa instagram, Mobeto amedai anachopenda kwenye maisha yake ni kuishi bila 'stresi' kabisa na ndiyo maana maisha yake yanasonga na 'madili' yanazidi kuongeza kila kukicha kwa sababu moyoni ana furaha tele.

"Nimechagua kuishi maisha yangu, mimi na si vinginevyo ndiyo maana kila kukicha sichuji na sichukii hata kidogo," aliandika.

"Maisha yangu ni mazuri kwa maana nina furaha moyoni mwangu na nina amani siku zote," aliongeza Mobeto.



# *Rapa Cardi B akiri kufanya vurugu klabu*

**NEW YORK,** Marekani

RAPA wa kike wa Marekani, Cardi B, amekiri makosa mawili yaliyotokana na ugomvi katika klabu ya utupu, kama sehemu ya makubaliano ambayo yanamaanisha kuwa ataepuka kesi na kutofungwa jela.

Rapa huyo aliyeshinda tuzo ya Grammy, mzaliwa wa Belcalis Almanzar, alikiri kosa la shambulio na kusababisha hatari na alihukumiwa kifungo cha siku 15 kufanya kazi za huduma za kijamii.

Mashtaka mengine kumi yalitupiliwa mbali; "Nimefanya maamuzi mabaya katika siku zangu zilizopita ambayo siogopi kukabiliana nayo na kuyasimamia," alisema katika taarifa.

Mahakamani, nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, alikiri kuandaa na kushiriki katika mashambulizi mawili dhidi ya wafanyakazi wa klabu ya usiku ya Angels kule New York mwaka 2018.

Kwa mujibu wa mamlaka, matukio hayo yalikua ya ugomvi kati yake na wadada wawili mmoja wao alimshutumu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wake.

## HABARI MICHEZO

# WASHIRIKI 3,000 WAJISAJILI NMB MARATHON, JEZI HADHARANI

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya washiriki zaidi ya 3,000 kujisajili kushiriki Mbio za Hisani za NMB Marathon 2022, Benki ya NMB imeeleza sababu za kusogezwa mbele kwa mbio hizo, huku ikitambulisha medali na jezi zitakazovaliwa, pamoja na kumthibitisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuwa mgeni rasmi.

**NMB Marathon zitafanyika Oktoba Mosi, mwaka huu badala ya Septemba 24 kama ilivyokuwa imepangwa awali, zikianzia na kumalizikia katika viwanja vya Leaders Cub Kinondoni, Dar es Salaam, lengo likiwa kukusanya Sh. milioni 600 za kusaidia matibabu ya kinamama wenye fistula kwenye Hospitali ya CCBRT.**

Akizungumza wakati wa utambulisho wa fulana na medali hizo, Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay, alisema hadi jana asubuhi zaidi ya washiriki 3,000 walikuwa wamejisajili na kuwa vifaa 'kits' viliyoandaliwa kwa wakimbiaji hao ni vya ubora wa kimataifa.

Alibainisha kuwa, katika kujiweka sawa kwa mbio hizo, NMB ilifanya bonanza la NMB na wabunge wiki jana, ambalo wamelitumia kama maandalizi, ushawishi na mialiko kwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili waweze kuwa sehemu ya washiriki wa mbio hizo.

"Tunaamini wabunge hao ni miongoni mwa watakaonufaika na uamuzi huu wa kusogeza mbele, ambao umetokana na maombi ya wengi miongoni mwa Watanzania, kututaka tusogeze ili waweze kushirikiana nasi katika tukio hili, linaloenda kurejesha tabasamu kwa kinamama wenye fistula.

"Kwa hiyo usajili unaendelea Mbezi Beach, Juliana Pub iliyopo Mtana Bar pale Kanisa la St. Peters, Mlimani City na kwenye tovuti ya marathon.nmbbank.co.tz. Watanzania wazidi kujisajili na waliofanya hivyo tayari, wafike kuanzia kesho (leo) Mlimani City kuchukua 'kits' (vifaa) vyao," alifafanua Akonaay.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya NMB Marathon, Mercy Nyange, alibainisha kwamba benki yao inashukuru kupata wadhamini wengi waliojitokeza kudhamini mbio hizo ili kuunga mkono jitihada za kulikomboa kundi la kinamama, wanaokabiliwa na changamoto hiyo.

Mercy aliwaomba Watanzania waliomba kuongezwa kwa muda wa usajili kujitokeza na kwamba udhamini mnono kutoka Sanlam, UAP, Toyota na kampuni nyinginezo, unawahakikishia zawadi nzuri kwa washindi wa kwanza hadi wa 10 kwa mbio zote, kilomita tano, 10 na 21, pamoja na mbio za watoto.

"Niweke msisitizo tu, kama ilivyosemwa washiriki zaidi ya 3,000 wamejisajili hadi sasa, kwa hiyo fursa hii iliyoombwa itumiwe vizuri na watu wajitokeze kujisajili katika maeneo yaliyotajwa hapo juu," alisisitiza Mercy.




Ofisa Mkuu Raslimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonnay (wa pili kushoto), Mkuu wa Idara ya Bima, Martine Massawe, Mwenyekiti wa Kamati ya Maaandalizi ya NMB Marathon, Mercy Nyange (kulia) na kushoto ni Nahodha Msaidizi wa NMB Jogging Club, Stella Motto wakionyesha jezi na medali zitazotumika kwenye Mbio za NMB Marathon zitakazofanyika Oktoba Mosi, mwaka huu katika viwanja vya Leaders Club, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# *Mafunzo yapania kuzindukia kwa Mlandege*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Mafunzo SC, Abdallah Bakari 'Edo', amesema licha ya kushindwa kuibuka na ushindi katika mechi zote tatu walizocheza msimu huu wa Ligi Kuu Zanzibar, bado anaimani timu hiyo itafanya vizuri katika michezo inayofuata hususan Jumamosi itakapovaana na Mlandege.

Katika mechi tatu ilizocheza hadi sasa, Mafunzo imepoteza moja na kutoka sare mbili, hivyo kujikusanyia pointi mbili tu zinazoifanya kushika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Baada ya kuanza kwa sare mbili mfululizo msimu huu, juzi Mafunzo ilianza kuonja machungu ya kipigo kwa kutandikwa mabao 2-0 dhidi ya Kundemba FC kwenye mchezo uliochezwa Uwanja wa Amaan majira ya saa 10 alasiri.

Katika mchezo huo, mabao ya Kundemba yalizamishwa nyavuni na Nassor Ali dakika ya 13 na Fahm Salum dakika ya 86.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo alisema kupoteza katika michezo hiyo haina maana kama timu yao haikuandaliwa vizuri, bali ni kawaida katika mpira hutokea mambo kama hayo hasa katika michezo ya kwanza ya ligi ambayo kila timu inaweka utayari wa kufanya vizuri.

Alisema Mafunzo SC ina wachezaji wazuri na wanaojituma, hivyo yapo mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ili timu ipate ushindi.

Edo alisema miongoni mwa mambo watakayoenda kuyafanyia kazi ni pamoja na safu ya ulinzi na ushambuliaji ili kuongeza umakini wanapokuwa katika sehemu sahihi ya kucheka na nyavu.

"Katika michezo hii mitatu tuliyocheza, tumeona mapungufu kadhaa, ikiwamo walinzi wetu kutokuwa makini, lakini washambuliaji wetu kukosa magoli ya wazi kabisa, hivyo lazima wachezaji tuwafunze kujiamini pale tunapolishambulia goli la wapinzani wetu, pia walinzi wawe makini pale tunaposhambuliwa," alisema.

Aidha, alisema sasa wanajipanga kupata ushindi katika mchezo wao wa nne wa ligi hiyo watakapovaana na timu ya Mlandege Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Amaan majira ya saa moja usiku.

# TBS waaswa kuendeleza utamaduni wa mazoezi

Na Mwandishi Wetu

WAFANYAKAZI wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wametakiwa kuendeleza utamaduni wa kushiriki michezo ili kujenga afya zao, kwani huo ndio mtaji mkubwa wa kufanya kazi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TBS, Rwalib Mmbaga, wakati akifungua mashindano ya michezo mbalimbali yaliyoandaliwa na shirika hilo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Alisema kwa maendeleo ya teknolojia ambayo dunia imefikia kwa sasa, ni wazi kwamba afya za watu ziko hatarini kutokana na kuongezeka kwa vyombo vya usafiri.

Hata mtu asiye na gari anatumia bodaboda na hata mtu akitaka fedha kutoka benki anazipata hapo hapo akiwa nyumbani kupitia simu, hivyo watu hawana muda wa kutembea.

"Ukiwa ofisini kazi nyingi zinafanyika kwa njia ya mtandao, ukitoka ofisini unapanda gari lako na kurudi nyumbani, kwa hiyo muda wa kufanya mazoezi unakuwa ni mdogo," alisema.

Aliipongeza menejimenti ya TBS kwa kuanzisha utaratibu huo kwani michezo inajenga afya na kuwafanya wafanyakazi kuwa sehemu ya familia moja.

Alishauri michezo hiyo ipanuliwe zaidi kwa kuwashirikisha wafanyakazi wa shirika hilo wanaofanya kazi kwenye kanda mbalimbali nchini.



Alisema anajua kwamba si rahisi kuwashirikisha wafanyakazi wote, lakini wanaweza kuleta wawakilishi ili waweze kujumuika na wafanyakazi wa makao makuu kushiriki michezo hiyo.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya (pichani), alisema mwaka huu ni mwaka wa tatu michezo hiyo kufanyika lengo likiwa ni kuwaweka karibu wafanyakazi pamoja na kujenga afya zao.

"Kwa hiyo hii ni njia mojawapo ya kuwafanya wafanyakazi wafahamiane na kujenga afya zetu, kwani afya ni mtaji muhimu sana katika maisha ya kila siku," alisema.

Alitoa wito kwa jamii na taasisi zote nchini kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi ili kulinda afya.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POTTER AMTAKA KANE

KOCHA wa Chelsea, Graham Potter, anataka kumnunua nyota wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29. ***(Calciomercato)***

### MUDRYK ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanavutiwa na winga wa Shakhtar Donetsk, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, ambaye anafananishwa na Neymar. ***(Calciomercato)***

### RODGERS HAFUKUZWI

KLABU ya Leicester haiwezi kumfuta kazi kocha, Brendan Rodgers kwani itawagharimu pauni milioni 10 kumlipa. ***(Sun)***

### WATATU WATAJWA LEICESTER

KAMA Leicester City itamfuta kazi Brendan Rodgers, makocha wapya wanaotajwa kuchukua nafasi yake ni Mauricio Pochettino, Rafael Benitez na Sean Dyche. ***(Sun)***

### GOMES AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanamfuatilia kiungo wa kati wa Flamengo, Joao Gomes mwenye umri wa miaka 21, huku Jurgen Klopp akitafuta msaada katika eneo hilo lenye tatizo. ***(Talksport)***

### PAVARD AWINDWA CHELSEA

MLINZI wa Ufaransa, Benjamin Pavard anafikiria kuondoka Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto, huku Manchester United, Chelsea, Paris St-Germain, Atletico Madrid na Juventus zikitaka kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Telefoot, via Standard)***

### MABOSI WATOFAUTIANA UTD

MABOSI wa Manchester United wamegawanyika katika sera ya uhamisho, huku Kocha Mkuu, Erik ten Hag akitaka kufanya usajili zaidi Januari, lakini Mtendaji Mkuu, Richard Arnold anataka kusubiri hadi majira ya joto. ***(The Athletic)***

### KNAUFF AWINDWA EPL

KLABU za Ligi Kuu England ambazo hazijatajwa, zinamuwania winga wa Eintracht Frankfurt, Ansgar Knauff mwenye umri wa miaka 20, huku akifananishwa na Arjen Robben. ***(Sport1)***

### LANZINI RUKSA KUONDOKA

WEST Ham wamemwambia winga wa Argentina, Manuel Lanzini mwenye umri wa miaka 29, kuwa yuko huru kuondoka Januari. ***(Football Insider)***

### ASENSIO BILA MALIPO

BARCELONA wana nia ya kumsajili winga wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio, 26, kwa uhamisho wa bila malipo mkataba wake utakapomalizika msimu ujao. ***(Mundo Deportivo)***

### SUAREZ MSIMU MMOJA

MCHEZAJI wa kimataifa wa Uruguay, Luis Suarez atatumia msimu mmoja pekee nchini kwao na klabu ya Nacional, huku rais wa klabu hiyo akithibitisha kuwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ataondoka mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LALIGA YALAANI MASHABIKI WA ATLETICO KUMBAGUA VINICIUS

**MADRID,** Hispania

LIGI Kuu ya Hispania, LaLiga, imelaani unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi aliofanyiwa Vinicius Junior na mashabiki wa Atletico Madrid kabla ya mechi ya Jumapili kwenye Uwanja wa Civitas Metropolitano.

**Real Madrid ilishinda 2-1 kwa mabao ya Rodrygo na Federico Valverde, huku Mario Hermoso akifunga la kufutia machozi.**

Hilo liliihakikishia Real Madrid kukaa kileleni wakati wakielekea kwenye mapumziko ya mechi za kimataifa, lakini mechi hiyo iligubikwa na vitendo vya kibaguzi kwa baadhi ya mashabiki wa Atletico.

Kundi kubwa lilionyeshwa kwenye video likiimba nyimbo za ubaguzi wa rangi kuhusu Vinicius nje kidogo ya uwanja kabla ya mchezo.

Mbrazil huyo alikuwa gumzo kabla ya mchezo baada ya wakala wa soka wa Hispania, Pedro Bravo kumwambia "acha kucheza kitumbili" kwenye kipindi cha televisheni cha El Chiringuito kuhusiana na tabia yake ya kucheza dansi anapoPsherehekea bao.

Bravo aliomba radhi na kusisitiza kuwa haikuwa nia yake kumbagua.

Wakati wa mchezo wa Jumapili, pia kulikuwa na ripoti za nyimbo za kibaguzi zikitokea ndani ya uwanja, ingawa matukio mabaya ya kabla ya mchezo tayari yalikuwa yametokea kutokana na video nyingi kuwekwa kwenye mitandao ya kijamii zikimzihaki. Msemaji wa LaLiga alisema: "Tunakemea matukio yote ya ndani na nje ya viwanja. Tunashirikiana na klabu kuweka soka letu kuwa la kirafiki na kufurahisha.

●●● Tunakemea matukio yote ya ndani na nje ya viwanja, matamshi ya chuki hayana nafasi...

"Matamshi ya chuki hayana nafasi kwenye LaLiga na kila mara tunashirikiana na klabu na mamlaka kubaini na kufikisha mahakamani kesi yoyote kama hiyo."

Mashabiki wa Atletico pia walirusha vitu uwanjani wakati Vinicius na Rodrygo wakicheza walipokuwa wakishangilia bao la kwanza la Madrid.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 346,

MECHI KALI

GEITA GOLD FC
VERSUS
SINGIDA BS FC


1 | 1.58
X | 3.58
2 | 5.30

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HUGO LLORIS KUWAKOSA ARSENAL




**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kumkosa mlinda mlango wake, Hugo Lloris, kwenye mechi ya dabi ya London Kaskazini dhidi ya Arsenal, Oktoba Mosi, mwaka huu kwa mujibu wa jarida la France Football.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 35, aling'ara sana wakati Spurs iliposhinda mabao 6-2 dhidi ya Leicester wikendi iliyopita, huku akizuia mpira wa kichwa uliopigwa na Patson Daka kipindi cha pili na kuwazuia 'Mbweha' hao kufanya matokeo kuwa 3-3.

Lloris alijiunga na timu ya Taifa ya Ufaransa Jumatatu kuelekea mechi za wiki hii za Ligi ya Mataifa Uefa dhidi ya Austria na Denmark, lakini ameondolewa kambini kule Clairefontaine.

Amegundulika kuwa na jeraha kwenye paja lake la mguu wa kulia, ambalo litamfanya kocha wa Spurs, Antonio Conte kutafuta mbadala wake kwenye safari ya kwenda kuivaa Arsenal, Oktoba Mosi.

"Alipowasili Jumatatu asubuhi katika Kituo cha Kitaifa cha Soka Clairefontaine, Hugo Lloris alikuja na daktari Franck Le Gall," ilisema taarifa kutoka Shirikisho la Soka la Ufaransa ikinukuliwa na Jarida la France Football.

"Jeraha dogo la paja la mguu wa kulia limegunduliwa kwa kipa wa Tottenham. Kwa hiyo hayupo kwenye mechi mbili dhidi ya Austria siku ya Alhamisi kule Stade de France na Denmark siku ya Jumapili."



## *Kounde aanika sababu kuikataa Chelsea ya Tuchel*

**BARCELONA,** Hispania

JULES Kounde amesema aliamua kuchagua kujiunga na Barcelona badala ya Chelsea kwa sababu "nilipenda zaidi mazungumzo ya Xavi" kuliko ya Thomas Tuchel.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alionekana kuwa tayari kusaini Chelsea wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto, lakini akaamua kwenda kule Camp Nou alikosaini mkataba wa miaka mitano.

Mkurugenzi wa soka wa Sevilla, Monchi alidai kuwa wakati huo Barca wanamchukua Kounde ni baada ya Chelsea kuondoa ofa yao kutokana na "kuwa na mashaka".

Hata hivyo, katika mahojiano na jarida la L'Equipe la Ufaransa, Kounde amesisitiza kuwa uamuzi huo ni wake mwenyewe baada ya kubembelezwa na Kocha Mkuu wa Barca, Xavi.

"Kwanza, nimekuja kwenye klabu kubwa, ambayo imejua nyakati nzuri," alisema Kounde.

"Ninakuja kwenye mradi ambao singeuita ujenzi mpya, kwa sababu tayari tuna timu ya ushindani.

"Nilikuwa na nia ya kuwa sehemu ya wimbi hili jipya, kusaka mataji, na kuirejesha Barca pale ambapo imekuwa siku zote, miongoni mwa klabu bora zaidi duniani.

## HABARI MICHEZO

,249,820

# MAYAY KAIMU MKURUGENZI MPYA WA MICHEZO NCHINI

**Na Shufaa Lyimo**

NGULI wa soka wa zamani wa Yanga na Taifa Stars, ambaye ni mchambuzi mashuhuri wa soka, Ally Mayay Tembele, amteuliwa na serikali kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini.

Uteuzi huo umefanywa na Waziri mwenye dhamana ya Sanaa Utamaduni na Michezo Mohamed Mchengerwa, baada ya aliyekuwa Mkurugenzi wa nafasi hiyo, Yusuph Singo kupangiwa majukumu mengine.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, John Mapepele, imeeleza Mayay ambaye alikuwa Ofisa Mwandamizi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini, atashikilia nafasi hiyo huku taratibu nyingine zikiendelea.

**"Mayay ambaye ni Ofisa Mwandamizi katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndge nchini, amehamishiwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuruhusiwa kukaimu majukumu haya kwa mujibu wa kibali cha Ofisi ya Rais Utumishi," ilieleza taarifa hiyo.**

Ilisema uteuzi huo umeanza rasmi tangu jana na kuwaomba wadau wa michezo kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha, ilieleza lengo la uteuzi huo ni kuimarisha utendaji kwenye sekta ya michezo nchini.

Kwa upande wa Singo, alisema ni jambo la kawaida serikali kufanya mabadiliko na kudai Mayay anauzoefu mkubwa kwenye michezo.

"Ninaomba Watanzania wampe ushirikiano kiongozi mpya aliyeteuliwa kukaimu nafasi yangu, ni kiongozi mwenye weledi mzuri wa kufanya kazi," alisema Singo.

Alisema kwa sasa ni mapema kuzungumzia majukumu aliyopewa na kudai mipango ikikaa sawa ataeleza hapo baadaye.

**MSHINDI...**



Meneja wa Masuala ya Burudani wa Micasa Lounge & Bar, James Pokoso (kushoto), akitoa zawadi ya jezi zenye thamani ya Sh. 200,000 kwa Meneja wa Timu ya U.N Veteran, Jeremiah Jeuri (wa pili kushoto), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya timu hiyo kuibuka mshindi wa mashindano ya mpira wa miguu ya Veteran Afya Bonanza. Kulia ni mratibu wa mashindano hayo ambaye ni Mkurugenzi wa Iron Digital Marketing, Eric Furaha na Kocha wa timu hiyo, Fikiri Christopher. **PICHA: MPIGAPICHA WETUJUMA**

## *Morrison: Al Hilal watang'oka*

INATOKA UKURASA 32

Nabi alisema wachezaji wake watakuwa wanafanya mazoezi na kurudi nyumbani hadi mwisho wa mwezi huu watakapoingia kambini kujiandaa na mechi hiyo ambayo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu ya Al Hilal kuwa na uzoefu wa muda mrefu katika michuano hiyo.

"Tumepata matokeo mazuri mechi iliyopita, ila kuna mapungufu tumeyaona ikiwamo safu ya ushambuliaji kwa kutengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia, sasa tunarudi uwanjani kufanyia kazi hilo na mechi yetu dhidi ya Ruvu Shooting itatupa taswira ya mchezo wetu wa kimataifa," alisema Nabi.

## Phiri: Kwa 'mipasi' ya Chama

INATOKA UKURASA 32

na hivi sasa anarejea kwenye kiwango chake kilichozoeleka, ni mtu ambaye huwa anampa pasi straika kutokana na uwezo wake au jinsi ya mikimbio yake. Anajua kila mmoja anahitaji pasi ya aina gani, inategemea tu na wewe ulivyo.

"Ukiona Chama ana mpira, basi wewe straika kimbilia tu kwenye eneo la hatari atakupa kulingana na jinsi ulivyojipanga, au unavyotaka uletewe, ukiwa huna kasi atakupa ya aina hiyo na kama una kasi atakutumbukizia hivyo kwa sababu anajua utaukuta tu," alisema Phiri.

Alisema kwake yeye anaweza kumfanya afunge mabao mengi kwa sababu pasi zake ni za kuelekeza nini cha kufanya.

Kwa sasa Phiri amejipambanua kuwa straika namba moja wa Simba akichukua taratibu nafasi ya Meddie Kagere aliyeachwa msimu huu na kutimkia Singida Big Stars.

Tayari, Phiri amefunga mabao matatu mpaka sasa kwenye Ligi Kuu na idadi kama hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

## JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/22 | 20:30 | Bastia Borgo vs Le Mans | 2.78 | 3.13 | 2.46 |
| 02. 23/09/22 | 20:30 | Saint Brieuc vs Orleans | 2.48 | 3.15 | 2.75 |
| 03. 23/09/22 | 20:30 | Villefranche Sur Saone vs Bourg Peronnas | 2.35 | 3.14 | 2.94 |
| 04. 23/09/22 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Avranches | 2.63 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 23/09/22 | 20:30 | FC Versailles 78 vs Nancy | 2.32 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/09/22 | 20:30 | Sedan vs Le Puy | 2.34 | 3.15 | 2.95 |
| 07. 23/09/22 | 21:00 | Ireland U21 vs Israel U21 | 2.27 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 23/09/22 | 21:45 | Italy vs England | 2.62 | 3.17 | 2.68 |
| 09. 23/09/22 | 21:45 | Finland vs Romania | 2.29 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 23/09/22 | 21:45 | Alloa Athletic vs Airdrieonians | 2.43 | 3.63 | 2.43 |
| 11. 23/09/22 | 22:00 | Dordrecht vs Maastricht | 2.33 | 3.53 | 2.68 |
| 12. 23/09/22 | 22:00 | Morocco vs Chile | 2.70 | 3.27 | 2.60 |
| 13. 23/09/22 | 22:00 | The New Saints vs Dundee FC | 2.64 | 3.57 | 2.27 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 21/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1142 | Cerezo Osaka vs Urawa Red Diamonds | 2.47 | 3.06 | 2.72 |
| 13:00 | 1611 | Anyang vs Daejeon Citizen | 2.35 | 3.29 | 2.70 |
| 13:00 | 3084 | Avispa Fukuoka vs Sanfrecce Hiroshima | 3.58 | 3.19 | 1.97 |
| 13:00 | 4068 | V Varen Nagasaki vs Tochigi SC | 2.38 | 2.84 | 3.04 |
| 13:00 | 5170 | Mito Hollyhock vs Tokyo Verdy | 2.17 | 3.28 | 2.99 |
| 13:30 | 4913 | Seoul E Land vs Gyeongnam | 2.56 | 3.20 | 2.51 |
| 15:00 | 4684 | Vietnam vs Singapore | 1.44 | 4.27 | 7.74 |
| 15:00 | 5285 | Wigan U23 vs Sheffield United U23 | 2.46 | 3.64 | 2.38 |
| 16:00 | 4368 | Geita Gold FC vs Singida BS FC | 1.57 | 3.67 | 5.29 |
| 16:30 | 2133 | MFK Snina vs FC KoÅiice | 7.63 | 5.29 | 1.28 |
| 16:30 | 2270 | Tj Slovan Bystricka vs Povazska Bystrica | 17.69 | 10.81 | 1.05 |
| 16:30 | 2716 | Rimavska Sobota vs Dukla Banska Bystrica | 12.72 | 8.02 | 1.12 |
| 17:00 | 1342 | Al Ahli Amman vs Al-Jalil | 2.65 | 3.19 | 2.45 |
| 17:00 | 1369 | MSK Thermal Velky Meder vs MFK Skalica | 14.66 | 10.75 | 1.07 |
| 17:00 | 2869 | Al-Arabi vs AL Hashemeya | 3.39 | 3.39 | 1.96 |
| 17:00 | 3400 | Alia Club vs Baalama | 2.10 | 3.28 | 3.14 |
| 17:00 | 3866 | Sama AL Sarhan vs Ittihad AL Ramtha | 2.05 | 3.14 | 3.39 |
| 17:00 | 5013 | Tigres U20 vs Necaxa U20 | 1.88 | 3.72 | 3.33 |
| 17:00 | 5029 | KFC Kalna Nad Hronom vs Spartak Myjava | 5.69 | 4.61 | 1.41 |
| 17:00 | 5871 | FK Nove Zamky vs FC Stk 1914 Samorin | 5.69 | 4.61 | 1.41 |
| 17:45 | 4644 | Esteghlal Khuzestan vs Mes Shahr-e Babak | 2.10 | 2.70 | 4.30 |
| 18:00 | 1298 | Belarus U19 vs Slovakia U19 | 3.29 | 3.43 | 1.98 |
| 18:15 | 2802 | Al Salmiyah vs Burgan SC | 1.56 | 3.92 | 4.90 |
| 18:15 | 3189 | Al Kuwait SC vs Yarmouk | 1.41 | 4.51 | 5.88 |
| 18:30 | 1826 | Sporting Gagnoa vs FC San Pedro | 2.59 | 2.98 | 2.64 |
| 19:00 | 5238 | Bosnia & Herzegovina U19 vs Poland U19 | 3.33 | 3.43 | 1.97 |
| 19:30 | 1812 | AS Ashdod vs Hapoel Afula | 2.56 | 3.16 | 2.76 |
| 19:30 | 5408 | Bnei Yehuda vs El Fahem | 2.44 | 2.89 | 3.19 |
| 19:30 | 5952 | Maccabi Petach Tikva vs Hapoel Petah Tikva | 1.54 | 3.92 | 6.04 |
| 20:00 | 1406 | Kray vs MSV Dusseldorf | 2.85 | 3.70 | 2.17 |
| 20:00 | 2087 | AD Grecia vs AD Guanacasteca | 1.95 | 3.44 | 3.39 |
| 20:00 | 2363 | Pirmasens vs Kaiserslautern II | 1.65 | 4.32 | 3.83 |
| 20:00 | 3301 | Schwarz-Weiss Essen vs TVD Velbert 1870 | 2.16 | 3.45 | 3.05 |
| 20:00 | 4612 | Municipal Turrialba vs CD Escorpiones Belen | 3.00 | 3.50 | 2.08 |
| 20:00 | 4816 | Futbol Consultants Moravia vs Municipal Santa Ana | 2.29 | 3.33 | 2.75 |
| 20:00 | 5203 | Latvia U19 vs Romania U19 | 9.78 | 4.60 | 1.28 |
| 20:30 | 2394 | 1.fc Monheim vs Cronenberger SC | 1.39 | 5.20 | 6.00 |
| 20:30 | 3008 | VfB 03 Hilden vs FSV Duisburg | 1.05 | 10.87 | 18.77 |
| 20:30 | 3338 | 1 FC Kleve vs SV Sonsbeck | 1.69 | 4.40 | 3.85 |
| 20:30 | 3522 | VfB Homberg vs Sportfreunde Baumberg | 2.26 | 4.31 | 2.35 |
| 20:30 | 3794 | SF Hamborn 07 vs Ratingen SV | 6.00 | 5.00 | 1.40 |
| 20:30 | 3955 | Turu Dusseldorf 1880 vs Spvg Schonnebeck 1910 | 2.34 | 3.50 | 2.70 |
| 20:30 | 5988 | Northern Ireland U19 vs Slovenia U19 | 3.10 | 3.59 | 2.01 |
| 21:00 | 3506 | K Bocholter VV vs MSK Deinze | 8.35 | 5.77 | 1.26 |
| 21:45 | 2321 | Kingstonian vs Bognor Regis | 2.21 | 3.44 | 2.80 |
| 21:45 | 4689 | Cray Wanderers vs Hastings United | 1.74 | 3.63 | 4.02 |
| 21:45 | 4696 | Scotland vs Ukraine | 2.51 | 3.08 | 2.88 |
| 22:00 | 4475 | Club Cortulua vs Deportivo Cali | 2.50 | 3.04 | 2.70 |
| 23:00 | 3656 | Uruguay De Coronado vs San Jose FC | 1.91 | 3.75 | 3.50 |
| 23:00 | 4521 | AD Aserri vs AD Cariari Pococi | 1.97 | 3.58 | 3.19 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatano Septemba 21, 2022

Nipashe



LaLiga yalaani Vinicius kubaguliwa UKURASA 29

# Morrison: Al Hilal watang'oka CAF

●●● Adai amerejea rasmi dimbani kwa kazi hiyo, Nabi naye asema atatesti mitambo kwa...

**Na Saada Akida**

WINGA machachari wa Yanga, Bernard Morrison baada ya kukosekana katika michezo miwili ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, amesema yupo fiti kurejea uwanjani kuisaidia timu yake katika michuano hiyo ya hatua inayofuata dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

**Morrison hakuonekana katika michezo hiyo miwili kutokana na kusumbuliwa na majeraha, lakini Yanga ilifanikiwa kutinga raundi ya kwanza kwa ushindi wa jumla wa mabao 9-0, ikishinda 4-0 mechi ya kwanza na 5-0 ya marudiano.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Morrison alisema amepona na kurejea uwanjani hivi karibuni, hivyo kwa kushirikiana na wenzake atahakikisha anapambana kuisaidia timu yao kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa hadi kufikia malengo yao.



Alisema malengo yao makubwa ni kuona Yanga inacheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo na anaimani hilo litafanikiwa kwa sababu ya ubora wa kikosi cha timu yao.

"Ni kweli sijaonekana uwanjani kwa sababu ya majeruhi na sasa niko vizuri, nimeanza mazoezi na nitarudi uwanjani kupambania timu kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Morrison.

Wakati Morrison akishuka na 'mistari' hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (pichani), ameweka wazi kuwa atatumia mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting kurekebisha madhaifu yao kuelekea mchezo huo dhidi ya Al Hilal watakaoanzia nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa Oktoba 8, mwaka huu.

Kabla ya kucheza mchezo huo Oktoba 3, Yanga itacheza mchezo wa tano wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kikosi chake kinaanza mazoezi leo kujiandaa na michezo mitatu iliyo mbele yao huku akiitumia mechi yao dhidi ya Ruvu Shooting kujiimarisha na kufanyia kazi mapungufu yao kabla ya kukutana na Al Hilal.

Alisema Ruvu Shooting si timu mbaya, lakini kwa kuwa wanakwenda katika mashindano makubwa wanapaswa kuwa na mchezo kabla ambao utampa majibu ya nini anatakiwa kufanya.

"Katika michezo yote hii tunahitaji ushindi, mchezo dhidi ya Ruvu Shooting tutatakiwa kupambana kupata mabao mengi ili niweze kuona mapungufu yaliyopo hasa ukiangalia tutakuwa tumetoka kwenye mapumziko kutokana na michezo ya timu za taifa," alisema Nabi.

Alisema mazoezi wanayofanya yatakuwa wanayatumia kumaliza mapungufu yao ili kuandaa kikosi imara kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wao dhidi ya Al Hilal ili kufikia malengo yao ya kucheza robo fainali ya michuano hiyo.

INAENDELEA UK. 31



Bernard Morrison akifanya vitu vyake katika moja ya mechi za Yanga. **PICHA: MAKTABA**

## Phiri: Pasi za Chama ni mabao tu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Moses Phiri ameeleza kufurahishwa na kiwango cha Mzambia mwenzake, Clatous Chama na kusema kuwa pasi zake zitamfanya aweze kufunga mabao mengi.

Phiri aliyecheka na nyavu mara tatu kati ya ushindi wa jumla wa mabao 4-0 wakati wakitoa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwenye hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, amesema Chama kwa sasa amerejea kwenye kiwango chake cha kawaida na atakuwa msaada mkubwa kwa timu, pamoja na wachezaji wenzake.

Nyota huyo wa Zambia, Phiri alifunga bao moja wakati Simba ikishinda 2-0 ugenini kabla ya Jumapili iliyopita kutupia yote mawili na kuwezesha Simba kushinda mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Kwanza kabisa nimefurahi kwa kufunga mabao na kuiwezesha timu kupata ushindi na kusonga mbele kwenye hatua inayofuata. Pia nawashukuru mashabiki wengi waliojitokeza kutupa sapoti, kusema kweli hii inatufanya wachezaji kucheza kwa bidii na kujituma kwa ajili ya mashabiki," alisema Phiri baada ya mchezo huo.

Kuhusu pasi mpenyezo ya Chama iliyosababisha kufunga bao la kwanza, Phiri alimsifu na kumtaja kama ni 'Master' wa kupiga pasi za mwisho.

"Chama ni 'Master', kila mtu anamfahamu, sidhani kama kuna mtu hafahamu uwezo wake,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >